ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae
56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali	-	Jimbo la Uzini

57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	-	Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	-	Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa	-	Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa	-	Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	-	Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis	-	Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini	-	Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy	-	Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali	-	Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid	-	Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi	-	Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa	-	Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said	-	Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said	-	Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma	-	Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal	-	Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali	-	Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said	-	Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya	-	Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali	-	Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said	-	Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi	-	Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla	-	Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir	-	Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum	-	Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar	-	Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem	-	Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tano – Tarehe 21 Febuari, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Omar Seif Abeid (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuweka mezani Muhutasari wa Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 78

Ubovu wa Barabara ya Msingini – Chake Chake

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Serikali ya Mapinduzi ina nia nzuri katika kuendeleza miji yake yote ya Zanzibar na katika mji wa Chake Chake ipo barabara moja ya Msingini ambayo ni moja ya kero kubwa za mji huo na Serikali imeshatoa ahadi za kujenga barabara hiyo.

(a) Jee, ni lini barabara ya Msingini itaanza kufanyiwa matengenezo.

(b) Ni lini upimaji wa barabara hiyo utaanza kwa kuonesha upana wa barabara hiyo na wale waliozidisha nyumba zao mbele ya barabara waweze kurekebisha nyumba zao kabla ujenzi haujaanza ili kuondoa usumbufu.

(c) Barabara ya Msingini ilikuwa njia moja *one way* ya kutoka Chachani kuelekea Kilimatinde. Jee, hivi sasa inaweza kubadilika matumizi ikawa ya kwenda na kurudi ili kukuza barabara hiyo kibiashara.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwanza naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, barabara ya Msingini iliyopo Mjini Chake Chake ni barabara ya ndani yaani *feeder road* yenye urefu wa kilomita 0.5, barabara hii ilikuwa ya kiwango cha lami, hata hivyo hivi sasa tayari imechakaa sana baada ya kutokufanyiwa matengenezo kwa muda mrefu. Kwa kutambua umuhimu wa barabara za ndani kijamii na kiuchumi, ofisi yangu inaendelea kufanya kazi ya usanifu (*design)* wa kina barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 50 kwa Unguja na Pemba ikiwemo barabara ya Msingini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo mafupi sasa naomba kumjibu kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa barabara ya Msingini tayari imeshafanyiwa usanifu wa kina hivyo matengenezo yake yatafanyika kama itakavyopangwa katika mpango wa miaka mitano wa matengenezo ya barabara za ndani. Uandaaji wa mpango huo utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa kazi ya usanifu wa barabara zote za ndani zilizomo katika mpango huo Unguja na Pemba.

(b) Mhe. Mwenyekiti, upimaji wa barabara ya Msingini utaanza mara tu baada ya kukamilika kwa mpango wa miaka mitano wa matengenezo ya barabara za ndani. Wakati huo huo alama zitawekwa ili kuwatanabahisha wananchi kwa usahihi wapi barabara itapoanzia na itapomalizikia kwa urefu na upana.

(c) Kwa kuwa matumizi ya asili ya barabara hii ni ya njia moja pekee na kwa kuwa matengenezo yanayotarajiwa kufanywa hayatahusisha utanuzi wa barabara iliyopo sasa, hivyo basi matumizi ya barabara ya Msingini yataendelea kuwa ya njia moja kutoka Chachani kuelekea Kilimatinde.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza lazima nimpongeze Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dr. Ali Mohamed Shein, Balozi Seif Ali Iddi pamoja na watendaji akina Mhe. Haji Omar Kheri, Mhe. Salama Aboud Talib, Mhe. Mohamed

Aboud, Dr. Mohd wa Mipango Miji, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Mwanasheria Mkuu (*AG*) kwa kukubali kwamba Mji wa Chake Chake sasa hivi unakuwa mji mkuu namba mbili kwa Zanzibar. Kwa hivyo, hilo lazima niwapongeze sana kwa.....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa twende kwenye swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nina swali ninataka kumuuliza kuwa:-

(a) Kutokana na hadhi ya mji huu ambao tunaupandisha. Jee, huoni umuhimu wa barabara hii kutanuliwa kidogo angalau ikaweza kupita kwenda na kurudi ili angalau mji ule ukapata hadhi yake.

(b) Ni lini kutokana na ahadi nyingi zilikuwa Wizara ya Ujenzi sasa hivi imekuwa Serikali za Mitaa na Idara Maalum, hii ni lini barabara hii itaanza rasmi kwa kujengwa na pia uko tayari kufuatana mguu kwa mguu mimi na wewe kupita barabara ya Msingini kuona hali halisi kabla ya ujenzi ili kutafakari na kuona mji wetu tunautekelezaje.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali la nyongeza lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la umuhimu kweli na mimi nikubaliane kwamba umuhimu ambao ameusema Mhe. Mwakilishi niseme kwamba na mimi bado naona kwamba umuhimu upo. Lakini sambamba na umuhimu wa barabara hii na vile kutaka kuona ushauri kwamba barabara ile inatanuliwa zaidi, nadhani lazima tuangalie msingi wetu wa fedha. Msingi wetu wa fedha ni kwamba tunatengeneza barabara ya ndani. Fedha ambazo tunazipata zinaweza zikawa na ugumu katika kufanya utanuzi wa barabara hiyo kwa sababu ukiangalia majengo yaliopo ni ya gharama kubwa na ambayo kwa kiasi fulani kwa uwezo wetu sisi na nafasi zetu sisi ni majukumu yetu sisi haitoweza kukidhi mahitaji ya malengo yaliyokusudiwa.

(b) Ni lini ujenzi kuanza. Mhe. Mwenyekiti, katika jibu langu la msingi nimesema kwamba hii baada ya kukamilisha utaratibu wa kufanya *design* na sio kwa Msingini tu na barabara nyengine ambazo tumezieleza kilomita 50 ambazo ni *feeder road* nazo tukamilishe.Sambamba na hilo itategemea na upatikanaji wa fedha. Kadri fedha zitakapopatikana kwa wakati na ndio hivyo

hivyo na sisi tunasema kwamba shughuli ya kuitanua barabara au kuifanyia marekebisho kuitengeneza barabara hii ndio utaendana sambamba na upatikanaji wa fedha.

(c) Mhe. Mwenyekiti, kutaka kwamba tufatane mguu kwa mguu kwenda kuangalia hali halisi ya barabara ilivyo, naona kwamba hilo kwa upande wetu sisi halina tatizo nakubalina naye Mheshimiwa kwamba tuko tayari kufanya hivyo. Lakini sio kwamba fursa hiyo mimi tayari mimi mwenyewe binafsi nimeshakwenda kujiona hali halisi barabara hiyo mimi naifahamu kuanzia mwanzo na mwisho na hiyo ambayo nimeielezea ni kwamba nimejionea mwenyewe kivitendo. Kwa hiyo, Mheshimiwa kwa hilo mimi sina wasi wasi tuko tayari kwenda na wewe.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake amesema kwamba wizara yake inatengeneza barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 50, Ndagoni ni kwenye roho ya Pemba kutokana na umeme uliotoka Tanga, njia ya Ndagoni haipitiki ni chafu.

Je, lini serikali kupitia wizara yako wataitengeneza barabara ile ili kuwaondoshea wananchi wale adha ya usafiri.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kwa kutaka kujua na umuhimu alionesha barabara ya Ndagoni kwamba nayo inahitaji matengenezo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba dhamira ya serikali inataka kuona kwamba kila barabara za ndani na zile ambazo si za ndani Unguja na Pemba inazifanyia matengenezo makubwa na madogo ili kuona zinaweza kupitika katika vipindi vyote vya msimu wa mwaka.

Lakini kwa upande wa Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tunao mpango kabambe wa kuona kwamba barabara hizi zinatengenezwa kwa mujibu wa hali na mahitaji ambavyo tutaweza kufanikiwa. Mheshimiwa kwa hilo naomba usiwe na wasi wasi tutafanya pale ambapo tutaona kwamba hali inaruhusu tuone kwamba wananchi wanaondokana na usumbufu ambao wanaendelea kuupata. Ahsante.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na barabara ya Msingini katika barabara hizi za ndani za *feeder road*. Kwa kuwa tunaelekea katika jiji lakini vile vile kutengeneza Ng'ambu tuitakayo, barabara ya Kisima Majongoo kuja Bondeni Kikwajuni Msikiti wa Mabati na Msikiti wa Makuti, barabara ile haipitiki na hasa tukizingatia kwamba tunaelekea kuwa katika jiji halafu vile vile kuitengeneza Ng'ambu tuitakayo.

Je, serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba barabara ile inatengenezwa ili kupata faida kwa wananchi wetu ambao barabara ile ni mbovu na haipitiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza ambalo alitaka kupata uhakika juu ya mkakati na lini barabara ya Kisima Majongoo ambayo ina umuhimu mkubwa katika maeneo ya mjini kwenye barabara za ndani kuona kwamba nayo inatengenezwa.

Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo nimetangulia kusema hapo awali. Dhamira ya serikali na mahitaji ambayo tulikuwa nayo katika nchi yetu ya barabara hizi za ndani tunahitaji zote zitengenezwe na ziweze kupitika kwa kadri wananchi vile ambavyo wanaweza zipitike. Lakini niseme kwamba orodha tulionayo ya barabara hizi za ndani ni kilimota 50 ambapo juhudi kutokana na muda siwezi kuzijataja zote.

Lakini nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba katika mpango huu tunazo barabara nyingi ambazo tumeziorodhesha ambazo kwa sasa kwa kuanzia zina urefu wa kilomita 50. Kwa hiyo, nataka nikuhakikishie Mhe. Mwakilishi juhudi hiyo ipo na nakuhakikishia kwamba kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu dhamira ya serikali ni kuona kwamba nayo inapata mafanikio katika kuona kwamba hali inakuwa nzuri zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kutoa majibu ya nyongeza ya swali la nyongeza la Mhe. Nassor Salim Ali kama hivi ifuatavyo.

Kwanza nataka nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa kufanya *home work* yake vizuri katika kujibu maswali ambayo ameulizwa.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nitoe majibu ya nyongeza kwa suala la Mhe. Nassor Salim Ali. Kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akimjibu Mhe. Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Kikwajuni swali lake la nyongeza, kwamba sisi tunafanya kazi barabara zenye urefu wa kilomita 50 za Unguja na Pemba ambazo ndizo tumezifanyia upembuzi yakinifu na hivi sasa kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri tunachosubiri ni kupata fedha ili tuweze kuzijenga barabara hizi.

Lakini atakumbuka Mhe. Mwakilishi kwamba ndani ya miaka miwili ya Bajeti Wizara yangu Afisi wa Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ imejenga barabara ya kutoka Gofu hadi Msikitini Kikwajuni, imejenga barabara kutoka Mitiulaya hadi Mwembeladu, imejenga barabara ya kutoka Misufini hadi Kwa Biziredi. Barabara hizo zote zimo ndani ya jimbo la Kikwajuni na kwa sababu fedha za wananchi inabidi tuzitawanye nchi nzima. Mhe. Mwakilishi atuvumilie serikali tuende katika majimbo mengine katika kutatua matatizo ya wananchi.(*Makofi*).

Na kuhusu suala la Ng'ambu tuitakayo kwa sasa hivi tunapata barabara kwa mujibu wa mpango uliopo sasa. Wakati ukifika wa Idara ya Mipango Miji itakapokuwa imeshaainisha maeneo mapya ya ujenzi wa barabara jambo hilo litafanywa na serikali kwa kujenga kwa yale maeneo ambayo Idara ya Mipango miji na vijiji itakuwa imeyaainisha. Lakini kwa sasa tumefanya upembezi yakinifu kwenye barabara ambazo sasa hivi zipo na zinatumiwa na wananchi. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nam. 106

Kucheleweshwa malipo ya Fundi

(Mheshimiwa Mwakilishi aliyeuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 94

Kauli ya Rais Kuhusu Bonanza la Michezo

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Kutokana na mapenzi makubwa ya michezo aliyonayo Rais wa Zanzibar na kupenda kuona kila siku Zanzibar inangara katika Tasnia hiyo, Rais alitamka rasmi kuwa tarehe 01 Januari kila mwaka itakua ni siku ya mazoezi ya viungo kwa Zanzibar nzima.

a) Je, Wizara inalijua hilo

b) Je, Baraza la Michezo linachangia kiasi gani katika Bonaza hilo

c) Wizara imefanya upembuzi wa kugundua wananchi wangapi wamehamasika kwa hili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu :-

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe swali lake nambari 94 lenye kipengele (a), (b)na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kupitia Baraza la Taifa la Michezo wanaelewa kuwa Mhe. Rais alitamka rasmi kuwa tarehe 1 Januari, kila mwaka kuwa ni siku ya ya mazoezi ya viungo kwa Zanzibar nzima.

b) Mhe. Mwenyekiti, naomba ifahamike kuwa Tamasha hili ni la Chama cha Mchezo wa mazoezi ya viungo ZABESA fedha zilizopangwa kufanikisha shughuli hii ni T.Shs. 11,745,000/- Baraza la Taifa la Michezo limechangia T.Shs. 10,000,000 ambazo ni sawa na asilimia 85.2.

c) Mhe. Mwenyekiti, takwimu zinazoonesha kuwa wananchi wamehamasika katika kufanya mazoezi ya viungo, idadi ya vilabu vilivyosajiliwa rasmi na Mrajis wa Vyama vya Michezo vimeongezeka kutoka 24, mwaka 2010 mpaka 2013 hadi vilabu 36 mwaka 2017. Pia vikundi vilivyoshiriki katika matembezi ya tarehe 01 Januari kila mwaka, kuanzia mwaka 2010 hadi 2017 vimeongezeka kutoka vikundi 12 hadi 88.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakiri majibu yaliyotolewa na Mhe. Waziri lakini katika kiwango cha fedha zile si kweli nathubutu kutamka kwamba mimi ni mjumbe wa hizi Kamati na ni mwanzilishi wa Bonanza lile mpaka hapa lilipofikia.

Swali langu linakuja hivi.

a) Je, ni lini Wizara ya Habari, Utamaduni itaipatia Ofisi ya Kudumu Baraza lile la mazoezi ya viungo, kwa sababu sasa hivi wamekuwa hawana ofisi wanatumia katika mlango wa mtu tu, kama ni Serikali inakitambua chombo kile ni lini watapatiwa ofisi.

(b) Mpaka dakika hii Baraza lile limeshindwa kukamilisha taratibu za kupata usajili. Je, Wizara itaisaidia vipi kuonekana kwamba inaondokana na tatizo la kupatiwa usajili kutoka kwenye vyama vya usajili.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengee (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Baraza lile halina Ofisi ya kudumu, lakini namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba tutafanya mpango wa makusudi tukishauriana na wenyewe watu wa Baraza tuwatafutie Ofisi ambayo itakidhi haja ya kufanyia shughuli zao zile.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mjumbe arejee swali (b) sikulisikia vizuri.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante, ZABESA ni Baraza la Mazoezi ya Viungo mpaka dakika hii limeshindwa kupata usajili kutoka kwa Msajili wa Vyama vya Michezo. Jee, Wizara yako itasaidia vipi kuonekana kuondokana na tatizo hili la kukosekana usajili mpaka dakika hii.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote kwanza nataka nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake aliyoyatoa kwa ufafanuzi kabisa na kama ninavyopenda kueleza hapa kuwa ni majibu ambayo yanafanya ufuatiliaji, majibu ambayo yanafanyiwa utafiti wa kina, kwa hivyo ninaendelea kumpongeza majibu yake aliyoyatoa.

Kwa kuendelea kumjibu swali lake Mhe. Abdalla Diwani Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe napenda nimjulishe kwamba ni kweli kwamba ZABESA hadi hivi sasa haijapata usajili, lakini aelewe wazi kwamba Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar ndio ambalo linahudumikia vyama vya michezo yakiwemo mabaraza hayo pamoja na ZABESA. Hivyo basi utaratibu uliowekwa pale ni utaratibu wa kisheria ambao unapaswa kufuatwa na wao wanapaswa kufuata utaratibu ule uliokuwepo. Taratibu zao zitapokuwa hazikukamilika usajili utaendelea kuwa mgumu. Lakini tunashirikiana kwa pamoja kuhakikisha kwamba usajili huo unapatikana na tunachukua jitihada za makusudi kuona kwamba na upande wa

Pemba nako tunawafanyia usajili vyama vyao kimoja kimoja ili suala hili liwe la kitaifa kabisa.

Kuhusu kiwango cha fedha ambacho amekizungumza nataka nimthibitishie kwamba inawezekana yeye ni Mjumbe lakini si Mshika Fedha wa pale. Lakini kama Mshika Fedha wa pale basi ninamuomba aje ofisini nitamueleza vielelezo tulivyovitumia vitu ambavyo tumewapatia na thamani kamili tuliyoipanga na tuliwapatia baada kutuletea bajeti yao.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri mwenyewe yenye kigugumizi naomba kuuliza swali dogo sana la nyongeza.

Kwanza tumpongeze Mhe. Rais kwa kuwa ameitambua siku ya tarehe mosi ni siku ya mazoezi na kwa Zanzibar nzima. Lakini jee, ni vikundi vingapi kutoka Pemba vimekuwa vikishiriki katika Bonanza hili kwa kila mwaka.

Lakini vile vile kwenye jibu la msingi amesema kuwa vikundi vya Pemba navyo vitapatiwa usajili, lakini tunataka kujua ni vikundi vingapi mpaka sasa vimepatiwa usajili huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, vikundi ambavyo vinashiriki katika mazoezi haya kutoka Pemba kwa sasa hivi vimeshiriki 15. Vile vile kwa njia ya usajili vikundi hivi kutoka Pemba kuna utaratibu maalum wa usajili wa vikundi hivi, vikundi ambavyo vinatakiwa visajiliwe ni vile vikundi ambavyo vitafuata utaratibu na sheria ambazo zinatakiwa kukamilisha taratibu hizi.

Kwa hivyo nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba pale vikundi hivi watakapoleta maombi yao tutachukua jukumu Baraza la Michezo la Taifa au ZABESA na wao au Mrajis pia na kusajiliwa vikundi hivi.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, lakini nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ila napenda nimuulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa umetwambia kwamba vikundi hivi vinakuwa vinasajiliwa, lakini jee hizi fedha ambazo zimekusanywa kwa ajili ya hivi vikundi zinatumika vipi, zinatumika kwa hivi vikundi vimesajiliwa tu au kwa ajili ya vikundi vyote.

Lakini pia tunafahamu kwamba kuna mazoezi ya *zone* ambayo kuwa yanafanyika ndani ya Wilaya na *zone* zote zenye vikundi hivi. Jee, kama Wizara inashiriki vipi kwenye kufanya mazoezi haya ya *zone* na kuvishughulikia hivi vikundi ambavyo viko nje ya mji na viko nje ya hizi *zone* ambazo zinafanyiwa haya mazoezi.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba vikundi hivi wakati vinaposajiliwa kuna fedha ambazo zinatozwa na fedha hizi zinakwenda kwa Mrajis ambaye anapokea maombi haya. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, naomba nimwambie Mwakilishi kwamba fedha hizi zinakuwepo pale kwa Mrajis na pesa zile ndipo ambapo zinaingia kupitia kwa usajili wa vikundi hivi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Wizara pia ushiriki wake wa mazoezi katika *zone* hizi Wizara imeonesha ushiriki mkubwa tu na ushahidi wa hili ni pale ambapo nimejibu katika swali mama kwamba tumechangia jumla ya shilingi milioni kumi.

Kwa hivyo huu ni uthibitisho kwamba bado Wizara inashirikiana na *zone* hizi na kufanya nao mazoezi lakini pia kabla ya ufunguzi au uadhimishaji wa tarehe 1 Januari na mazoezi haya Wizara nikiwemo mimi mwenyewe na Mhe. Waziri tumepangiwa kushirikiana nao mazoezi, kwa mfano kama mimi nimeshiriki katika usafishaji na vikundi hivi vya mazoezi kule hospitali ya Mnazi Mmoja.

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Kanuni ya 37 ninafikiri inafahamika, katika majibu ya Mhe. Naibu Waziri alilioulizwa swali kuhusu fedha za usajili. Nathubutu kusema usajili haupo kwa sababu hicho chama kikuu bado hakijapata usajili, vipi kitaweza kusajili vyama vidogo vidogo au vilabu naomba aweke sawa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kuendelea kumpongeza sana Mhe. Naibu Waziri kwa

ufafanuzi wake anaoutoa, lakini vile napenda kumuweka sawa Mhe. Abdalla Diwani wa Jimbo la Jang'ombe kwa mujibu wa Kanuni aliyoionesha.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ZABESA yenyewe haijapata usajili katika jibu mama, lakini Baraza la Taifa la Michezo kupitia Msajili wake linasajili vyama mbali mbali na ndio hapa alilolieleza Mhe. Naibu Waziri kwamba fedha zote za usajili zinaingia Baraza la Taifa la Michezo na zinatumika kwa mujibu wa bajeti iliyokuwepo ambayo tumeipitisha sisi Wawakilishi ndani ya Baraza hili mwaka jana na kila mwaka unapofikia.

Hivyo basi nataka kumjulisha kwamba bado hakujaingia fedha za usajili lakini fedha tunazozitoa ni pale ambapo wanakuwa na matatizo na wanayawasilisha Wizarani, matatizo yale Wizara yetu huwa inachangia kupitia mfuko wa bajeti ya Wizara na sio kupitia Mfuko ambao umechangiwa kupitia usajili wa vyama mbali mbali.

Fedha zile za usajili si lazima zitoke vyama vya kufanyia mazoezi lakini vyama vyote ambavyo vimesajiliwa 36 vinachangia wakati wanaposajili vilabu vyao. Kwa hivyo na vilabu vyao vitaposajiliwa fedha hizo zitaingia katika Mfuko wa Taifa, Mfuko wa Baraza la Taifa la Michezo na zitatumika kwa utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa bajeti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Sawa, swali la msingi tulilolizungumza hapa ni ZABESA, kwa hivyo hata haya majibu yalikuwa yamekidhi majibu ya msingi kwenye suala la ZABESA na ndio maana Mjumbe aliyesimama aliuliza suala zima la fedha za usajili wa vilabu vya mazoezi viko chini ya mwamvuli wa ZABESA. Mhe. Mwenyekiti, ni swali jepesi sana, ni kweli vyama havijasajiliwa kwa hivyo je, hakuna pesa hiyo.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomwambia kwanza tumekiri kwamba hakijasajiliwa Chama hicho cha ZABESA na vilabu vyake havijasajiliwa hapa.

Lakini fedha zinazopatikana kwenye usajili ni vyama vya aina yoyote ya michezo na ndivyo vinavyobakia katika Baraza la Taifa la Michezo. Hivyo hadi hivi sasa wao hawana mchango wowote waliouweka kwenye Baraza la Taifa la Michezo na hakuna fedha za ZABESA ambazo zimetumika kwa ajili ya Baraza la Taifa la Michezo.

Nam. 7

Umalizaji wa Majengo ya Skuli

Mhe. Ali Khamis Bakari – Aliuliza:-

Mpango wa Serikali ni kuwaondolea usumbufu wanafunzi na walimu kwa kuwapunguzia idadi kubwa ya wanafunzi katika chumba kimoja. Hata hivyo, bado inaonekana katika sehemu nyingi majengo ya skuli ambayo hayajakamilika kwa kuezekwa tu.

Jee, Waziri haoni kuwa kuendelea kujenga majengo mengi ya skuli bila ya kuezekwa kunazorotesha hatua za kupunguza tatizo la upungufu wa vyumba vya madarasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe swali lake nambari 7 kama ifuatavyo:-

Kabla ya kutoa majibu ya swali hili ningependa kuwakumbusha Wawakilishi kwamba sehemu kubwa ya suala hili linafanana na swali namba 62 ambalo tulijibu juzi tarehe 17 Februari, kwa hivyo itakuwa sehemu kubwa ni marejeo.

Kwanza, napenda kuwapongeza wananchi katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba kwa juhudi kubwa wanazozifanya na mchango mkubwa wanaoutoa katika ujenzi wa madarasa kwa dhamira ya kuwapatia watoto nafasi zaidi za kusoma zaidi na pia kupunguza msongamano wa wanafunzi madarasani. Serikali inazithamini juhudi hizo na itaendelea kushirikiana na wananchi katika kukamilisha ujenzi wa madarasa yaliyofikia hatua ya kuezekwa. Kwa hivi sasa yapo majengo ya madarasa yanayofikia 285 yanayohitaji kuezekwa.

Napenda kumuhakikishia Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali inachukua jitihada kubwa katika kukamilisha ujenzi wa madarasa hayo. Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita idadi ya madarasa haya ilifikia 501 na kupungua hadi madarasa 285 yaliyopo sasa yakiwemo ya skuli ya Mgambo Wilaya ya Kaskazini B Unguja. Ujenzi wa Madarasa 31 yanatarajiwa kukamilika katika mwezi huu wa Februari. Madarasa hayo ni katika skuli 9 za Unguja na Pemba. Skuli hizo ni Magogoni madarasa 3, Chutama madarasa 4, Ghana madarasa 3, Binguni maandalizi madarasa 3, Kihinani madarasa 4 na Bwereu madarasa 4 kwa

Unguja na skuli ya Mgogoni madarasa 4, Chokocho madarasa 4 na Jambangome madarasa 3 kwa Pemba.

Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wahisani mbali mbali wanaounga mkono juhudi za wananchi na Serikali katika ujenzi wa madarasa. Pia Wizara kwa kushirikiana na Jumuiya isiyo ya Kiserikali kutoka Korea imekamilisha na kufungua Skuli mpya ya Sekondari ya Kwarara na Kituo cha Kutolea matangazo ya Elimu kwa njia ya Radio na Televisheni huko Kwarara. Skuli hiyo ilifunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tarehe 11 mwezi Januari 2017. Skuli hii itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Skuli za Kijitoupele, Fuoni na Mwanakwerekwe C.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi inakusudia kuanza ujenzi wa Skuli 11 za ghorofa; tano katika hizo zitajengwa Pemba na sita Unguja. Ujenzi huo utakapokamilika utasaidia katika kupunguza msongamano wa wanafunzi katika madarasa. Wizara itaendelea na kushirikiana na wananchi katika kuyakamilisha majengo yaliyobakia hatua kwa hatua kwa kadri ya uwezo wetu. Pia, napenda kutoa wito kwa wahisani mbali mbali wakiwemo wawekezaji na wafanya biashara kujitokeza kuunga mkono miradi ya wananchi ya kuanzisha skuli au kujenga madarasa mapya. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Ali Khamis Bakari: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwanza nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kutuletea maendeleo kwa kasi kwa Serikali hii ya awamu ya saba.

Mhe. Mwenyekiti alipokuwa akijibu Mhe. Naibu Waziri katika majibu yake nilimsiliza vya kutosha, kwamba serikali sasa hivi ina mpango wa kujenga skuli ya ghorofa karibuni 11 lakini mimi nilikuwa nataka kusema jambo moja baadae nitauliza swali. Hivi sasa mimi ndani ya jimbo langu nina sehemu tatu za skuli, Shumba Viamboni, Kinowe na Tumbe zote zina sehemu ya madarasa ambayo yamekaa kwa muda wa miaka mitatu mengine hayajaezekwa, pamoja na kwamba serikali inajenga. Jee, nimuulize Mhe. Waziri wizara yake ina mpango gani kwa hawa wahisani ambao wanakuja kutusaidia kuwa *convince* na kuwashauri watuezekee yale majengo yaliobakia badala ya kutujengea.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Tumeeleza kwa wazi kwamba serikali kwa upande wetu tutajitahidi kuchukua hatua lakini pia kwa njia nyengine tutaendelea kuwashawishi na kuwaomba wahisani mbali mbali ili kutusaidia katika kukamilisha ujenzi wa madarasa yaliobakia yakiwemo na Jimbo la Tumbe. *(Makofi)*

Mhe. Hamad Abdalla Rashid (Gerei): Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi na kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika jibu mama la Mhe. Waziri limeeleza wazi lengo la Serikali au Wizara yake ni kuhakikisha linakimbiza ufinyu wa madarasa na kuwafanya wanafunzi wasome kwa raha.

Swali langu linakuja hapa, Skuli ya Birikau iliyoko katika Jimbo la Ziwani ina madarasa matano ambayo yana nyenzo safi za kufundishia yamekaa bure bila ya kutumika na skuli ile inatoa ufaulu wa wanafunzi wa sekondari, swali langu linakuja hapa.

a) Mhe. Waziri ni kitu gani kinachofanya skuli ile ishindwe kuingiza wanafunzi wa sekondari kwa kusoma pale badala yake madarasa yale yakaachwa yanakaa matupu.

b) Tatizo gani linalofanya wanafunzi wasipelekwe kwenye Skuli ya Kwale, Kondeani na Wesha baada ya kutumika madarasa kikamilifu ili kuthamini juhudi za wananchi wale. Ahsante Mhe. Mwenyekiti**,**

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo**.**

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inathamini juhudi za wananchi lakini na wakati huo pia tunaelekeza zaidi katika suala la ubora na tunaposema ubora ni kwamba inawezekana wananchi wanatamani wafunguliwe sekondari katika eneo lao, katika madarasa yao, lakini sisi kiwizara baada ya kutathimini hali ya wanafunzi, hali ya walimu pamoja na mahitaji mengine tunahisi kwamba si busara kwa sasa kuanzisha jambo hilo.

Kwa hivyo niseme tu kwamba wakati uchunguzi mwengine tukaufanya juu ya skuli hiyo tukaona kwamba yale mahitaji ya kuwepo sekondari wapo walimu na vipo vifaa wakati wowote tutachukua uamuzi wa kufungua sekondari sehemu hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Ahsante sana Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri katika maelezo yako kwamba kunajengwa skuli za ghorofa kumi na nne, nane zinajengwa Pemba na sita zinajengwa Unguja kwa mujibu wa takwimu na idadi ya watu ukiangalia Unguja kuna watu wengi sijui wamezingatia kigezo gani cha kuweza kujenga skuli hizi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali napenda kumjibu Mhe. Mtumwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni kwamba katika kugawa ujenzi wa skuli hizi kuna vigezo mbali mbali kwamba Wizara inachukua, kigezo kimoja wako ni mahitaji yaani wingi wa wanafunzi katika eneo lao fulani, kigezo chengine tunaangalia jiografia ya sehemu yenyewe na wakati mwengine huwa tunaangalia *interest* au maelekezo ya wahisani, hivyo ndivyo vigezo ambao tunavyotumia.

Kwa mfano, tunapotizama kigezo cha uhitaji katika Skuli ya Mwambe Pemba ambayo nako itajengwa ghorofa, sehemu hiyo wanafunzi wanasoma katika *shift* tatu asubuhi, saa nne na jioni kutoka na wingi wa wanafunzi na sehemu nyengine Mheshimiwa utaona kama kwamba tunaipendelea lakini hali halisi kuna idadi kubwa ya watoto kwa mfano sehemu ya Wingwi.

Wingwi kadri skuli tunazozijenga zinazidi zaidi ya watu, kwa hivyo utaona hata mradi huu pia Wingwi tumeiweka na hii tumeiweka kwa mujibu wa takwimu za wanafunzi. Kwa hivyo, ndio vigezo tunavyotumia lakini pia napenda kumrekebisha kidogo Mhe. Mwakilishi tumesema skuli 11 za ghorofa si 14.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante.*(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa Kanuni ya 59(3) ambayo inasema:

"Mjumbe yoyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kwa kuwa na sababu ya msingi maelezo anayotoa sahihi na sio mambo ya kubuni au ya

kubahatisha tu na Spika mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atowe uthibitisho wa usemi na uhaohusika"

Mhe. Mwenyekiti, niseme kweli kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Serikali ambayo imekamilika ambayo ina Rais wake, ina Makamu wa Rais, ina Mahakama pamoja na nchi huru. Katika vigezo ambavyo Mhe. Waziri amevijibu amesema kwamba kufuata vigezo ambavyo ni maelekezo ya wahaisani. Kwa upeo wangu ninavyohamu kwamba nchi sisi tunapotaka msaada au tunapotaka mahitaji yetu yote tunakuwa tunazungumza na wahisani wetu wao wanafuata maelekezo yetu sisi.

Sasa ningemuomba Mhe. Naibu Waziri anithibitishie hapa kwamba, jee Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inafanya kazi kwa kazi kwa vigezo vya wahisani na maelekezo yao. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako na niaba ya Mhe. Waziri ningesema kwamba tumesema kuwa wakati mwengine ushauri wao na ushauri wao si kwamba wanalazimisha, kwa mfano tumeitaja skuli mbili hapa au moja walitwambia kwa mujibu wa idadi ya watu walivyo ni vyema mkaihamisha sehemu moja kule Micheweni mkaileta Wingwi, hayo ni mashauri ambayo mashauri hayo baada ya mazungumzo tukakuliana ipo hoja kweli kufanya hivyo. Si kwamba walisema fanyeni, hata walikuja na hoja kwa idadi ya wanafunzi waliopo kujenga skuli sehemu hii ni bora zaidi kuliko hapa. Ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Simai Mohamed Said: Mhe. Mwenyekiti, samahani kidogo.

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea. Mjumbe kaa chini. Katibu endelea.(*Makofi*).

Nam. 13

Kusaidiwa kwa Wakulima wa Mpunga

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:-**

Kilimo ndio uti wa mgongo wa taifa hili na wakulima wengi wa Unguja na Pemba hutegemea sana kilimo cha mpunga. Kwa kuwa ukanda wa mashariki wa kisiwa cha Pemba kwa zaidi ya misimu mitano sasa mavuno yao sio mazuri na baadhi yao hawavuni kabisa.

a) Je, kuna mpango gani wa Serikali kuwasaidia wakulima hao.

b) Je, Serikali ina mkakati wowote wa kuwasaidia wananchi njia nzuri ya kilimo cha mpunga ili wapate mavuno mazuri ya kilimo hicho.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi- Alijibu

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, napenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Saidi swali lake nambari 13 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba "Kilimo ni uti wa mgongo wa Taifa letu" inakadiriwa asilimia 70 ya Wazanzibari wamejiajiri katika sekta ya Kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeandaa mkakati maalum wenye lengo la kuwashajihisha wakulima wa mpunga wa kutegemea mvua kujenga matuta kuzungushia mashamba yao kwa dhamira ya kuvuna maji ya mvua ili kuongeza uzalishaji.

Mkakati huu umeanza utekelezaji wake kwa majaribio kwenye msimu wa Masika wa mwaka uliopita 2015/2016 katika Shehia ya Kangagani (bonde la Mjumbe) eneo litakalofaidika kwa bwawa hilo ni hekta 6.2 na bwawa lina ukubwa wa sq metre 10,000.

Mhe. Mwenyekiti aidha, kwa upande mwengine Serikali inao mpango maalum wa ruzuku unaowasaidia wakulima wa mpunga uliozinduliwa rasmi mwaka 2011/2012 na ambao unaendelea hadi sasa. Katika mpango huu Serikali inachangia kwa wastani wa asilimia 75 ya gharama za pembejeo (mbolea, mbegu na dawa za kuulia magugu) pamoja na ukulima wa matrekta.

b) Mhe. Mwenyekiti kwa vile ukanda wa mashariki wa visiwa vya Unguja na Pemba ni eneo la ukanda wa maweni na linapata wastani wa mvua kidogo kila mwaka, Wizara imefanya majaribio ya mazao mengine mbadala ya mpunga pamoja na kuhimiza kupanda mbegu za muda mfupi na kujenga makinga maji, ili kupata mazao mengi ya mpunga mazao ambayo yamejaribiwa na ambayo wananchi wameanza kuyapokea na kuongeza uzalishaji wake ni pamoja na mazao ya alizeti na mboga mboga hasa matikiti maji ambayo yanastahamili hali ya ukame.

Tayari Wizara imenunua mtambo ya kukamulia mafuta ya alizeti na umefungwa katika kituo cha Ole Dodeani ili kuwasaidia wakulima kwa kukwamua mafuta na kujiongezea kipato.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti nashukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ingawa namuonea huruma kwa hali aliyokuwa nayo lakini, mimi Mhe. Mwenyekiti nitakuwa radhi kunijibu vyovyote kutokana na hali aliyokuwa nayo.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti na swali langu la nyongeza linakuja kwamba katika bonde la Kibirinzi Mhe. linaingia maji ya chumvi na kwa takriban sasa yamekuwa kama ndiyo kawaida.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. twende kwenye swali kwa kuokoa muda twende kwenye swali.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa kama sijamfahamisha atakuwa hafahamu na nikimwambia mbio mbio hali aliyonayo Mheshimiwa tutagongana. (*Makofi*).

a) Mhe. Mwenyekiti bonde la Kibirinzi takribani sasa ishakuwa kama misimu mitano linaingia maji ya chumvi, na kwa kweli imekuwa sasa hali ishakuwa mbaya katika maeneo yale. Sasa nilikuwa namuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba jee yuko tayari kufanya fidia kwa wananchi wale ili wananchi wale waondoke na waipishe Serikali katika bonde lile, wafanye vitu vyengine ambavyo Serikali ina mkono mrefu. La kama si hivyo jee iko tayari kuwafidia maeneo ambayo Serikali ama yako wazi au mashamba ya Serikali ili wananchi wale wawapishe katika eneo hilo.

b) Upande wa Mapungwi, Kusiambini, Maumbwini katika Kusini Pemba kule ambapo ni Kengeja kuna mabonde ambayo haya yanaingia maji mengi sana kama yanakuwa mito. Jee, Serikali ina mpango gani wa kuwafahamisha wananchi wake jinsi ya kutumia maji yale kwa utaratibu mpaka yakaweza kuwa na mahitaji mazuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti naomba angefanuna vizuri swali lake mwisho (b) kasema maji sijui maji gani ya mvua ama maji ya chumvi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mheshimiwa maji ya mvua *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Tusubiri Mhe. Waziri atasaidia.

UTARATIBU

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Pamoja na majibu ya maswali mazuri anayouliza Mheshimiwa alilouliza swali hili Kifungu cha 68 ukurasa wa 52;

> "Baada ya kujulisha Baraza juu ya tabia ya Mjumbe anayeshikia kusema mambo yasiyofaa kwa mujibu wa Kanuni hizi Spika anaweza kumuamuru Mjumbe huyo kukatisha hotuba yake na kukaa". *(Makofi).*

Mheshimiwa sababu ninayosemea hii ni kusema kwamba amekuwa akirudia rudia rudia hali ya Mjumbe ya Mheshimiwa anayezungumza kwa upande mmoja ni suala halipendezi, suala la udhalilishaji na kutia hofu. *(Makofi).*

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakiendelea kupiga makofi)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Wajumbe tumemuelewa Mhe. Waziri.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti mimi sijamvunjia mtu heshima, nimezungumza kiutaratibu na nimezungumzia kwamba huyu mama kwa hali aliyonayo na tunamuona sote.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, asiendelee aombe radhi.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakipiga mayoe)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo majibu lete, Waheshimiwa utulivu. Naomba utulivu Waheshimiwa *(Makofi)*

Waheshimiwa utulivu. Sasa naomba munisikilize naomba mimi ndiye nitakayetoa taarifa hiyo. Kwanza utulivu Waheshimiwa Wajumbe, tusibiri.

Waheshimiwa Wajumbe naomba muwe watulivu kwanza, haya yenu hayatapatikana kama sijatoa ruhusa wala hatutaelewana, tunaomba utulivu kwanza.

Mheshimiwa uliyeleta maelezo haya inaelekea Wajumbe wote wanahitaji uombe radhi. Kwa hivyo kuomba radhi ni uungwana.(*Makofi*).

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti mimi sikuwa na lengo baya na nilimuonea huruma Mjumbe mwenzangu, lakini...

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakipiga mayowe ya kuashiria kukataa)

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa endelea kuomba radhi, lete radhi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Sikiliza basi Mheshimiwa. Mheshimiwa nilinde. Lakini Mhe. Mwenyekiti, wengi wape, kama wanaona nimekosea basi naomba radhi Mheshimiwa. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Haya nimemaliza. Mhe. Naibu Waziri endelea na majibu.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakifanya zogo kiasi cha kutosikilizana ndani ya ukumbi)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa utulivu sasa katika Baraza, nawaombeni sana, nawaombeni sana.

Mhe.Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana, siwezi kuongea...

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa nawaombeni sana utulivu wa Baraza upatikane au tunamuondosha Mhe. Naibu Waziri na yeye akapumzike. Mhe. Naibu Waziri jawabu lete kama unalo jibu, endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na ....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako nimeshakupa muda mwingi, sasa ninaomba ukae chini. Naomba ukae chini.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ninapenda kumjibu Mhe Mwakilishi wa Jimbo la Chake Chake swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ardhi ni mali ya serikali kwa hivyo Wizara ya Kilimo bado haipo tayari kulipa fidia kwa wananchi hawa isipokuwa ni kuwapa ushauri mbadala baada ya kulima mpunga wanaweza wakalima chumvi ama wakafuga samaki.

(b) Suala la maji mengi yanaingia katika mabonde haya, kama nilivyosema katika jibu langu mama serikali imeandaa mkakati maalum wenye lengo la kuwashajihisha wakulima wa mpunga kwa kutegemea mvua kujenga matuta kuzungushia mashamba yao kwa dhamira ya kuvuna maji ili kuongeza uzalishaji.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 37 (1) Waziri au Mjumbe yoyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine na Mwanasheria Mkuu.

Mimi nilikuwa nataka kufahamu kulima chumvi ndio maana yake nini?

Mhe. Mwenyekiti: Sijakusikia unataka kitu gani.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Naibu Waziri kwenye majibu yake kwamba hiyo inatumika kulima chumvi. Mimi sijaelewa kulima chumvi, atufahamishe vizuri kulima chumvi.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa wewe siye uliyeuliza swali la msingi. Kwa hivyo tunaendelea. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Biashara.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Mwenyekiti, suala la kulima chumvi, chumvi inalimwa kama vitu vyengine na chumvi ni mradi mkubwa sana ambao unachukua sasa wafanyakazi zaidi ya elfu kumi na tano wamo katika sekta ya chumvi. Kwa hivyo, Waziri wa Kilimo alivyosema kama sehemu nyengine inalimwa chumvi ni kweli na chumvi hiyo inalimwa na tunaitia katika bajeti, nafikiri kaelewa. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante. Swali la nyongeza litakwenda kwa Mhe. Shaib Said Ali.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri inavyoelekea kwamba kilimo cha mpunga cha kutegemea mvua katika ukanda wa Mashariki wa kisiwa cha Pemba umekuwa mgumu na wananchi wamekata tamaa.

Jee, Mhe. Waziri una mpango gani kuyeendeleza mabonde ya Mlemele, Kwa pweza na Tibirinzi ili wananchi wapate mavuno ya uhakika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu swali lake Mhe. Mwakilishi lilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ina mpango wa kufanya kilimo cha umwagiliaji katika mabonde hayo ambayo umenitajia likiwemo Mlemele, tunaombwa tuwe wastahamilivu tusubiri mradi wetu ukamilike wa *E-xim* baadae tutaendelea na watavuna mavuno kama wanavyovuna wenzao.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri nilikuwa na swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa kilimo cha mpunga kinalimwa sana hapa nchini petu na kipindi kilichopita tulipatiwa mbegu ya Nerika. Lakini katika mbegu hii hakukuwa na matokeo mazuri.

Je, serikali imeandaa mbegu gani bora kwa wakulima wetu ambayo itaweza kuleta tija.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Panya Ali Abdalla swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, serikali hadi sasa bado haijaandaa mbegu rasmi ya wakulima kuvuna kwa sababu wakulima kila mtu na mapendekezo yake, kila mtu na mbegu ambayo anaipenda, lakini tunatumia kilimo chetu cha Shadidi ili

tuweze kupata mazao mazuri na mengi na utumiaji mbegu kidogo na maji kidogo. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuuliza swali namba 30 naomba uniruhusu kwa dakika moja ili kuweka *hansard* sawa juu ya swali la jana namba 21 la Mhe. Waziri wa Afya, naweka *hansard* sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa tumia muda wako kwa kuuliza swali.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naweka *hansard* sawa Baraza limepotoshwa jana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakupa dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru ninasimama kwa Kanuni 59. Mheshimiwa mimi sijawahi kulewa wala kuvuta bangi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba arekebishe kauli yake hakuna aliyelewa wala kuvuta bangi, naomba arekebishe kauli hajaambiwa mtu kiswahili nafikiri hakijui. Nilichozungumza mimi nafsi yangu naomba uchukue *hansard* umpelekee Mhe. Spika na moja Mhe. Waziri ili kuweka *hansard* sawa.

Baada ya maelezo hayo naomba kuuliza swali langu Nam. 30.

Nam 30

Utoaji wa hati za ardhi kinyume na utaratibu:

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza**:-**

Upatikanaji wa hati za ardhi unalalamikiwa kwa kuwa na urasimu na kusababisha wananchi kushindwa kuendeleza miradi yao ya ujenzi wakiwemo wawekezaji, jambo ambalo halileti sura nzuri katika misingi ya utawala bora na kuvutia uwekezaji.

a) Je, tangu Serikali ya Awamu ya 7 kwa kipindi cha pili kuingia madarakani, hati ngapi za Ardhi zimesainiwa na kupewa wahusika.

b) Je, kuna sababu gani za msingi zinazopelekea hati hizo kuchelewa kupewa wahusika ambao wanaathirika na gharama za ujenzi kupanda kwa sababu mbali mbali.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu**:-**

Mhe. Menyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 30 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, urasimu wa upatikanaji wa Hati za Umiliki wa Haki ya Matumizi ya Ardhi unaolalamikiwa na wananchi kimsingi unatokana na sababu ya msingi ya kuanzishwa upya kwa Kamisheni ya Ardhi ambayo ilipaswa kisheria kujipanga vyema kuchukua na kutekeleza majukumu yake ya kiutawala na kiutendaji.

Mhe. Mwenyekiti, katika hatua hiyo Kamisheni ilianza kuupitia upya utaratibu uliokuwepo wa utoaji wa Hati za Umiliki wa Matumizi ya Ardhi na Mikataba ya Ukodishwaji Ardhi na hatimae kufanya marekebisho ya Sura ya Nyaraka hizo pamoja na kuandaa mfumo wa utoaji wake kwa kuzingatia usalama na kupunguza migogoro itokanayo na ardhi, kuongeza uwazi juu ya utaratibu mzima wa utayarishaji na utoaji Hati na Mikataba pamoja na kuimarisha ukusanyaji wa mapato yatokanayo na ardhi.

a) Tangu Serikali ya Awamu ya Saba kipindi cha pili kuingia madarakani, wizara yangu imeshaandaa Hati za Kumiliki Haki na Matumizi Ardhi 392 na Mikataba ya Ukodishwaji Ardhi 28, kati ya Haki 404 na Mikataba 39 iliyojipangia kuitayarisha katika kipindi cha robo mwaka cha utekelezaji wa kazi zake.

b) Sababu za msingi za kukawia kwa utayarishwaji wa nyaraka hizo ni kama nilivyozitaja hapo juu ambapo Kamisheni ya Ardhi ambayo ni Taasisi dhamana ya utayarishaji nyaraka hizo ilipaswa kupitia upya mfumo mzima wa utayarishaji ambao ulionekana kutoa mwanya na kupunguza usalama wa nyaraka hizo na kupelekea kuongezeka kwa migogoro ya ardhi.

Mhe. Menyekiti, kwa mantiki ya kuuimarisha mfumo wa utayarishaji na utoaji wa Hati na Mikataba ya Ardhi, wananchi watanufaika kwa kuwa na umiliki bora wenye usalama utakaoweza kufuatiliwa kielektroniki na kumhakikishia mpewaji usalama wa haki yake ya umiliki wa matumizi ya ardhi na hatimae kumuepusha kuingizwa katika migogoro ya umiliki wa haki ya matumizi ya ardhi.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kusikitisha ya Mhe. Naibu Waziri nataka nimuombe Mhe. Makamu wa Pili Ofisi ya Rais aanze kuandika leo alivyokuambia Mhe. Simai Mohemmed Said hivi sasa, jana akaambiwa aombe radhi anza kuandika la kwanza hili.

Tumepitisha Kamisheni ya Ardhi miaka mitatu nafikiri nyuma, leo mwananchi anaambiwa bado aendelee kusubiri, hati ile ile anamsomeshea mwanawe, anakwenda benki kukopea anafanyia biashara miaka mitatu.

Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili naomba uanze kuandika kauli ya Mhe. Simai Mohammed ndio majibu ya serikali haya.
Lini hati hizi zitatoka ili wananchi wanyonge waanze kujikomboa. Lakini kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri umekiri upatikanaji wa hati unatokana na kuanzishwa upya kwa Kamisheni ya Ardhi, majukumu yake jee, Kamisheni hiyo ilianzishwa mwanzo au utafiti ndio unaendelea. Kwanza unafanywa utafiti ndio Kamisheni inakuja baadae.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa swali limesikilikana sasa muache Mhe. Waziri akujibu, amelifahamu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Naam! Mhe. Mwenyekiti, sijasikia.

Mhe. Mwenyekiti: Naibu Waziri atajibu swali lako. Swali lako ameshalisikia Mhe. Naibu Waziri sasa muache alijibu, usitoe maelezo mengine zaidi. Ahsante sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuidhinishwa na serikali kama nilivyokuwa nimejibu katika swali la msingi kwamba hati tayari zimeshaandaliwa. Kwa hivyo, iliyobakia ni *approval* na ikimaliza hapo basi inatolewa kwa wahusika. Ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kifungu Nam. 37 nimeuliza maswali mawili kajibu moja labda nirudie jengine au vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Uliza tena.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, nisimamie Kanuni ya 37 niendelee tena niliuliza maswali mawili, limepatikana jawabu moja.

Mhe. Mwenyekiti: Sema hilo ulilolikusudia katika Kanuni hiyo, eleza hilo ulilokusudia katika hiyo Kanuni ya 37.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Waziri au Mjumbe yeyote aliyeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi kwa ufupi isipokuwa kwamba suala alilouliza Waziri moja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu.

Mhe. Mwenyekiti: Swali lako ni lipi sasa mheshimiwa ambalo halijawekwa sawa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri urasimu wa upatikanaji hati unatokana na kuanzishwa upya kwa Kamisheni ya Ardhi ambayo Kamisheni ya Ardhi imeanzishwa miaka mitatu karibu nyuma.

Swali ninalouliza utafiti upi uliokuja mwanzo kati ya Utafiti na hiyo Kamisheni ya Ardhi, kipi kilichokuja mwanzo, sawa sawa na hiyo kesi ya kuku na yai lipi limekuja mwanzo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla ya kujibu mwanzoni nilipojibu nilikuwa naamini kwamba tayari karidhika kwa sababu nilijibu kwa pamoja. Kwa sababu suala lake hasa lilikuwa lini hati hizo zitapatikana. Lakini kama hakuridhika basi naomba nimuongeze ni kwamba baada ya kufanyika utafiti na utafiti siku zote unakuja mwanzo halafu ndio kinafanywa hicho kitu husika.

Ahsante sana.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza katika swali hili mama

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii ya Ardhi ina sheria nyingi ambazo zina mapungufu ambayo wakati mwengine huchangia migogoro ya ardhi na kwa kuwa pia baadhi ya sheria hizo hadi leo hazijatungiwa Kanuni.

(a) Je, ni lini serikali italeta marekebisho ya Sheria hizo zenye mapungufu Barazani.

(b) Je, lini wizara itakamilisha utungaji wa Kanuni wa Sheria hizo ili kupunguza migogoro.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Mwakilishi kwa muono wake na kwa nia yake njema ya kutaka kutatua migogoro ya ardhi nchini. Lakini pia basi tumuombe atubainishie ni Sheria ipi na ipi na mapungufu ili tushirikiane kwa pamoja kutengeneza. Kwa sababu Baraza lako Tukufu Mhe. Mwenyekiti, ndilo lenye uwezo wa kutunga Sheria ya nchi hii.

Lakini pia tutazingatia ushauri wake na kuangalia Kanuni zipi zinahitajika kwa Sheria ipi ili iweze kutekelezwa kwa haraka sana.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe.Naibu Waziri ninapenda nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala la upatikanaji wa hati linalalamikiwa sana. Jee, Wizara imeandaa mikakati gani ya kuhakikisha wanamaliza kero hii na kuhakikisha hati zinapatikana kwa wakati na bila usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, ni mambo mawili tu yatapelekea hizi hati zisichelewe.

Kama tulivyokuwa tunasema tayari zimeandaliwa lakini tunasubiri utaratibu ukamilike, ukikamilika utaratibu ni la kwanza lakini la pili ni mwananchi mwenyewe kufuata sheria. Ahsante sana. (*Makofi*)

Nam. 19

Mipaka ya Eneo la Uwanja wa Ndege wa Zanzibar

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:**

Kwa kuwa serikali inapanua Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume ambao inaonekana uwanja huo umeingiliana na maeneo ya viwanja na nyumba za wananchi lakini mpaka leo suala la mipaka ya uwanja huo linaonekana bado lina utata na kuwafanya wananchi kuingia hofu ya kukosa haki zao.

(a) Je, ni lini serikali itaonesha mipaka yake wazi wazi katika eneo hilo ili wananchi waondoe hofu hiyo.

(b) Kwa nini serikali haioneshi mipaka yake mapema katika maeneo ya taasisi zake badala ya kusubiri hadi migogoro ijitokeze.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 19 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Kiwanja cha ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume kina hati ya mwaka 1997 ambayo imeanisha mipaka na maeneo yote ya Kiwanja cha Ndege kwa upande wa Mashariki, Magharibi, Kusini na Kaskazini. Kwa mujibu wa hati hiyo kiwanja hicho kina ukubwa wa hekta 575.123.

Katika hatua ya kuweka wazi mipaka ya kiwanja hicho, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira pamoja na Masheha wa Shehia tano zilizozunguka eneo la kiwanja, iliweka alama 155 pamoja na kuainisha nyumba zote zile, maboma, misingi ambayo imeingia ndani ya mipaka ya kiwanja hicho. Changamoto inayojitokeza ni kuwa kuna baadhi ya wananchi bado wanahodhi baadhi ya maeneo hayo kwa vile walikuwepo katika maeneo hayo kabla ya uwanja huo kupimwa.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imo katika kutafuta fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao ili waweze kuondoka katika eneo hilo la kiwanja.

Kwa upande mwengine kuna wananchi wamekuwa wakilivamia eneo hilo licha ya kufahamu kwamba hilo ni eneo la Uwanja wa Ndege. Serikali ina mpango wa kuwaondosha wananchi hao ili kupisha uendelezaji wa Uwanja huo na vile vile kuwachukulia hatua za Kisheria wale wote waliovamia maeneo hayo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza awali kwamba wananchi wamekuwa na tabia ya kuvamia maeneo licha ya kujua kwamba maeneo hayo tayari yameshatengwa kwa shughuli za uendelezaji wa miradi mbali mbali ya kimaendeleo. Kwa mfano, tunazo kesi nyingi za aina hiyo hasa katika maeneo ya hifadhi za barabara. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wawakilishi watusaidie katika kutoa elimu hii kwa wananchi wao majimboni kwao wapate kuelewa hatua za kisheria zinawahusu pale wanapovamia maeneo yetu.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri lakini nina maswali (a) na (b) katika swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli amesema Mhe. Naibu Waziri kwamba bado kuna wananchi wanavamia maeneo hayo kwa kuyajenga na kila kitu.

(a) Sasa haoni kwamba ni kuiongezea mzigo serikali kila siku kulipa watu wanaojijengea ovyo wakati ambapo kama serikali ingepiga marufuku kujenga katika eneo hilo ili walipwe hao ambao walikuwepo zamani.

(b) Kwa manufaa ya wananchi wote na kwa manufaa ya serikali Mhe. Naibu Waziri angalau tu anaweza kututajia hiyo mipaka kwamba hivi sasa tu Kaskazini mpaka wapi, Kusini mpaka wapi angalau tu wananchi wakajua kama mpaka hapa ni eneo la Uwanja wa Ndege.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye Kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mwanzo eneo lile lilipimwa tokea mwaka 1967 na tukapewa na hati, lakini mipaka yote imejionesha wazi kutoka eneo fulani mpaka fulani. Kwa hivyo, wananchi wote ambao walikuwepo kabla ya hapo tumesema tutawalipa fidia, lakini wale wote waliovamia tayari wanajua kwamba wao wamevamia maeneo hayo na ni karibuni tu nilikuwa na Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Chukwani na Masheha wake tumekwenda na tukazikuta alama zipo kila sehemu.

Kwa hivyo, ni eneo kubwa lipo mpaka Buyu, tunakuja mpaka maeneo ya Wizara yetu na barabara ile ya pembeni. Hivyo, ni maeneo ambayo yameshapimwa na yanajulikana na wananchi wa pale wanajua kwamba kuna maeneo haya tayari yameshapimwa na wao wenyewe wamekiri kwamba wanasubiri wakati wowote tutakapoamua waondoke na hivi sasa tuko katika mpango wa *master plan,* ikiwa tayari basi tutaendelea kuwaondosha wale watu kwa ajili ya ujenzi au upanuzi wa uwanja wetu wa ndege wa kimataifa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona na mimi pia baada ya muda mrefu nilikuwa nina nyoosha mkono lakini ulikuwa unanipita, nashukuru sasa umenipa nafasi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa *airport* ni katika eneo muhimu la wageni au wasafiri wengi wanaoingia katika nchi yetu kama wanavyotumia bandari kuingia na kutoka. Lakini pia ni eneo ambalo linahitaji usalama na umakini mkubwa kwa ajili ya wasafiri au watu ambao wanatumia hiyo *airport.*

Mhe. Mwenyekiti, *airport* yetu ya Zanzibar tangu umekamilika ukuta lakini bado watu wamekuwa wanaingia kwa kupanda ukuta maeneo tofauti mpaka kuingia ndani ya uwanja na kutoka kwa njia moja au nyengine, kitu ambacho kinapelekea...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa uliza swali, umesimama kwa kuuliza swali.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nakuja kwenye swali. Kitu ambacho kinapelekea kuleta usalama mdogo.

> (a) Je, serikali itachukua hatua gani kuhakikisha kwamba *airport* yetu usalama unaendelea na ili kuleta matumaini kwa kampuni za ndege tofauti za kimataifa kuweza kuja.

b) Tunatambua kwamba serikali tayari ina mpango wa kujenga *terminal* mpya au *terminal II* ambayo tayari ujenzi wake umeshaanza na hatujui hadi lini utakamilika, lakini tunatambua kwamba bado serikali ipo katika mchakato kuweza kukamilisha. Jee, serikali imejipangaje kujua idadi ya wafanyakazi watakaohitajika kwa ajili ya *airport* mpya itapokamilika ili kuleta ufanisi na matumaini mazuri kwa watu ambao wanaotumia huduma hiyo ya *airport*. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said maswali yake yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a)Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaendelea kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba ulinzi unaimarika katika maeneo yote yale na kweli tuna changamoto hiyo, lakini hivi sasa tumejipanga na karibuni kuna mpango mkakati kuna wawekezaji wamekuja wanataka kuangalia namna gani ya kushirikiana na sisi. Lakini bado mipango hiyo iko katika hatua za awali na itapokuwa tayari basi tutaipeleka serikalini kwa ajili ya kupatiwa baraka zake. Lakini Uwanja wetu wa ndege sasa hivi unalindwa vizuri na kunapotokea tatizo lolote basi lile tatizo tunalichukulia hatua pale ambapo watu wanapovamia uwanja wetu.

(b) Kuhusu suala la pili ambalo anasema kwamba itahitaji....

Mhe. Mwenyekiti: Muache Mheshimiwa alikuwa anaendelea kujibu hajamaliza kujibu sasa unamkatisha.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni inaniruhusu kwa sababu swali la (a) tayari ameshalijibu na hajamaliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri majibu endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliani na Usafirishaji: Swali lake la (b) aliuliza kwamba, *Terminal II* itapokuwa tayari itahitaji wafanyakazi wangapi.

Terminal II itapomaliza itahitaji wafanyakazi wasiopungua 350.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37 "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba swali alililoulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Mwenyekiti, swali langu nililouliza la (a) ni swali la usalama na ulinzi wa *airport* Mhe. Naibu Waziri amesema wawekezaji.

Sasa nataka atufahamishe wawekezaji wanaingilia vipi na masuala ya usalama wa *airport*. Kwa sababu *airport* iko chini ya Mamlaka yake na mimi hili naliangalia kwa *interest* ya *public*. Kwa sababu hapa ni maeneo ambayo wageni wanaokuja ni watalii, Wazanzibari na Usalama. Sasa wawekezaji kama watakuwa wanapewa nafasi ya kulinda *airport* basi tungeelezwa hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana nataka kumwambia kwamba viwanja vyote vya ndege vina utaratibu wake wa ulinzi na ulinzi huu unakuwa ni siri zetu.

Kwa hivyo, mimi namuomba sana uamini kwamba uwanja wa ndege wetu uko katika hali ya usalama na hauna tatizo lolote na hata kama watakuja wawekezaji tunasema kwamba ni aina gani ya wawekezaji. Kwa sababu kama nilivyosema uwanja wetu utakapokuja kuongezeka *Terminal II*, maana yake itahitaji vile vile ulinzi uimarike na hilo ndilo tulilokusudia kwanza.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu maswali yake mbali na majibu mazuri aliyoyajibu lakini katika majibu yake amesema kwamba serikali imo katika kutafuta fedha kwa ajili ya kuwalipa wananchi hao ili waweze kuondoka na kuweza kuuendeleza uwanja ule.

(a) Jee, ni kiasi gani cha fedha ambazo zinatakiwa kuwalipa wananchi hao.
(b) Ni wananchi wangapi ambao wanatakiwa kuondoka katika maeneo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hapo awali kwamba Mhe. Nassor Salim Ali ameuliza swali hili na nimelijibu katika swali mama kwamba kuna *trend* kuwa

wale ambao wanakuwa tumeshawalipa fidia wanauza yale maeneo kwa watu wengine.

Kwa hivyo, hivi sasa sisi tuko katika mchakato wa kuwafanyia tathmini wale watu wote ambao tutajua wangapi wanastahiki fidia na wangapi hawastahiki. Kwa hivyo, namuomba atupe muda mpaka huo mchakato utapomaliza tutapata kujua idadi hasa ya watu wangapi wanatakiwa walipwe fidia na kwa gharama za kiasi gani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu kama nilivyosema hapo mwanzo watu wakishakujua kwamba maeneo haya yako katika maeneo ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wao wanayavamia. Sisi tunachukua hatua za kutaka kuwaondosha na vile vile hatua ya kutaka kuwalipa fidia ambao wanastahiki kulipwa. Kwa hivyo, atupe muda baadae tutajua ni wangapi na gharama zao na thamani yao za kulipwa hiyo fidia.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ningependa nitoe wito kwa wananchi ambao wanauza maeneo katika maeneo ambayo serikali inayahitaji kwa matumizi ya kiserikali na tayari wananchi hao wamelipwa fidia.

Kwa vyovyote vile, serikali itaendelea kuyamiliki maeneo hayo na haitotoa fidia nyengine na wale wanaouza maeneo hayo ambao tayari wamelipwa fidia watashtakiwa kwa mujibu wa sheria. Hivyo naomba sana wananchi ambao wanataka kununua maeneo wahakikishe pale wanaponunua panastahili kwa kuulizia katika wizara husika au katika ofisi zetu za Wilaya au katika vituo ambavyo serikali inavitambua kwa ajili ya kuhakikisha uhakiki wa mambo ya ardhi, sio tu kwenda kujinunulia eneo bila ya kufahamu taratibu zilizopo katika eneo hilo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Waziri kwa kuweka sawa jibu hilo. Wizara inaendelea kuulizwa na Mhe. Tatu Mohamed Ussi.

Nam. 20

Ujenzi wa Barabara za Wilaya ya Mkoani

Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibiwa swali langu kwanza naomba nirekebishe kuna neno 'ghala la mkaa', sio ghala la mkaa ni ghala la akiba Mkoani.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia kwa sababu swali langu nililipeleka katika Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ lakini kwa bahati mbaya swali langu limekuja kwenye Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji; kwa sababu serikali ipo na Waziri husika yupo wa Tawala za Mikoa naomba swali langu Nam. 20 nijibiwe. *(Makofi)*

Kwa kuwa katika mji wa Mkoani ndani ya Shehia ya Mbuguani, Ng'ombeni na Mbuyuni kuna barabara za ndani ambazo kwa sasa ni mbovu na zinahitaji ukarabati. Barabara zenyewe ni

barabara kutoka Mbuguani hadi kijiji cha Tironi, barabara inayotoka Ghala la Mkaa kuelekea Mapinduzi hadi kufika barabara kuu inayotoka Soko Kuu pwani kupitia Mahakama ya Mkoani kuelekea barabara kuu.

Je, wizara ina mkakati gani wa kuzifanyia ukarabati barabara zetu za ndani ili kuondosha usumbufu unaowapata wananchi wakati wa kipindi cha mvua.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri anaweza kulijibu aliyeopo, muache ajibu kama atashindwa yupo Waziri mwengine ataweza kunyanyuka. Mhe. Waziri endelea kujibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 20 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kabisa barabara alizozitaja ni za ndani na kwa mujibu wa sheria barabara hizo zinasimamiwa na Wizara ya Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hivyo basi, naomba kumwambia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali tunashirikiana katika kufanya kazi hizi na pale ambapo hali itaruhusu basi tuko tayari kushirikiana na Wawakilishi kuhakikisha kwamba barabara zile zinapitika kwa urahisi zaidi.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza.

Kwa sababu amenijibu atashirikiana na wizara husika hali itakaporuhusu. Sasa kama ni hivyo haoni kuna haja ya kushirikiana katika bajeti yao ya mwaka wa fedha unaokuja suala hili likatekelezwa kwa faida ya wananchi, hasa

ukizingatia barabara ya Mbuguani-Tironi ambayo ina wakulima wengi wa mazao ya biashara na chakula, lakini pia ni barabara ambayo ina mikarafuu mingi ambayo inazalisha zao la karafuu kwa taifa letu. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda Mhe. Tatu Mohammed Ussi kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni mimi pamoja na Mwakilishi wa Jimbo la Mkoani tulifanya ziara ya kutembelea hizo sehemu na yeye akanambia kwamba ana mpango mkakati kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya ya Mkoani kuhakikisha kwamba tunaanza kuzifanyia ukarabati sehemu zile ambazo ni korofi. Kwa hivyo, serikali inakuwa na mpango wake kupitia Ilani ya Uchaguzi wa CCM wa miaka mitano. Katika kipindi hiki cha miaka mitano tutahakikisha kwamba zile ahadi zote zilizotoka kwa wananchi basi tunazitekeleza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Bismillahi Rahmani Rahiim. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi nitakuwa na swali ya zaida yenye (a) na (b).

(a) Kwa kuwa barabara hizi za Pemba na nyenginezo ziko katika mazingira hatarishi hasa vilima ni lini Wizara yake itaweka vyuma au zege kwa kuzuwia ajali kwa gari zinazotumbukia ndani ya mashimo.

(b) Wananchi wangu wa Jimbo la Chaani wameathirika macho, kifua na hali zao sio nzuri kwa mavumbi na kuna hatari ya Naibu Waziri na Waziri wakazomewa watapokuja Chaani kwa barabara yao ilivyokuwa mbovu. Ni lini barabara ile watapewa ukweli wananchi wa Chaani kujengwa kuliko maneno ya kila siku yaliyokuwa hayafahamiki.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Nadir Abdul-latif maswali yake yenye Kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, tunapojenga barabara tunakuwa tunapeleka *tender* kwa zile barabara ambazo zitajengwa na wakandarasi kutoka nje na zile barabara ambazo tunazijenga sisi vile vile tunakuwa tunakwenda kwa mujibu wa vigezo vinavyoruhusiwa.

Hilo wazo lake la kuweka vyuma tunalichukua na pale ambapo tutahisi kuna uwezekano au kuna hali ya kuweka hivyo vyuma tutaweka.

b) kuhusu barabara ya Chaani, ile sio barabara ya Chaani peke yake barabara ile inaanza Bububu mpaka Mkokotoni. Mimi napenda kumhakikishia kwamba katika kipindi hiki hiki cha awamu hii ya bajeti tutahakikisha kwamba tunaanza matengenezo ya ile barabara.

Hivi sasa tuko katika hatua nzuri na hivi juzi tumetangaza *tender* na mpaka sasa hivi wameshajitokeza wazabuni 15 kwa ajili ya ujenzi wa barabara ile ya Kwanyanya mpaka Mkokotoni wanavyoiita. Kwa hivyo, avute subra tunajua kilio cha wananchi wa Chaani sio Chaani tu na maeneo mengine kama Gamba, Mshelishelini mpaka Bububu wana kilio cha aina hiyo na wao zaidi watu wa Chaani. Kwa hivyo, watustahamilie tu serikali itaijenga barabara ile karibuni.

Nam. 23

Uhaba wa Madaktari Bingwa wa Mifupa Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:

Kumekuwepo na malalamiko ya wagonjwa wanaopata ajali na kuathirika mifupa, ambapo wagonjwa hao hulazimika kutafuta tiba hiyo Muhimbili au Kibaha Tanzania Bara wakati tuna Hospitali yetu ya Mnazi Mmoja inayotegemewa kuitwa Hospitali ya Rufaa.

(a) Hospitali ya Mnazi Mmoja ina madaktari bingwa wa mifupa wangapi na mahitaji yetu kwa Zanzibar tunahitaji kuwa na madaktari wa mifupa wangapi ili huduma hizo zipatikane kwa asilimia 100.

(b) Kama tuna upungufu wa madaktari wa mifupa, kwa nini serikali isiombe msaada kwa washirika wetu wa Maendeleo kama China, Cuba au kuazima kwa ndugu zetu Tanzania Bara ili kupunguza tatizo la madaktari bingwa wa mifupa Zanzibar.

(c) Je, serikali inawasaidia vipi watu wanaotafuta huduma hizo Tanzania Bara kwa kutumia gharama zao baada ya kupata ajali na kuvunjika mifupa wakati tiba ni haki ya kila mwananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 23 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja...

UTARATIBU

(Hapa Mhe. Mjumbe alikuwa amezongwa na Waheshimiwa Wajumbe)

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Tulieni nyinyi, nina Kanuni mimi. Ninaongozwa na Kanuni, nataka nijibiwe...

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mheshimiwa pamoja na Kanuni lakini ungelisubiri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni inaniongoza, Kanuni inaniruhusu, tupitie hizi Kanuni mumetupa nyinyi wenyewe na zinaturuhusu.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mheshimiwa naomba ukae kwanza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sasa siwezi kumuacha Mhe. Naibu Waziri akalipotosha Baraza. Baraza linapotoshwa, haliwezi kupotoshwa. Nisikilize kwanza Mhe. Mwenyekiti, hoja ipo vipi Kanuni inaniruhusu, mimi sitaki kurukia tu.

Mhe. Mwenyekiti: Elezea hiyo kanuni inasemaje.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kanuni ya 59(3) inasema kwamba:

"Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu, na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika". Sasa natoa uthibitisho wangu.

Mhe. Naibu Waziri sitaki uombe radhi lakini bado Hospitali ya Mnazi Mmoja haijafikia kuitwa ya Rufaa, naomba tufute usemi huo.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub mimi sijakuelewa unachokitaka hasa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Aah! Hoja aliyosema Hospitali ya Rufaa na Hospitali ya Mnazi Mmoja haijafikia Rufaa, afute usemi wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 23 lenye kifungu (a), (b), na (c) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Mnazi Mmoja ina daktari bingwa mmoja mzalendo wa mifupa ambaye anashirikiana na madaktari wengine wanne wa kawaida katika kutoa huduma za mifupa. Mahitaji halisi ni kuwa na madaktari bingwa wanne. Ili kuziba pengo la uhaba wa madaktari bingwa wa mifupa, wizara imewapeleka madaktari wawili masomoni mmoja amepelekwa KCMC na mwengine nje ya nchi.

   Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kuchukua madaktari kutoka nje ya nchi tayari upo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja tangu mwaka 2008. Kwa sasa yupo daktari kutoka Cuba ambaye anatoa huduma za mifupa kwa muda mrefu. Vile vile wizara imo katika harakati za kupata madaktari kutoka Jamhuri ya Watu wa China.

b) Mhe. Mwenyekiti, upo utaratibu maalum wa kusafirisha wagonjwa nje ya nchi kwa wale ambao matatizo yao hayawezi kupatiwa ufumbuzi katika Hospitali ya Mnazi Mmoja, wagonjwa hao hupelekwa kwenye bodi inayohusisha madaktari bingwa na kupatiwa rufaa ikiwa Tanzania Bara au kwengineko baada ya kuonekana ipo haja ya kufanywa hivyo.

   Mhe. Mwenyekiti, naomba nieleweke kwamba kuna baadhi ya wagonjwa huamua wao wenyewe kwenda kufuata matibabu nje ya Zanzibar bila ya kufuata taratibu za kupitia kwenye Bodi ya Madaktari bingwa, hivyo wagonjwa hao hulazimika kujigharamia wenyewe. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kuuliza maswali madogo sana ya nyongeza.

a) Kwa kuwa ajali haichagui maskini wala tajiri, wala Waziri, wala watendaji wakuu, hatua ya kukosekana kwa daktari bingwa wa mifupa serikali haioni anayeumia zaidi ni maskini na ndiye aliyekuwa hana uwezo na hana uwezo wa kwenda Tanzania Bara.

b) Kwa kuwa tatizo hili ni la muda mrefu na tatizo nyeti na sio tatizo la kusubiri madaktari wa kujitolea, serikali imechukua hatua gani ya kutumia fedha zake za ndani ili kuweka madaktari wengine kupunguza hatari hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, serikali inafanya kila inavyowezekana inatumia juhudi zake zote kuhakikisha kwamba inatoa huduma ya matibabu haya na mengineyo kwa mwananchi aliye maskini na aliye tajiri. Katika hili serikali na kwa mengine haichagui ni mwananchi gani ambaye atapewa matibabu ilimradi ni mwananchi wa Zanzibar basi atapewa matibabu kwa mujibu wa Sheria za matibabu.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, na mimi napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri pamoja na majibu yako mazuri ambayo umetueleza hapa kuna baadhi ya wagonjwa wanaopata ajali na kuumia mifupa wanatibiwa hapa hapa Zanzibar hulazimika kutoleshwa pesa kiasi cha shilingi 600,000/= mpaka 800,000/= kwa ajili ya kununuliwa chuma, na baadae wakati wa kuja kutolewa chuma kile hulazimika kutoa shilingi 200,000/=.

Jee, huu ni utaratibu wa Wizara na kama ni utaratibu wa Wizara, Mhe. Naibu Waziri huoni kwamba husababisha wananchi waliokuwa na uwezo wa chini kubaki na vyuma vyao ili kuwaletea athari zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, huo sio utaratibu hata kama zinatoka pesa za kusaidia sio laki au laki hizo ambazo umezitaja. Kama lina uhakika Mheshimiwa naomba utuletee kwa maandishi na ushahidi ambao wametozwa kiasi hicho, basi Wizara yangu italifuatilia na hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya ambao wanahusika.(*Makofi*).

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa bahati nzuri nimezaliwa mtu wa mwisho kabisa kichinja mimba nafikiri ndio mtu wa mwisho katika maswali haya.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri nakiri kwamba hospitali yetu ya Mnazi Mmoja ni Hospitali ya Rufaa kwa kuwa tumeipitisha sheria katika nchi yetu. Lakini linalohitajika kuongeza bidii na ufanisi katika utekelezaji wake kwa maslahi ya watu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, wananchi wetu wengi wanapata ajali au wengine baada ya kupata misukosuko ya kuvunjika na mambo mengineyo huwa hawana uwezo wa kupelekwa kama Hositali ya Muhimbili, Kibaha na sehemu nyenginezo.

Jee, kwa kuzingatia hilo na kwa kuwa mpaka Bodi ikutane na ajali haina kinga, pana dharura gani ya mfuko wa kuwasaidia watu ambao wamefikwa na shida kama hiyo ambapo uwezo wa kusafirishwa kwa haraka hawana Wizara inawasaidia vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, wizara ina mfuko maalum ambao unawasaidia wale ambao wanapata dharura ya ghafla na ushahidi wa hayo, ila tu Mfuko huu siku nyengine huwa umejaa, siku nyengine huwa umepungua na siku nyengine huwa haupo kabisa kutokana na mahitaji.

Sasa linapotokea jambo kama hili Wizara inajitahidi kwa nguvu zake zote na saa nyengine Mhe. Mwenyekiti, inabidi mpaka wafanyakazi wanaohusika na Kitengo kile wanatoa chao kilicho mifukoni ili kuhakikisha maisha ya mwananchi yule ambaye ameathirika kwa haraka haraka kuyanusuru na baadae kufuata utaratibu mwengine.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.(*Makofi*).

Nam. 29

Upungufu wa Madaktari na Wauguzi katika Vituo vya Afya

Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Aliuliza:-

Naipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga vituo vingi vya afya, lakini hivi sasa kumekuwa na upungufu mkubwa wa wauguzi na madaktari wa ganzi.

Je, serikali ina mpango gani wa kuandaa ajira maalum kwa ajili ya Wizara ya Afya tu, kwa lengo la kuondoa upungufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 29 kama hivi ifuatavyo: -

Mhe. Mwenyekiti, swali hili nilishajibu juzi lilikuwa ni swali la 58 kwa Mhe. Suleiman Makame Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Ziwani. Hata hivyo kwa sababu umeniruhusu naomba nilijibu.

Mhe. Mwenyekiti, wizara tayari imeshapata ruhusa ya kuajiri Madaktari na Wafamasia wenye Shahada ya Chuo ikuu. Aidha, serikali imetoa ruhusa kwa kuajiri mafundi wasanifu wa dawa waliohitimu mwaka 2014 na 2015 katika Chuo cha Afya Mbweni.

Pamoja na hawa, serikali imeshatoa ruhusa pia ya kuajiri wafanyakazi 221 wa kada ya afya ambao watakidhi viwango kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi. Hivi sasa yaani katika kipindi hiki tulicho Wizara tayari inaendelea kukamilisha ajira za Madaktari 44 na Wafamasia 4 na wataendelea kufanya hivyo kwa utaratibu maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu watu wa ganzi ameuliza pia ni jumla ya wafanyakazi wa Wizara ya Afya, kwa hiyo, pia miongoni mwa ambao wataajiriwa tutajitahidi pia kuhakikisha tunaajiri watu wa kada hiyo. Ahsante.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, ahsante naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri Hospitali ya Kivunge ina daktari mmoja tu wa ganzi na hivyo hupelekea ikifika muda wa saa 9:30 anarudi mjini kutokana na kuwa hana sehemu ya kuishi pale Kivunge. Jee, Wizara yako ni lini itampatia nyumba ili aweze kuishi pale Kivunge ili kuwaondoshea matatizo wananchi ambao kuwa inawalazimu ikifika muda huo wa saa 9:30 kuweza kuletwa mjini na kusababisha hasara kubwa ya mafuta.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali hili la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na uhaba uliopo wa nyumba za kuisha wafanyakazi Kivunge pamoja na hospitali nyengine zote, basi Wizara ina uwezo wa kumpatia makaazi mfanyakazi huyo. Mhe. Mwakilishi naomba kama kakulalamikia basi mwambie aje aripoti Ofisini aone kama Wizara haitampatia nyumba ya kuishi Kivunge ili kuweza kukidhi mahitaji ya wananchi.(*Makofi*).

Mhe. Mtumwa Peya Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi napenda kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Vituo vya Afya kwa muda mwingi sasa vimekuwa vinakosa fedha za kulipia umeme, hiyo inapelekea wakati wa usiku kuwa kiza na kusababisha kupungua kwa kazi wakati huo wa usiku.

a) Mhe. Naibu Waziri naomba unieleze huu utaratibu wa kupewa fedha za umeme kwa vituo vya afya kwa sasa haupo.

b) Kama haujafutwa na ungali unaendelea kwa nini fedha hizo hazipelekwi vituoni ipasavyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, utaratibu wa kutoa au wa kupeleka pesa kwa ajili ya umeme katika vituo bado upo na unaendelezwa, isipokuwa mahitaji ya baadhi ya vituo huwa ni makubwa kulikoni pesa ambazo zinapelekwa. Mara nyingi katika vituo takriban vyote isipokuwa labda hicho ambacho umekianisha wewe Kamati za Afya zilizomo katika vituo vile, huwa wanajitahidi na tunaomba na kituo ambacho umekianisha kifanye hivyo kwa kushirikisha Kamati ya Afya basi tatizo dogo la umeme katika sehemu ambayo imebakia mara nyingi huwa wanalikamilisha wao.

Sasa tunakuomba mheshimiwa pamoja na Waheshimiwa wengine kwamba inapotokea tatizo kama hili, basi mjitahidi kuzishirikisha Kamati zenu za Afya zilizopo katika vituo, na naamini kwa mashirikiano makubwa yenu Waheshimiwa Wawakilishi na Wabunge mliomo katika majimbo hayo ambayo vituo vimo, basi hili sio tatizo kubwa linarekebishika. Tunaomba sana muwape mashirikiano lakini Wizara yangu inatoa bado mpango wa pesa hizo kwa ajili ya umeme. (*Makofi*).

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Jimbo la Kijitoupele kwa bahati nzuri Mhe. Shamsi Vuai Nahodha wakati huo Mwakilishi na Mhe. Haji Juma Sereweji wakati huo Mbunge wamejenga hospitali nzuri tu ambapo kutokana na msongamano mkubwa uliokuwepo Hospitali ya Fuoni ikimalizwa hii yaani ile ya Jimbo la Fuoni hospitali hiyo ya Magirisi kwa Jimbo la Kijitoupele itawasaidia watu wengi sana kuondokana na msongamano uliokuwepo Fuoni. Hospitali imekamilika kujengwa, imeezekwa bado madirisha na milango na mambo mengineyo ya kupiga sakafu.

a) Jee, kupitia taarifa ya hapa ambayo wananchi wanasikia huko sasa hivi, Wizara inaichukulia hatua gani hospitali hiyo ili kuimaliza.

b) Kama kuna changamoto ambazo za msaada mimi kama Mwakilishi na mwenzangu Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Mbunge tuko tayari kusaidia ili wananchi wetu wapate shufaa ya kupata manusura ya matibabu pale wanawake na watoto pamoja na watu wengine kuwa rahisi matibabu yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi kutokana na matatizo ambayo yapo katika kituo chake cha Kijitoupele ulichokitaja, ukipata nafasi uje ofisini ili kwa mashirikiano ya Wizara pamoja na wewe Mwakilishi wetu na ikiwezekana na Mhe. Mbunge basi tuzungumzie zile changamoto ambazo tunazihisi Wizara kwamba zitaendelea kuwa changamoto wakati tukishakukifungua, tutafute njia ya kuzisuluhisha baadae tuendelee na utaratibu ili wananchi waanze kupata huduma katika kituo kile bila ya matatizo yoyote.(Makofi).

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2016

(Kusomwa kwa Mara ya Pili)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, majadiliano yanaendelea. Kwenye meza yangu hapa kuna Mhe. Hassan Hafidh lakini simuoni, kwa hivyo ninampa nafasi Mhe. Naibu Waziri wa Afya kutoa mchango wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo hapa kwetu lakini pia kwa uongozi wetu ambao munaokaa hapo mbele na kutuongoza pamoja na kudhibiti mambo yote ambayo yamo katika Baraza hili na hatimaye Mwenyezi Mungu kutujaalia kwenda sawia na kumaliza mambo yote kwa manufaa ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, pili napenda nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti na Wajumbe wote wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kwa kuupitia na kuufanyia marekebisho katika baadhi ya vifungu vya Mswada huu. Ushauri na mapendekezo yao ni msingi na tunaahidi kuufanyia kazi kwa ukamilifu kwa lengo la kutekeleza malengo tuliyokusudia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Wajumbe wote wa Baraza lako Tukufu kwa michango yao mizuri yenye lengo la kuimarisha Mswada wetu huu ili iweze kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, bidhaa zinazodhibitiwa na wakala wa kusimamia chakula, dawa na vipodozi ni muhimu sana katika maisha yetu ya kila siku. Aidha, masuala ya utengenezaji, utumiaji uhifadhi na usambazaji wa lazima udhibitiwe kisheria. Hata hivyo, udhibiti huo ni lazima ushirikishe wadau wote wanaohusika katika kulinda afya za Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, ubora na usalama wa chakula ni jambo jema kwani kufuatia mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi ulimwenguni baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa wakiitumia vibaya fursa hii kwa kufanya udanganyifu katika bidhaa wanazozizalisha ikiwemo kubadilisha vifurushi, kughushi tarehe na muda wa matumizi wa bidhaa, kuhifadhi katika sehemu zisizo rasmi na

kuongeza *chemical* mbali mbali katika bidhaa zao. Wahalifu hao lazima washughulikiwe kisheria niwaombe Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wasisite kutoa taarifa kwa wakala pale inapobainika mambo haya yanafanyika katika majimbo na Shehia zao.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili tunawaomba sana wananchi kwa Waheshimiwa Wawakilishi peke yao basi litawashinda, lakini naomba pia na wananchi wanaotusikia hili walichukulie kwamba ni moja kati ya mashirikiano kuishirikisha na kushirikiana na hii Bodi yetu ya Chakula, Dawa na Vipodozi. Njia moja ya kuwasaidia ni kuwabaini wale wote ambao wanafanya udanganyifu na kuwaripoti kunakohusika.

Mhe. Mwenyekiti, ubora na usalama wa chakula ni jambo jema kwani hufatia mabadiliko ya mifumo ya kiuchumi ulimwenguni baadhi ya wafanyabiashara wakitumikia vibaya fursa hii kwa kufanya udanganyifu katika bidhaa wanazozizalisha ikiwemo kubadilisha vifunganisho. Mhe. Mwenyekiti, vita dhidi ya dawa duni na dawa bandia ni suala la ulimwengu mzima, hakuna sehemu iliyokuwa salama ikiwemo Zanzibar juu ya uhalifu huo wa kifamasia. Niwaombe Waheshimiwa Wawakilishi na wananchi kupitia kwenu tushirikiane pamoja kuzibaini bandari bubu zinazotumika kupitisha bidhaa ambazo ubora wake haujahakikiwa kwa kuingia kwa dawa hizo kutahatarisha afya za jamii na kutumia dawa ambazo hazina nguvu za kutibu, hivyo kupoteza fedha nyingi na baadae kusababisha vifo kwa watumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, vifaa tiba navyo ni lazima vidhibitiwe kwani usahihi na usanifu wa bidhaa hizo ni muhimu katika kuwaongoza wataotoa huduma za afya juu ya matibabu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, natoa wito kwa jamii kurudi katika mfumo wa vipodozi asilia, vipodozi hai (*organism*) ambavyo havina madhara juu ya mtumiaji. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitoe mfano kwamba wazee wetu zamani walikuwa wanatumia vipodozi vya asili. Kwa mfano, mawardi, asumini, vilua, mipachori, mipompia na maua tofauti. Mhe. Mwenyekiti, vifaa vile au mazao yale ambayo yalikuwa yanatumika kwa wazee wetu yalikuwa yanawasaidia sana na mara nyingi wazee wetu walikuwa wanaonekana wazuri zaidi kulikoni hata tulivyo sisi sasa hivi.

Mhe. Mwenyekiti, wazee wetu walikuwa wanatumia liwa kwa ajili ya kusugua nyuso zao na mwili wao pamoja na karafuu, lakini sisi leo liwa lile lile tumeliacha letu la asili tunatumia liwa ambalo linaletwa kwenye kikopo kutoka China, kutoka Singapore, kutoka sehemu nyengine yoyote ya dunia. Liwa

ambalo tayari limeshachanganywa na mambo mengine, limeshawekwa na ma-*chemical* sisi wenyewe tunajiona ndio tunajisaidia kwa liwa lile, matokeo yake kijana mdogo ana umri wa miaka 20 au 25 akikuangalia uso wake unaona una rangi zisizopungua tatu.

Mhe. Mwenyekiti, ile ni athari kubwa, *chemical* tunazozitumia kwa sababu tunabinya tunapata, sisi wenyewe tunaona lile ni jambo rahisi zaidi. Urahisi ndio lakini unatuathiri na unawaathiri vijana wetu. Mimi napenda nitoe wito kwa vijana, akinamama wenzangu, lakini pia wapo na akina baba ambao wanajichubua na wanafanya mambo kama haya na wanaharibu *face* zao.(*Makofi*).

Naomba nitoe wito sana kwamba turudi katika matumizi ya vipodozi vya asili. Asumini ukiianika ukichanganya na liwa, kiluwa ukiisaga, ukiiweka vizuri na ukijipaka kwenye uso basi amini Mwenyezi Mungu uso wako utaendelea kuwa mzuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya vipodozi vyenye viambata vya sumu ni hatari kwa afya ambavyo vinapelekea aina mbali mbali ya maradhi, ikiwemo saratani za ngozi. Mhe. Naibu Spika, sasa hivi saratani za ngozi ni nyingi. Mtu akikuangalia utaona siku za mwanzo uso wake unameta uko vizuri sana, lakini baada ya mwaka au miaka miwili basi anaanza matatizo, kama *fungus* na mengineyo. Kwa bahati nzuri vipodozi hivi tunavitia katika sehemu mbali mbali, sehemu nyengine ambazo hata hazihitaji kuwekwa vipodozi hivi, ungeweka kikuba ingependeza na ingefurahisha, ingemfurahisha na ambaye unataka afurahi. Lakini matokeo yake tunaweka ma- *chemical* makubwa mazito. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, sikufichi sasa hivi asilimia kubwa ya wanawake, niseme ya wanawake lakini pia na ya wanaume wanakulalamikia wana *fungus*, *fungus* hizi zinasababishwa na vipodozi ambavyo tunavitumia ndugu zangu. Nawaomba sana tuwache kutumia vipodozi ambavyo sisi wenyewe tunaviona ni salama, lakini haviko salama. Kipodozi ambacho ni salama ndugu zangu nawaomba hebu turudi kwenye kikuba, kilua tukivitayarisha vizuri vile, tukiviweka chumbani kwetu, bila ya kupiga ile pyuu! pyuu! ku-*press* ile, basi ukifungua tu chumba kwa mara ya kwanza utaona jinsi chumba kinavyokufurahisha wewe mwenyewe mtumiaji wa chumba kile.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kuna wazee maalum, kama kule Pemba tulikuwa tunaye bibi mmoja tulikuwa tunamwita bibi mlezi. Tulikuwa tunamwita bibi mlezi kwa sababu alikuwa kawaida yake anapita majumbani akiuza vitu kama hivi,

alikuwa ana mkoba wake mwenyewe katengeneza vikuba, mawardi basi anapita anakuuzia unaweka chumbani kwako unatumia kwa matumizi yako. Hapa Unguja nasikia alikuwepo bibi mmoja au sijui yuko mpaka leo Bi. Sihaba, na yeye pia alikuwa akifanya biashara kama hizi, nawaomba sana. Halafu vitu kama hivi havina gharama kubwa, kwa sababu kilua unapanda nyumbani kwako unapata kuchuma miaka chungu nzima mkilua haufi. Mwasmini, wengi Wazanzibari tuna miasmini nyumbani kwetu na mambo mengine ya kawaida unaweza kuwa nayo, kwa nini upate shida ya kununua ma-*chemical* upoteze pesa bure wakati vitu vya asili vipo. Ndugu zangu nawaomba akinamama wenzangu nawaomba turudi kwenye vipodozi vyetu vya asili, ambavyo walikuwa wakitumia mabibi na mabibi na wakaa na mababu zetu mpaka wakatujukuu sisi.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, wakala itakapoanzishwa itakuwa na kazi ya udhibiti wa sumu mbali mbali, hususan zinazotokana na uhifadhi mbaya wa nafaka na *chemical* mbali mbali zinazoongezwa katika bidhaa za chakula.

Mhe. Mwenyekiti, Kanuni za afya nazo ni lazima zifuatwe kwa kuwashajihisha jamii kupunguza matumizi ya vyakula vyenye mafuta mengi, badala yake kutumia mboga za majani na suala zima la ufanyaji wa mazoezi ili kujikinga na maradhi, kufika mapema katika vituo vya afya mtu anapojibaini kuwa anaumwa na sio kusubiri mpaka maradhi yakiwa yamemwangusha. Usafi wa mazingira nao ni jambo muhimu la kuzingatia na kujikinga na maradhi mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili nilitaka kidogo nitoe wito kwa wananchi huko mitaani tunakokaa. Tuna tabia moja, mgonjwa akishaanza ugonjwa akianza kwenda hospitali mpaka akishafikia hali hajisikii vizuri sasa hawezi tena kutoka anahitaji asilimia 100 ya msaada wenu familia ili mumpeleke hospitali, basi mgonjwa yule anawekwa kitandani, badala yake familia wanakusanyika wanatoka sehemu mbali mbali wanakuja kukaa pale kwa ajili ya kumshughulikia mgonjwa. Hawamchukui mgonjwa yule wakamkimbiza hospitali akaenda kupata matibabu, wao wanaridhika kwamba kutokana na hali hii aliyo, basi huyu tena ni wa kufa tu, sasa tutakuwa tunamsaidia sisi wenyewe. Lile sio sahihi hawamtendei haki mgonjwa. Mgonjwa anatakiwa amalize saa yake ya mwisho akiwa anashughulikiwa na daktari. Daktari ndio mthibitisho wa mwisho kubaini kwamba huyu ameshamaliza na kwa hapa hata huduma yoyote ambayo nitampa haimsaidii.

Mhe. Mwenyekiti, lakini matokeo yake mgonjwa yule anaongea taratibu, anaweza kula taratibu, anaweza kunyanyuka taratibu, basi yupo tu nyumbani

kitandani hapelekwi hospitali kwa sababu nini, aah! hali yake imeshakuwa mbaya, huyu tena sio wa kupelekwa hospitali. Mheshimiwa kama si wa kupelekwa hospitali, na kule hospitali wakifika wale madaktari watamuambia kwamba huyu mrudishe sio wa kumleta hapa hospitali, kitu ambacho daktari sio rahisi kumrudisha mgonjwa.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba sana wananchi ambao wanawaweka wagonjwa majumbani kwao, kwa kutegemea kwamba atakufa sasa hivi, atakufa baadae huyu sio wa kumpeleka hospitali. Basi nawashauri wagonjwa wale wawapeleke hospitali, washughulikiwe wapate huduma za afya kule, kwa vyovyote vile jinsi atakavyofanyiwa huduma na daktari ambaye anaujuzi maalum kasoma na ana *degree* au ana *diploma*, basi ni tofauti na nyinyi nyumbani mtakavyomshughulikia, kumwacha nyumbani, mukamshughulikia bila ya kumpa matibabu sahihi ambayo angeyapata hospitali kule mimi naita ni kumtayarisha kufa, sio kumtayarisha kuendelea kuishi.

Ndugu zangu wanachi naomba hili tulizingatie sana na tulifanyie kazi. Mimi nasema hivi kwa sababu nina ushahidi nimeshawaona wagonjwa ambao wako majumbani na hali ni mbaya na wanafamilia wanasema aah! sio wa kupelekwa hospitali. Mhe. Naibu Spika, kwa haya machache naomba kutoa mchango wangu huu, na naunga mkono kwa asilimia 100 ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Naibu Waziri kwa mchango wako katika hoja ya chakula, dawa na vipodozi. Kwa sababu Wajumbe wamemaliza basi namwita mtoa hoja kuja kutoa maelezo, majibu na ufafanuzi ya Wajumbe.

Mhe. Waziri tafadhali.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza kabisa naomba kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukiwa wenye afya njema na wazima, kuja hapa kuwatumikia wananchi wa Zanzibar.

Pili nakushukuru sana wewe Mhe. Mwenyekiti, pamoja na utufikishie salamu zetu za shukrani kwa Mhe. Spika, Naibu Spika, Mwenyekiti mwenzako Mhe. Bi. Mwanaasha Khamis Juma, pamoja na watendaji wako wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kutupa mashirikiano yao ya dhati katika Mswada huu na mambo mengine yote ambayo tunafanya kama Wizara ya Afya katika kutekeleza majukumu yetu.

Tatu, Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Kamati ya Ustawi wa Jamii, nitaomba niwataje, ikiongozwa na;

1.	Mhe. Dk. Mwinyihaji Makame	Mwenyekiti
2.	Mhe. Tatu Mohammed Ussi	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Ame Haji Ali	Mjumbe
4.	Mhe. Hidaya Ali Makame	Mjumbe
5.	Mhe. Makame Said Juma	Mjumbe
6.	Mhe. Masoud Abrahman Masoud	Mjumbe
7.	Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	Mjumbe
8.	Mhe. Viwe Khamis Abdallah	Mjumbe
9.	Ndg. Aziza Waziri Kheir	Katibu
10.	Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru Kamati hii kwa michango yao yote, pamoja na marekebisho ambayo tumekubaliana na yote leo yamewasilishwa, na kwa upande wetu wa Wizara ya Afya tumeshirikiana nao vizuri na tumekubaliana na marekebisho yote hayo. (*Makofi*).

Nne, naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wawakilishi wote wale waliochangia kwa kuzungumza na wale waliochangia kwa maandishi, pia na wale ambao hawakubahatika kuchangia, lakini wamekuwa wakitupa maoni yao na mawazo yao mbali mbali katika mazungumzo ambayo tumefanya nao.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme kwamba mara hii katika uzoefu wangu humu Barazani, basi Wawakilishi wametoa michango mingi sana ambayo tumeikubali na itafanya Sheria hii iwe nzuri zaidi. Kwa hivyo, naomba sana kuwapongeza kabla sijatoa ufafanuzi wa baadhi ya yale mambo waliotoa, lakini naomba kuwapongeza sana Waheshimiwa Wawakilishi wote waliochangia. Lakini nitatoa pia pongezi maalum kwa Wawakilishi watatu ambao tumekaa kwa kina na kuyajadili masuala yao ama maoni yao, ama marekebisho waliyotoa.

Mjumbe wa kwanza kabisa ni Mhe. Wanu Hafidh Ameir, namshukuru sana. Sio mimi tu, hata watendaji kwa kweli wanalipongeza hili, tumepokea mengi pamoja na *consultation* ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu tumepokea mengi miongoni mwa michango yako, na nitaitolea ufafanuzi.(*Makofi*).

Mjumbe wa pili ni Mhe. Miraji Khamis Mussa Kwaza, kwa kweli yeye michango yake mingi sana aliyoitoa tumeipokea na tumeweza kufanya

marekebisho mbali mbali. Wa tatu nitamtaja baadae wakati natoa maelezo haya.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, waliochangia kwa kuzungumza moja kwa moja ndani ya Baraza ni:

1.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Viti Maalum
2.	Mhe. Ali Suleiman Ali	Jimbo la Kijitoupele
3.	Mhe. Ali Khamis Bakari	Jimbo la Mgogoni
4.	Mhe. Rashid Makame Shamsi	Jimbo la Magomeni
5.	Mhe. Asha Abdallah Mussa	Jimbo la Kiwengwa
6.	Mhe. Miraji Khamis Mussa Kwaza	Jimbo la Chumbuni
7.	Mhe. Zulfa Mmaka Omar	Viti Maalum
8.	Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf	Jimbo la Chaani
9.	Mhe.Simai Mohammed Said	Jimbo la Tunguu
10.	Mhe Salma Mussa Bilal	Viti Maalum
11.	Mhe Suleiman Sarahani Said	Jimbo la Chake Chake
12.	Mhe Amina Idd Mabrouk	Viti Maalum
13.	Mhe. Omar Seif Abeid	Jimbo la Konde
14.	Mhe. Machano Othman Said	Jimbo la Mfenesini

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri, naomba ukae kidogo, nataka kumwita Mhe. Naibu Spika. Naomba ukae. Waheshimiwa Wajumbe, muda sio mrefu nitampisha Mhe. Naibu Spika, kuendelea na kikao hiki.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri wa Afya. Karibu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuendelea.

15.	Mhe. Sheha Hamad Mattar	Jimbo la Mgogoni
16.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Jimbo la Ziwani
17.	Mhe. Dr Sira Ubwa Mamboya	Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
18.	Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali	

Mhe. Naibu Spika, waliochangia kwa maandishi ni;

1. Mhe. Mohd Mgaza Jecha Jimbo la Mtambile
2. Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
3. Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
4. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo
5. Mhe. Bahati Khamis Kombo Jimbo la Chambani
6. Mhe. Said Omar Said Jimbo la Wingwi
7. Mhe. Juma Ali Khatib, Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum
8. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira.
9. Mhe. Zaina Abdullah Salum Viti Maalum
10. Mhe. Khadija Omar Kibano Jimbo la Mtambwe
11. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Jimbo la Chaani
12. Mhe Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.
13. Mhe. Ussi Yahya Haji
14. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
15. Mhe. Mwanasheria Mkuu

Mhe. Mwanasheria Mkuu ambaye ametuchangia miongozo mingi sana ya Kisheria na kutuletea uwiano wa Sheria nyengine mbali mbali, tunamshukuru sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya kuwatambua Wajumbe waliochangia, kwa heshima naomba sasa nitoe maelezo na majibu ya hoja na michango mbali mbali iliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe hao katika Mswada wetu huu ambao ni muhimu sana kwa maisha ya wananchi wa Zanzibar.

Kwanza kabisa maoni ya Kamati ya Ustawi wa Jamii, ushauri wote tuliopewa Mhe. Naibu Spika, wa Kamati hii ya Ustawi wa Jamii tumeupokea, tumeuchukua kwa ajili ya kuufanyia kazi, pia yakiwepo marekebisho yaliyoletwa na kukipa meno chombo hiki kwa ajili ya kupewa bajeti zaidi na ya kutosha, ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Kwa hivyo, hayo yote tumeyapokea.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, michango ya Wajumbe wengine, nitaanza na Mhe. Wanu Hafidh Ameir Viti Maalum. Neno “Bodi ya Ushauri” lililotafsiriwa katika kifungu cha 3 cha Mswada huu, tumekubali tunalirekebisha kwa kufuta neno “Ushauri” na sasa litabakia neno, “Bodi”. Ni kwa sababu hii ni *Board semi autonomous* yaani ya uwakala, kati kati baina ya mamlaka na hiyo Bodi ya awali. Kwa hivyo, lazima iwe ni Bodi ya Ushauri. Kwa hivyo, Bodi ya Ushauri

itatumika katika maelezo, lakini pale katika tafsiri ya neno "Bodi" tutatumia neno "Bodi la Ushauri tunaondosha. Naomba pia meza ya Katibu i-*note* hilo.

Aidha, Mhe. Wanu Hafidh Ameir pia alishauri kwamba marejeo ya kifungu cha 7 yabadilishwe na badala yake yawe Kifungu cha 5A. Majibu ya hoja hii ni kwamba marejeo ya kifungu cha 7 yabaki kama yalivyo, baada ya kuchukua ushauri kutoka kwa wanasheria. Huu ni uandishi wa sheria yenyewe, kwa sababu ndio utaratibu sahihi wa uandishi, hasa pale unapofanya marekebisho ya sheria, kutoka sheria ya zamani kuja sheria mpya ambayo inakuwa na marekebisho. Marejeo ya kifungu cha 4 yaliyopo katika tafsiri ya neno "Wakala" na marejeo ya kifungu cha 8 katika tafsiri ya "Mkurugenzi Mtendaji", yatabaki kama yalivyo kama nilivyoeleza katika mfumo na utaratibu mzuri wa kuandika sheria.

Mapendekezo ya Mhe. Wanu Hafidh Ameir pia kuhusiana na malipo kwa Wajumbe wa Bodi katika kikao chetu cha pamoja, yamekubaliwa na kifungu hicho sasa kitaingizwa kwenye jadweli la marekebisho ya sheria hii na hivyo itasomeka kama ifuatavyo. Tunakushukuru sana Mheshimiwa kwa mchango wako *detail analysis* uliyotupa, sasa itasomeka kama ifuatavyo.

"Wajumbe wa Bodi watalipwa posho kutoka katika fedha za Wakala kwa kiwango kama kitakavyoidhinishwa na Waziri".

Kwa hivyo, Waziri atatia saini zile Kanuni ama ule utaratibu huu wa kulipana maposho, ataweka saini na kuanzia hapo ndio maposho hayo wataweza kulipana hawa Wajumbe wa Bodi kutokana na utaratibu huo. Kwa hivyo, tumekubaliana na mapendekezo hayo.(*Makofi*).

Mapendekezo ya Mhe. Mjumbe kuhusiana na kifungu cha 15A(2) juu ya kukosekana kwa tafsiri ya maneno, "*regional information*", yatajumuishwa pia kwenye tafsiri ya kifungu hicho, tunayapokea hayo.

Katika kifungu cha 60B mapendekezo ni kwamba maneno "inaweza kuanzisha", katika tafsiri ya Kiingereza iliyochukuliwa ikaletwa kwenye tafsiri ya Kiswahili, maneno haya yafutwe na badala yake liwekwe neno "itaanzisha", ili kuweka ulazima kwa wakala wa kuanzisha mpango huo uliokusudiwa katika kifungu hicho. Kwa hivyo, kwenye tafsiri ya Kiingereza iko sawa, ila tafsiri hii ya Kiswahili itarekebishwa. Pendekezo hilo Mhe. Naibu Spika, naomba nikujulishe la Mhe. Wanu Hafidh tumelikubali.

Kifungu cha 93A, kwa mujibu wa hoja ya Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Wizara inapendekeza kifungu hiki kiandikwe upya kama ifuatavyo na nitaomba nikinukuu Mhe. Naibu Spika.

Kifungu cha 93A(1)

"Mtu hatoruhusiwa kumiliki ama kuhodhi alama yoyote ya dawa isiyo sahihi".

Hizi *fake products W*aheshimiwa wengi walichangia kwenye *labelling for the fake products* ama *label* kutumika. Kwa hivyo, kifungu cha 93(A)(1) tumekubali marekebisho hayo na tunashauri iwe hivi.

(2) Mtu yeyote atakayemiliki au kuhodhi alama ya dawa kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa la jinai na atakapopatikana na hatia atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita au faini isiyopungua shilingi milioni moja au adhabu zote mbili kwa pamoja". Kwa hivyo, marekebisho hayo yatahusika hivi sasa.

Kuhusu suala la kumaliza kosa chini ya kifungu cha 124A juu ya uwezo wa Mkurugenzi Mtendaji kumaliza kosa yaani (*Compounding of offences*). Tunaomba tumjibu Mheshimiwa kwamba Mkurugenzi Mtendaji ndiye Mtendaji Mkuu wa Wakala. Hivyo yeye ndiye anayepaswa kuchukua hatua kwa jambo lolote lile linalotokea kwenye Wakala au linalohusiana na Wakala. Kuishirikisha Bodi kutapelekea kuongeza urasimu, kutapelekea pia kuchelewa kutoa maamuzi.

Mhe. Naibu Spika, natoa mfano, mtu kakamatwa na kontena la kuku bandarini, ameshapigwa faini. Sasa tunasema kwamba ile *fine* wakati kuna *negotiate* ya malipo ya ile *fine* basi amalize Mkurugenzi, tusubiri mpaka Bodi ambayo inaitwa kila baada ya miezi mitatu inakaa *quota*, tusubiri mpaka Bodi wale kuku watakuwa hali gani, yule mtu atakuwa hali gani na ile biashara yake itakuwa hali gani, alipe *fine* sheria ifuate mkondo wake aendelee yeye na biashara na sisi tuendelee na kazi yetu.

Kwa hivyo, tunamuomba sana Mheshimiwa atukubalie kwamba tusimuangalie mtu, tuaangalie yule Mkurugenzi wenyewe na tunaamini ndio maana kule tumeomba *experience* ya miaka saba, wengi wamesema miaka mitano kwa sababu hii ni Bodi ya kitaaluma. Sababu moja kubwa ni dhamana anayopewa ya kutoa misamaha kwa *fine*, ndiyo maana tukaomba miaka saba mtu anakuwa

kisha-*mature*, miaka mitano bado tunahisi ni machache sio kwamba anaondoshwa kijana anatafutwa mzee, hapana.

Lakini la pili hii inaweza kusababisha pia kuongeza kwa urasimu ikiwa inakwenda kwenye Bodi na kuathiri pia maisha ya wananchi moja kwa moja, kama yale maamuzi hayakufanyika haraka na *products* zile za chakula zikatoka pale bandarini zikaingia sokoni huku tunaendelea na mlolongo ule mrefu wa kushauriana, basi yale yanaweza kuathiri jamii. Kwa sababu hii ni Bodi inayodhibiti moja kwa moja, tunataka hatua hizo zichukuliwe haraka sana.

Kuhusiana na uwezo wa kumaliza kosa hili, ni utaratibu wa kawaida unaotumika pia katika taasisi zinazotoa huduma kutolingana na huduma hizi. Utaratibu huu pia unatoa fursa kwa Ofisi kufanya mashauriano na mkosaji ili kuweza kufanya malipo ya kiwango cha *fine* kama ilivyoelezwa katika Sheria husika. Endapo ikitokea mkosaji atakataa kulipa *fine* hiyo ndiyo taratibu sasa za kijinai zinaweza kuchukuliwa dhidi yake yeye. Nitatoa mfano wa makosa kama hayo.

Sheria ya Mamlaka ya Usafiri Baharini (*Zanzibar Maritime Authority -ZMA)* inayo Sheria ya Taasisi iliyokuwako chini ya Mhe. Amina Salum Ali (Waziri wa Biashara na Viwanda) Taasisi ya Kulinda Viwango (*ZBS),* pia Sheria hii iko huko kwamba yule Mkurugenzi Mtendaji anafanya maamuzi moja kwa moja kuondosha urasimu. Utaratibu kama huu unatumika pia kwa makosa ya jinai unaojulikana kama *pre-bargain*, Wanasheria watatusaidia hapa baadae ambapo mkosaji wa jinai hupewa fursa ya kwanza kukubali kukosa na ya pili kulipa *fine* na badala ya kifungo. Kwa sababu nia yetu ni pia wafanyabiashara waweze kuendelea na biashara zao. Makosa haya huwa yanatokezea lakini wakati huo huo kumlinda mwananchi na kumpatia kinga katika chakula, dawa ama vipodozi atakavyotumia.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) ushauri wake Mhe. Naibu Spika, tumeupokea na kuhusu kuimarisha bidhaa zinazoingia nchini pia tumepokea na Bodi inaendelea kufanya ukaguzi wa bidhaa hizo kutoka nchi za nje na zile zilizozalishwa nchini zikiwemo pia bidhaa za chakula, dawa, vifaa, tiba na vipodozi. Vifaa vya nje kidogo vinakuwa na bei kubwa na vinalipwa kwa Dola, vifaa vya hapa hapa nchini kwa Tanzania Shilingi.

Kwa upande wa bidhaa za chakula zinazotokana na mifugo, Bodi imeanza kutekeleza Kanuni ya nyama na maziwa. Jumla ya machinjio 13 yameshakaguliwa tayari na machinjio 7 yamefungwa rasmi baada ya kubainika hayakuwa katika hali ya kuridhisha, ninayo pia orodha ya hayo machinjio.

Machinjio hayo hayakuridhisha kiafya. Miongoni mwa machinjio yaliyofungwa ni Mkwajuni, Matemwe, Kidoti, Donge-Chakachua, Donge-Eneani, Mfenesini na Kinyasini.

Machinjio 4 yamepewa muda ya kufanya marekebisho ya haraka sana, nalo ni chinjio moja ni la serikali tumelipa onyo la kufanya marekebisho haraka ni chinjio la Kisakasaka. Mengine yaliyopewa onyo ya kufanya marekebisho haraka sana Mhe. Ussi yapo kwako, ni chinjio la Muwanda, chinjio la Mwera na chinjio la Mahonda, chinjio moja halitumiki tena na moja limepasi, nyumbani nimekusudia Tumbatu, Ninarekebisha kidogo hapo ni chinjio moja lililokubalika ni chinjio la Machui, nadhani wengi mnalifahamu chinjio hilo. Nyama yote inayochinjwa kwenye machinjio yaliyoruhusiwa hukaguliwa na kupigwa muhuri maalum with *Edible Ink*, ule wino ambao unaweza kulika ili kuthibitisha ubora wake na usalama wake kwa wananchi.

Mhe. Ali Khamis Bakar Jimbo la Mgogoni, ushauri wake Mhe. Naibu Spika, tumeukubali na kwa kushirikiana na wadau mbali mbali tutaendelea kudhibiti uigizaji wa bidhaa katika njia zisizo rasmi pamoja na hizi bandari bubu Unguja na Pemba kwa kushirikiana na taasisi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, aidha uuzwaji wa dawa katika maduka ya kawaida ni jambo ambalo halikubaliki na tumekuwa tukifanya ukaguzi wa kuziondoa dawa hizo madukani. Zamani kama mtakumbuka kulikuwa na dawa nyingi zilikuwa zinatoka Kenya, kama dawa za panadol, dawa ya kikohozi na kadhalika. Sasa tumesema tutenganishe duka linalouzwa unga wa sembe na peremende tusiweke tena madawa hayo.

Mhe. Naibu Spika, hivyo tunawaomba wananchi na Waheshimiwa Wawakilishi mtusaidia na wafuate utaratibu huu wa kufungua maduka rasmi ya dawa kwa mujibu wa Sheria hizi. Hapo zamani Sheria zile zilikuwa hazipo. Kuna dawa mimi nakumbuka utotoni tulikuwa tukila zilikuwa tamu kama peremende, lakini tulikuwa hatujui kama ni dawa na tunazila kwa wingi. Sasa kijana mmoja wakati nasoma Skuli ya Hamamni alianguka ghafla akatoka povu, kumbe alikula *over dose* kwa sababu alifikiria ni peremende.

Kuhusu agizo la Mhe. Rais alilolitoa katika ufunguzi wa jengo jipya la Hospitali ya Mnazi Mmoja juu ya udhibiti wa maduka ya dawa. Bodi yetu ya Chakula Dawa na Vipodozi imeshafanya ukaguzi katika maduka yote ya kuuza dawa Unguja na Pemba. Naomba nilithibitishe hilo. Katika ukaguzi huo maduka 282 yamekaguliwa na jumla ya maduka 19 yamefungwa moja

likiwemo la Mwakilishi alikuja kuniona sitomtaja hapa, tukampa utaratibu na sasa hivi nashukuru amerekebisha na anafuata utaratibu.

Mhe. Rashid Makame Shamsi wa Jimbo la Magomeni, ninakushukuru sana kwa mchango wako. Mhe. Naibu Spika, mchango wake ni mzuri sana amekwenda *deep* sana mpaka watendaji wamekubali kwamba umekwenda *deep* katika mchango wako huu tunakupongeza sana. Ufafanuzi wa neno virutubisho, neno hili limeelezwa katika kifungu cha 2 cha Sheria mama, naomba uangalie ile Sheria mama yenyewe ambacho kwa muhtasari maana yake ni bidhaa zilizotengenezwa kwa mjumuisho wa viini vya lishe muhimu, kama vile *vitamin* na *protein* kwa madhumuni ya kuimarisha afya. Kwa Kiingereza ina tafsiri pana kubwa sana, kwa sababu maneno mengine yale hayamo kwa Kiswahili. Naomba uridhike kwa jibu letu hili.(*Makofi*).

Katika kifungu cha 6(2)(a) tumekubali pamoja na Waheshimiwa wote walichangia pale neno "Zanzibar", litakuwa, "Mzanzibari". Kifungu 6 (2) (c) mwisho yanaongezwa maneno katika fani inayohusika. Tunakubaliana nayo maoni yako tunalipokea na naomba tutaliingiza rasmi katika marekebisho haya tunayoyapitisha hapa na Kamati ya Ustawi wa Jamii pia ilipendekeza neno hilo. Kifungu cha 13(a)(2) "Mchunguzi aliyeteuliwa na ikathibitika kwamba ana mgongano wa kimaslahi yanayohusiana na kazi chini ya Sheria hii atapoteza sifa za kuwa mchunguzi".

Kifungu cha 124(a), (1) (b) Mhe. Shamsi pia alitaka kujua kwa nini maneno mawili, yaani Sheria na Kanuni yametumika kwa pamoja. Majibu ni kwamba *fine* huweza kuelezwa katika Sheria ya Kanuni ambayo hutungwa na Mhe. Waziri na yeye Waziri ndiye anayesaini. Hivyo, maneno hayo mawili ni lazima yatumike sambamba katika kifungu hichi, tunaomba hapo utukubalie. Katika kifungu cha 3 cha jadweli imekusudiwa kwamba maamuzi ya Bodi yafanywe na Wajumbe wakiwa ndani ya Zanzibar. Tunahofia wanaweza wakafanya maamuzi wakenda kutembelea vile viwanda huko Urusi, Saiberia na kwengineko na kule yakifanywa maamuzi nadhani mmeshaelewa mazingira yatakuwa ya utatanishi. Tunataka arudi hapa wawepo watendaji, iwepo sekretarieti yao, Bodi iwe imekamilika kikamilifu ndio maamuzi yafanywe. Hata kama wamekwenda kukagua wote kiwanda huko lakini maana kule tena unaweza ukapewa vile vitu alivyosema Mhe. Suleiman Sarahan Said vya kuonja vile, ukapewa kule ukirudi huku inakuwa tofauti. Kwa hivyo wote ni lazima warudi hapa wasije wakafanye maamuzi huko nje.

Mhe. Asha Abdalla Mussa kuhusu kufanyika utafiti wa bandari zisizo rasmi. Ushauri wake tumeuchukua na tutaufanyia kazi kwa kushirikiana na Wizara

nyengine mbali mbali pamoja na Wizara ya Mhe. Haji Omar Kheir. Kwa mujibu wa Sheria mtu atakayepata madhara ya chakula dawa, vifaa tiba au vipodozi anatakiwa kuripoti wakala. Kuna fomu maalum na fomu hizo zinapatikana katika vituo vyote vya afya na huyo muhusika anatakiwa. Ila hapa tumeshauriana pia kwamba na Wakala sasa hivi ni lazima watoke nje wakajitangaze wamekaa ndani mno. Baada ya kufanya kazi yao ya *inspection* kupitia maduka, watoke nje kwa wananchi wafanye kampeni maalum, waandae majukwaa kama yale ya akina Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwenye majumbo yao, waweze kutoa elimu ya kueleza nini dhamana yao ili wananchi wajue wapi pa kupeleka malalamiko yanapokuwepo, ili kuingiza bidhaa nchini ni lazima msafirishaji afuate taratibu zilizowekwa na wakaguzi hufika katika viwanda vinavyozalisha bidhaa hizo ili kuhakikisha usalama wake kama nilivyoeleza kwenye uwasilishaji Mswada wenyewe.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, namshukuru sana Mhe. Miraji Khamis Mussa pia kwa mchango wake katika kifungu cha 5(b)(i) kitaendelea kusomeka kama ilivyo kwa sababu uhalisia wa Bodi ni kutoa ushauri kwa uongozi wa Wakala. Kwa Wakala bado anakuwa na Bodi ya Ushauri, bado hajawa na ile Bodi siyo ya Ushauri. Kazi za Mwenyekiti zimeelezwa katika kifungu cha Kwanza cha jadweli ambazo ni kuongoza vikao vya Bodi na kutokana uhalisia wa taasisi yaani Wakala hadhi ya Bodi ni kushauri utendaji wa mambo mbali mbali yanayohusu Wakala. Kwa mujibu wa kifungu cha 12(1) uanzishwaji wa Kamati ya Kitaalamu uko chini ya Ofisi ya Wakala. Ofisi ya Wakala inamaanisha ni uongozi wa taasisi, sifa na uteuzi wa Wakuu wa Idara kwa mujibu wa kufungu cha 7(2) zitaelezwa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma.

Kuhusiana na sifa ya Mkurugenzi Mtendaji kuwa Mfamasia mwenye Shahada ya Pili. imezungumzwa na Wajumbe wengi sana na hapa naomba nitoe majibu ya jumla kama ifuatavyo. Yaani hapa nazungumzia ile Digirii ya pili, nazungumzia ile miaka ya 7. Mhe. Naibu Spika, wengi wa Wajumbe mlipochangia ilikuwa mnatuonesha kama sisi tumem- *target* mtu. Naomba ieleweke hatuja m-*target* mtu, sisi tumekusudia kumlinda mwananchi. Tunaamini kwa fani hii kwa taaluma hii kama huyu kiongozi wa taasisi hii hakuwa na *Master Degree* ni *specialization* akiwa na Digirii ya Kwanza atakuwa hana taaluma ya kutosha ya kuweza kudhibiti ama kuzuia hizi dawa kwenda kwa jamii moja kwa moja, Digirii ya kwanza haitoshelezi.

Mhe. Spika, wengi wamesema hapa kwamba hata kwenye uongozi kwenye Katiba yetu kuna nafasi ya watakaojua kusoma na kuandika tu, tunakubali kwenye uongozi. Kiongozi wa Wizara anatakiwa ajue kusoma na kuandika tu

tunakubali hilo, lakini Bodi hii huwezi kuiwekea kiongozi anayejua kusoma na kuandika wala wa diploma, wala *first degree*, anayetakiwa hapa ni lazima awe na *masters*, kwa sababu ya *sensitivity* yake, yaani mambo ya hatarishi ambayo yanagusa katika jamii moja kwa moja. Hapa kuna dawa tunatumia sana kila mtu anapokuwa mgonjwa, lakini kuna chakula ambacho tunatumia siku zote, mbali ya hilo kuna na vipodozi. Kwa hivyo kutokana na sensitivity hii lazima, miaka saba katika Sheria kuu ya Utumishi kwa taarifa yenu Waheshimiwa Wawakilishi kupitia kwako Mhe. Naibu Spika, katika Sheria Kuu ya Utumishi tayari nafasi hizi nyeti inasema miaka 15 *experienced*, sisi tumekwenda nusu tu ya hiyo miaka 7.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba Waheshimiwa katika hili mtukubalie hatujam-*target* mtu, hatujazuia nafasi ya vijana kuingia na huyu mkurugenzi aliyekuwepo sasa hivi aliyekuwa anatimiza sifa hii ni kijana tu. Mkurugenzi naomba usimame uonekane kidogo, ni kijana. Kwa hivyo hatujam-*target* mtu ni kijana sana huyu, mdogo sana kwangu mimi, mimi mwenyewe kijana hapa nilipo.(*Kicheko*).

Mhe. Naibu Spika, Sheria hii ikihusisha na baadhi ya sheria nyengine za miti shamba na sumu. hivyo Mfamasia ni mtaalamu aliyepata mafunzo ya bidhaa zote zilizotajwa, wengi walitaka kwenda kwenye mtaalamu wa chakula. Miongoni wa Wajumbe walizungumza pia kwa nini mtaalamu wa chakula asiwe chakula chenyewe kina kemikali ndani, chakula chochote, ukiunguza unapata *carbon* mwisho hata wali, mchuzi, unatokana na *chemical component*. Kwa hivyo tunataka Sheria hii pamoja na Sheria nyengine za Kimataifa zinatutaka huyu lazima awe ni Mfamasia.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa ufafanuzi zaidi tofauti na mtaalamu wa chakula ambaye utaalamu wake huishia kwenye chakula tu. Aidha msingi wa Sheria hii yaani *Supreme National Legislation,* Sheria zinazotokana na kuridhia mikataba mbali mbali ya Kimataifa ambayo ni Sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria iliyoridhia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo imetiwa saini na Wakuu wa nchi tatu wakati huo, akiwemo Mhe. Yoweri Kaguta Musseven, Mhe. Danier Arap Moi na Mhe. Benjamin William Mkapa mnamo tarehe 30/11/1999, unatudhibiti sisi pia kama Tanzania lazima mkuu wa taasisi hii awe ni Mfamasia. Kwa hiyo mtu wa chakula hatofaa, atafaa Mhe. Miraji Khamis Mussa na Mhe. Shamsi Rashid, mtaalamu yule wa chakula Mhe. Naibu Spika, atafaa kwenye zile idara husika, wale wataalamu wa *feld* zile mbali mbali watafaa. Lakini mkuu wa taasisi lazima awe Mfamasia kutokana na unyeti wa kazi yenyewe.

Katika mkataba huo kifungu cha 118 bahati nzuri mkataba huo upo na nimekuja nao Mkataba wa Afrika Mashariki ambao Zanzibar pia ilishiriki kusaini. Kifungu cha 118 kinazungumzia makubaliano hayo ya kwamba Bodi hizi katika kuanzishwa lazima Mfamasia atakuwa ndiye Mkuu wa Idara hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka zote za udhibiti za nchi wananchi wa Jumuia ya Afrika Mashariki zinaongozwa na Wafamasia. Nitatoa mfano *TFB* ya Tanzania inaongozwa na Dkt. Sile ambaye ni Mfamasia, taasisi kama hii Kenya inaitwa *KPPB* inaongozwa na Mfamasia Dkt. Fred Sioyi na kwa upande wa Uganda *National Drug Authority* inaongozwa na Mfamasia Dkt. Dora Husemelwa.

Mhe. Naibu Spika, hata Sheria ya Umoja wa Afrika ya jina la *Africa Union model law on Medical Product Regulation* katika kifungu chake cha 10, kimetaja sifa za wakuu wa taasisi wanaosimamia udhibiti wa dawa kuwa ni *medicine, pharmacy, nursing, veterinary medicine, or public health* kwa ujumla sifa zote hizo zinahusiana na dawa moja kwa moja, chakula ikifuata baadae.

Mhe. Naibu Spika, chombo hichi ama taasisi hii kinachopewa uwezo wa kisheria kuwasajili Wafamasia lazima Mfamasia huyu anayewasijili Wafamasia wote wengine Zanzibar awe na *master's degree,* huwezi kuwa Msajili, huwezi kuwa *Professor* huwezi kuwa na wanafunzi wa digirii ya kwanza na mwalimu akawa na digrii ya kwanza, lazima awe na digirii ya pili. Kwa hivyo, hapa umuhimu wa kuwa na *master's degree* kwa sababu yeye ni Msajili wa Wafamasia wote hapa nchini. Hivyo sio busara hata kidogo kwa wataalamu wa aina hii wakasajiliwa kuwa chini ya usimamizi wa mtu asiyekuwa na utaalamu uliobobeya wa dawa.

Mhe. Naibu Spika, kuhusiana na Wakala kwamba itaandaa taarifa kuhusu kifungu cha 15C (2). Mhe. Rashid alitaka pia kujua neno "kila baada ya muda", maana yake ni nini. Kifungu hicho sasa kinarekebishwa na kitasomeka kama ifuatavyo, naomba nikinukuu.

"Wakala itaandaa taarifa kila baada ya miezi mitatu na kuiwasilisha katika Bodi".

Kifungu cha 6(2)(b) kuhusiana na sifa za Mkurugenzi Mtendaji.

119A (2) tamko la mgongano wa maslahi litashughulikiwa kwa mujibu ya miongozo iliyotangazwa na tutaongeza maneno na Waziri kwenye Gazeti Rasmi la Serikali. Kwa hivyo tunakubaliana na wewe Mhe. Rashid.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa nikenda kwa Mhe. Zulfa Mmaka Omar, ushauri wake tumeupokea na ni lazima nikiri kuwa Wakala hii imepewa dhamana nzito kwa wasimamizi wa ubora, usalama, chakula, dawa na vipodozi. Suala la Darajani na Wamachinga linasimamiwa na taasisi nyengine zikiwemo Baraza la Manispaa. Aidha ukaguzi wa machinjio pia unafanyika na machinjio kadhaa tayari yameshafungwa, kama nilivyoeleza hapo awali na kupewa muda na kufanya na hayo mengine kupewa muda wa kufanya marekebisho hususan masuala ya usafi.

Mhe. Nadir Abdul-latif, yeye alizungumzia masuala ya udhibiti wa vitu feki. Huu utafanywa kwa kushirikiana na wenzetu wa Taasisi ya Viwango Zanzibar na kuchunguza bidhaa zote zinazoingia na kuzalishwa nchini katika lengo la kulinda afya za wananchi. *Inspection* zinazofanyika nchi za nje kwa mujibu wa sheria na bidhaa za dawa hukaguliwa sambamba katika yale maeneo yaliyokuwa muhimu kama vile kuku, samaki, maziwa na *tomatoes paste.* Hizi kwanza hazikai muda mrefu sana na zikiingia wadudu wowote zinakuwa hatari sana kwa afya ya binadamu. Kwa hivyo, viwanda vyote hivyo ni lazima twende tukakague, tumeanzia hapo kwanza halafu tutakwenda kwenye bidhaa nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, taasisi hii na kwa kushirikiana na taasisi mbali mbali za kimataifa pia inaendesha *operation* mbali mbali za kudhibiti dawa feki na bandia hapa nchini. Aidha majaribio ya dawa zinadhibitiwa kwa mujibu wa Sheria hii. Ukaguzi maalum wa kubaini udanganyifu katika bidhaa za chakula unaendelea. Kwa hivyo, hata hizo dawa zinazotoka India kama ulizotoa mfano Mhe. Nadir zikijakugundulikana hapa pia nazo tunazichukua hatua na hata huko India baadhi ya viwanda pia tayari vimeshatembelewa na jana katika hotuba yangu nilitaja baadhi ya nchi zilizotembelewa kwa ajili ya kupata ukaguzi wa viwanda vyao.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Simai Mohammed Said viongozi watakaochaguliwa watakuwa wazalendo tunamuhakikishia hilo na watasimamia vyema dhamana zao watakazopewa. Aidha fomu za maadili zitajazwa kwa mujibu wa Sheria na Wakala itafanya kwa karibu sana na kwa kushirikiana na wenzetu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko (*ZBS*) yaani Taasisi ya Viwango hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, *ZFDB* inafahamu dhana ya *Public Private Partnership* (*PPP)* na mfanyabiashara ni muda wao mkubwa *ZFDB,* vile vile Wakala atashirikiana kwa karibu sana na Mamlaka za Usimamizi wa Mazingira katika kuteketeza bidhaa zisizofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Salma Mussa Bilal ushauri wake tumeupokea ushirikiano na *ZBS* utaimarishwa na kamati za kitaalam zitaekewa miongozo maalum ya kutekeleza kazi zao. Nakushukuru sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Suleiman Sarahan Said elimu itaendelea kutolewa juu ya ubora na usalama wa chakula na vipodozi, *engineer* wanafaa sana katika masuala ya udhibiti hususan vifaa tiba, *biomedical engineers* na *chemical process engineering*, tunakubaliana na wewe. Aidha viwango vya kimataifa vilivyokusudiwa hapa ni vile vya *ISO* yaani *International Standard Organization* ambazo taasisi na maabara lazima wavipate ili maamuzi yetu yaweze kutambuliwa kimataifa.

Mhe. Naibu Spika, nimempigia debe kidogo Mhe. Suleiman Sarahan kwamba katika baadhi ya viwanda wakenda wamchukue na yeye apate kwenda kuonja onja kule, kwa sababu kunakuwepo na vionjo kule pia. Kwa hivyo hilo usiwe na wasiwasi.(*Makofi*).

Mhe. Amina Iddi Mabrouk elimu ya shahada ya pili kama nilivyoeleza hapo awali ni muhimu katika masuala ya udhibiti hasa katika *field* hii nyeti na inayodhibiti pamoja na kutoa vibali kwa Wafamasia wengine wote. Kwa hivyo muhimu sana naomba utukubalie ikiwezekana hata *PhD* baadae tutachukua lakini sheria ikomee hapa kwenye *master's degree*.

Mhe. Omar Seif Abeid bidhaa ya mchele huthibitishwa baada ya kuchukuliwa *sample* bandarini na huchunguzwa kwenye maabara. Wakala itaanzisha program maalum ya ufuatiliaji wa athari za dawa kwa watumiaji wa dawa hizo pamoja na chakula kisichofaa kimezingatiwa katika sheria mama. Fidia itatolewa kwa atakayeathirika kwa matumizi ya dawa kwa mpango maalum utakaowekwa na wakala.

Mhe. Machano Othman Said Wakala atakuwa na Makao Makuu katika maeneo ya Mombasa ambayo ninajua umeshawahi kufika na Ofisi ndogo yao itakuwa Wete Kisiwani Pemba na watafanya kazi za ukaguzi, usajili kwa visiwa vyote viwili cha Unguja na Pemba pamoja na visiwa vidogo vidogo, wakati Maabara Kuu itakuwa Unguja. Ipo programu maalum ya ukaguzi vijijini Unguja na Pemba ambayo inafadhiliwa na *Global Fund* hilo wataendelea nalo. Pia Taasisi hii Mhe. Naibu Spika, inatoza asilimia 2 ya thamani ya Ankara yaani *proforma invoice* kwa uingizaji wa dawa nchini. Kwa hivyo wale waliotoa masuala ya madola yale yote kama mzigo Mhe. Nadir na wewe unahusika, kama mzigo umekuwa mkubwa na *proforma invoice* ni kubwa tuseme mfano mzigo wa dola milioni moja. Kwa hivyo ukichukua asilimia 2 ya dola milioni moja unapata

dola elfu ishirini. Kwa hivyo itapita kiwango hicho cha 6500 inategemea na ukubwa wa mzigo, wao wana-*charge* asilimia mbili ya *proforma invoice*.

Wakala ataimarisha mashirikiano na *ZBS*, hilo nimeelielezea, vile vile Taasisi ya Kumlinda Mlaji Serikali hilo inashughulikia vizuri na hivi sasa naomba nikujulisheni liko chini ya Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko limefikia pahala pazuri sana. Ninamshukuru Mhe. Waziri Amina Salum Ali kwa mchango wake, kutupa kwa hatua zilizofikiwa. Tunakushukuru Mhe. Waziri. *(Makofi)*

Mhe. Shehe Hamad Matar, ushauri wako wote tumeupokea, Wakala utaandaa utaratibu maalum wa kushirikiana na Masheha katika Shehia mbali mbali katika kudhibiti hizi bandari bubu na masuala mazima ya uuzwaji wa bidhaa zinazodhibitiwa na Bodi. Pia tutawatumia Masheha kufikisha elimu hii kwa wananchi kwa sababu mwananchi wa kawaida elimu hii hana, ukimchukua mkaazi wa Nungwi pale kwenye diko la uvuvi hana bado. Kwa hivyo tutashirikiana na Waheshimiwa Wawakilishi ili elimu hii kuweza kuifikisha na kupitia Waheshimiwa Masheha elimu hii kuweza kufikia chini. Bodi itakuwa inafanya kazi hiyo wakati huo itakuwa inaitwa Wakala.

Mhe. Suleiman Makame Ali, ushauri wako juu ya bidhaa zinazosemekana zinatoka China, wauzaji wa maduka ya dawa vijijini na bandari bubu tumeuchukua na tutahakikisha kuwa vituo vya afya binafsi vinatoa taarifa ya athari hizo zinazotokana na dawa kwa Wakala na udhibiti wa suala zima alama ya dawa kinyume cha sheria. Kwa hivyo naomba niwajulishe Waheshimiwa Wawakilishi wote na Mhe. Miraji nilimtolea ufafanuzi lakini nilikuwa sijamuona kidogo pale, lakini ufafanuzi mkubwa sana tumekupa katika eneo lako na ninaamini Mhe. Rashid Shamsi atamnon'goneza mengi miongoni mwa niliyosema.

Hospitali binafsi ndugu zangu Waheshimiwa Wawakilishi hizi zote zitakuwa chini ya Sheria hizi na pia nazo zitakuwa na udhibiti wa dawa ambazo zitauzwa katika katika hospitali binafsi.

Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya Waziri asiyekuwa na Wizara Maalum (MBM). Pongezi na ushauri wake tumeupokea Wakala utashiriki kikamilifu katika uwiano wa udhibiti wa bidhaa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha Wakala itafanya kazi kwa karibu na Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala na mashirikiano na Idara ya Mazingira yataimarishwa. Hizi ni pamoja na zile dawa za Sunna zinazouzwa nje ya Msikiti wa Ijumaa ninaosali mimi kila Ijumaa.

Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri Naibu Waziri, kama alivyoeleza hapo awali Mhe. Amina Salum Ali alivyoeleza katika maelezo yake ya maandishi, kuwa suala hili linashughulikiwa kwa kina sana na ni suala la watumiaji yaani *Consumer Council*, kutakuwa na Sheria hii ya *Consumer Council*, lakini *Consumer Council* haiko kwetu sisi Wizara ya Afya, sisi ni watu wa kutoa matibabu na kuwalinda, walaji wote wako chini ya Mhe. Amina Salum Ali. Kwa hivyo Sheria hii inafanyiwa kazi na itaendelea kuwalinda kwa upande wake walaji na watakuwa na haki yao na sauti yao maalum ambayo itakuwa inatolewa kupitia Serikali. Elimu hii pia itatolewa na tutaendelea kutoa kila wiki kwa kutumia vipindi mbali mbali vya televisheni na radio.

Mhe. Lulu Msham Khamis Naibu Waziri wa Kilimo, ushauri wake Mheshimiwa tumeupokea na tunaahidi kuufanyia kazi kwa mashirikiano na wizara yake yeye mwenyewe na taasisi zote nyengine zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, niko mwisho mwisho sasa hivi, Wajumbe waliochangia kwa maandishi naomba niwataje Wajumbe wafuatao waliochangia kwa maandishi pamoja na baadhi ya maelezo yaliyotolewa.

Mhe. Mohammed Mgaza Jecha, Mhe. Rashid Ali Juma na Mhe. Moudline Castico, ushauri wenu tumeupokea na tutaufanyia kazi.

Mhe. Chum Kombo Khamis Naibu Waziri Habari, Utalii, Michezo na mambo mengine yanayohusiana na hayo ushauri wako tumeupokea, utafiti juu ya mafuta hayo ya *Okay* uliosema utafanyika. Vipodozi vinavyoongeza sehemu za mwili yaani wale wanaojiongeza sehemu za mwili zitaendelea kudhibitiwa sambamba na dawa zinazoleta athari kwa watumiaji. Naomba sana mama zangu, naomba sana dada zangu, naomba wadogo zangu wa kike turudini tena kwenye masuala yetu yale ya asilia, tunakuombeni sana turudini kwenye dalia, turudini kwenye liwa.

Kuna Mheshimiwa mmoja humu ndani sitomtaja mtaalamu yeye atatusaidia, kaniletea mimi orodha yote yale ya mambo ya jadi, kanambi kuna vipodozi vya asili kama vile liwa, kuna behedan, kuna zingifuri, kuna wanja wa kombe, kuna wanja wa ukuti, kuna karafuu ya kujisugulia, kuna mafuta maalum ya mlangilangi, yanatiwa ndani viluwa na mpompia, kuna zile asumini zinazokaushwa zikatwangwa zikatiwa, tuacheni kutumia hizi *relaxer* kali kali *super* na *miles* hatari, nyengine zinachomoa hizi nywele, tunaishia kwenye mawigi. Naomba turudi kwenye hina iko bado hina kavu inayotangwa imeandikwa humu yote.

Naomba sana turudi kwenye haya na wale wazee nimeambiwa majina yao pia yameorodheshwa wapo bado wale wazee aliowataja Naibu Waziri wangu ninamshukuru sana turudi kwenye mafunzo tutaepukana na mengi. Leo unamkuta mtoto mdogo hata hajatimia umri ameanza nywele zake kutia *relaxer* je, akifikia miaka 50 atakuwa na kichwa gani huyo? Nadhani mnanielewa sina haja ya kusema zaidi ya hayo. Watoto wadogo siku hizi juzi juzi wakati wa sikukuu nilikwenda pale kwenye uwanja kumpeleka mwanangu nikamkuta mtoto mdogo kavalishwa wigi karibu lile wigi limuangushe yule mtoto. Nikasema mbona huyu mtoto mdogo nikaambiwa ana matatizo ya vidonda, ninafikiri alitiwa dawa ikatoa vidonda. Kwa hivyo tuondokeni kwenye hizi *chemical* jamani turudi kwenye asilia. Ninaamini Wizara ya Utamaduni nayo itatusaidia kurudisha mafunzo haya ya asilia, tutaepukana na mambo mengi sana. Kwa hivyo Mhe. Chum Kombo Khamis tunakubaliana na wewe tunashukuru.(*Makofi*).

Mhe. Bahati Khamis Kombo Chambani, ushauri wako tumeupokea na hili suala la ubadilishaji la vipolo pamoja na tarehe, ubadilishaji hizi tarehe kwenye bidhaa za samaki kutoka nchi za nje, hili naomba nirejee tena tutaendelea kuwa wakali zaidi na Waheshimiwa Wawakilishi msije mkawaombea, mnakuja kuwaombea wakati mwengine watu wenu, tunakuombeni msije Wizarani kuwaombea watu wenu. Hili tutalichukulia hatua kwa sababu mwisho wa siku tunamlinda nani mwananchi aliyetuleta humu kuja kumtetea. Kwa hivyo hilo litaendelea naomba niwahakikishie na Bodi hii watakuwa wakali zaidi na wengi hawa ni Ma-Alhaji hawachukui hata rushwa, kwa hivyo si rahisi kuhongwa hawa.

Mhe. Naibu Spika, ushauri wa Mhe. Said Omar Said pia tumeupokea Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala litaendelea kudhibiti na bahati nzuri Mjumbe wa huku anaingia kwenye Baraza la Tiba Asilia. Kwa hivyo tutaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Juma Ali Khatib, Mhe. Salama Aboud Talib na Mhe. Zaina Abdalla Salum ushauri wenu tumeupokea tunakushukuruni sana. Mhe. Khadija Mohammed Kibano ushauri wako tumeupokea Wakala itashirikiana sana na wadau husika katika kudhibiti bandari hizi bubu kama nilivyoeleza.

Mwisho kabisa naomba tena Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe naomba sana niushukuru uongozi wa Baraza, niwashukuru watendaji wa Baraza, niwashukuru Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa kufanya Mswada huu kuwa mzuri na imara zaidi kwa ajili ya wananchi wa Zanzibar. Michango yenu

tumeithamini, tunaendelea kuithamini na yote tutaifanyia kazi pamoja na yale marekebisho ambayo tumekubali.

Sasa Mhe. Naibu Spika, naomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada ya kifungu. Naomba kutoa hoja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri ulikuwa utoe hoja tu ukwanza, hiyo ya pili ndiyo ulikuwa useme kwa ajili ya nani hii. Umetoa hoja sawa nenda kakae. Ni utaratibu, ni utaratibu Waheshimiwa Wajumbe sasa niwaulize Mhe. Waziri ameshatoa hoja wale wanaokubaliana na hoja hii wanyooshe mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Waziri urudi tena. Sasa ndiyo uliombe Baraza kukaa kama Kamati.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, sasa naliomba Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia Mswada huu kifungu baada kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Namba 2 ya 2006

Sehemu ya Kwanza

Utangulizi

Kifungu 1	Jina fupi na kuanza kutumika pamoja na marekebisho yake
Kifungu 2	Kusomwa pamoja na marekebisho yake

Sehemu ya Pili

Marekebisho

Kifungu 3	Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kusimama, lakini kwanza kabla sijatoa hoja yangu naomba nitumie sekunde 30 kusema yafuatayo, kwamba kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo ameifanya lakini pia nimpongeze kwa majumuisho yake mazuri ambayo ameyafanya, ametuonesha usikivu lakini pia amekuwa *considerate,* lakini pia amekuwa muungwana ku-*recognise* michango yetu ambayo tumechangia na sio ku-*recognise* tu lakini pia ametushukuru kwa kuboresha Mswada wake. Nadhani Mhe. Naibu Spika, hili liwe funzo kwa wengine kwamba sio kila kitu kinachokuja hapa kipo *perfect*.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, *for the first time* nimejihisi kama na mimi mtunga sheria. Kwa hivyo nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo wameifanya. Hoja yangu Mhe. Naibu Spika, ni kwamba wakati nilipochangia nilizungumzia kuhusu *reference* ambazo zimefanywa katika kifungu cha Bodi ya Ushauri, kifungu cha Wakala na kifungu cha Mkurugenzi Mtendaji.

Mhe**.** Naibu Spika, jana nilipata wasaa kidogo wa kukaa na Mhe. Mwanasheria Mkuu akanielewesha jinsi gani, Serikali isione wivu Mwanasheria Mkuu ni wa Serikali na sisi Baraza ni *part* ya Serikali. Kwa hivyo kama Baraza tuna haki ya kufanya *consultation* kwa Mwanasheria Mkuu. Kwa hivyo akanielewesha ni jinsi gani Mswada wa Marekebisho unavyosomwa na Mswada mama. Kwa hivyo hizi tunazoona kama *numbering,* sio *numbering* isipokuwa ni vifungu ambavyo vitakavyosomwa na Sheria mama. Kwa hivyo ninamshukuru Mwanasheria Mkuu lakini ninamshukuru na Waziri kwa ufafanuzi wake ambao ameutoa. Nadhani na wawakilishi wengine pia na wao wamejifunza. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tuendelee.

Kifungu 3	Marekebisho ya Kifungu cha 2 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 4	Marekebisho ya Kifungu cha 3 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 5	Marekebisho ya Kifungu cha 4 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 6	Marekebisho ya Kifungu cha 6
Kifungu 7	Kuongezwa Vifungu vipya vya 5A na 5B pamoja na marekebisho yake

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi wakati nikichangia jana nilizungumzia kuhusu kifungu cha 7(4) na nimemsikiliza Mhe. Waziri kwa makini kabisa lakini sikumsikia wakati anajibu hili. Kifungu cha 4 kinasema:

“Bodi ya Ushauri itamteua Mwanasheria na Wakala...", hili neno na lililokuwepo hapa linabadilisha maana nzima ya kifungu na nikapendekeza iwe "Bodi ya Ushauri itamteua Mwanasheria wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi".

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba niseme kweli kwamba hili neno hili linabadilisha maana. Kwa hivyo "Bodi ya Ushauri itamteuwa Mwanasheria wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi", tunakubaliana na marekebisho ya Mhe. Mwakilishi, tunakubaliana nayo ahsante. (*Makofi*).

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti hiyo ndiyo *spirit* tunayoitaka.

Kifungu 7 Kuongezwa vifungu vipya vya 5A na 5B pamoja na marekebisho yake

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti na mimi ningekichangia kifungu hicho nikasema kifungu cha 7 namba 4 ambacho Mhe. Waziri amekitolea ufafanuzi, nilisema hii ni miongoni mwa kazi za Bodi ya Ushauri. Nikashauri pia kwa sababu ni kazi basi ihamishwe kunako maeneo ya "Uwezo wa Bodi na Wajibu", kisibaki hapa. Sasa kiondoke hapa kiingie katika 5B(1) kwenye "Uwezo na Wajibu wa Bodi", kupata maelezo ya kina kwa Mhe. Waziri naomba niyapate kwenye hili.

Lakini la pili kifungu cha 7 hicho hicho 5B (1) nilizungumza kwa urefu sana na nikasema tunaandaa Bodi ya Ushauri ambayo kuna mamlaka mengine Mkurugenzi Mtendaji tumempa makubwa sana ya kuwa ataandaa Kamati, lakini leo hii tunajadili huku mbele kuna Idara, Bodi hii hatukuipa baadhi ya mamlaka ambayo yanaweza yakaja kusaidia, atakapokuwa na Idara mpya kinyume na hizi zilizokuwepo hapa zitakujabarikiwa na nani nikasema tusije tukarudi Barazani, basi tuone Mkurugenzi Mtendaji ataleta mapendekezo yake hapa kwenye Bodi ya Ushauri na Bodi ya Ushauri itakuwa na idhini ya kupitisha hiyo idara au Kamati ambazo zitzaundwa na Mkurugenzi Mtendaji sikupata majibu naomba nipate majibu na maelekezo ya vifungu hivi viwili.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na nashukuru sana kwa alilouliza Mhe. Miraji. Bahati mbaya hakuwepo humu ndani na mimi wakati nilikuwa najibu nilikuwa namwangalia, kwa hilo la pili nilitolea maelezo ya kutosha pale, lakini kwa hili la kwanza alosema sisi hatuna *objection* ya 4 ikija huku, ilipokaa hapa sisi tunaona sawa, lakini kama anataka kuweka huku na inasema kitu hicho hicho, haina na nini lakini hapa ilipokaa sisi tunaona iko sawa katika kifungu cha 5(b) "Uwezo na Wajibu wa Bodi", huku inasema Bodi ya Ushauri itamteuwa Mwanasheria wa Wakala kuwa Katibu wa Bodi. Huku

inaeleza Uwezo wa Bodi nzima. Hi ni kazi ni uwezo wa bodi. Kwa hivyo huku ilikokaa kiko sawa naomba atukubalie lakini kama atataka kiletwe huku, mwisho wa siku nadhani wanasheria watakuwa wanajua hili zaidi.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, hili la pili nililitolea ufafanuzi wa kutosha kwamba mtendaji huyu lazima apewe mamlaka ya kutosha na yawe yafanyike ndani ya muda mfupi yale maamuzi, yakiachwa muda mrefu tukampungumzia mamlaka tukayapeleka kwenye Bodi au tukayapeleka kwa Waziri, inaweza pakawa na *perishable goods* pale bandarini zinatakiwa kuwa-*penalized*, zinatakiwa kuwa-*destroyed* ikachukua muda mrefu patatoka harufu pale ya kuku na samaki na vifaa vyengine vilivyoharibika ama *chemical* zikaweza kutoa *reaction* pale bandarini pale zinazaweza kutokezea. Kuna ma-*liquid* yalishaletwa hapa ma-*chemical* sijui ya kuchanganyia ma *bleach* kutoa nguo na kadhalika, yalimwagia mengine yameleta athari kubwa sana. Kwa hivyo, tunasema hivi kwamba apewe mamlaka yeye ili uamuzi ule ufanyike ndani muda mfupi siyo kwa nia nyengine yeyote. Kwa sababu akinyimwa mamlaka hiyo akashauriane na Bodi, akashauriane na Wizara pengine ashauriane na Waziri itachukua muda mrefu sana. Ni hilo tu Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti mimi naomba nieleweke nayasema haya kwa nia safi kabisa. Mimi nina imani na Wakurugenzi wote nchini wa Serilikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. *(Makofi)*

Lakini kwenye jambo moja la msingi Mhe. Mwenyekiti, huku mbele tutaona kuna muundo wa zile Idara ambazo tunazipitisha leo na tukipitisha leo yawezekana mbele kukawa kuna *demand* ya Idara, huyu Mkurugenzi mwenye mamlaka ataelekea wapi au aendelee kurejeshwa Barazani. Sasa Waziri anachonijibu tofauti ndio maana nikasema Uwezo wa Bodi tumeunyima alau ule tutakapoanzisha Idara mpya, aidha twenda kwenye ile Bodi ya Ushauri ikaidhinishe au tutoke pale twende huko kwa Waziri ambapo yeye pengine anakukumbia.

Lakini utanuzi wa hii Taasisi utakuwepo tu kulingana na mahitaji huko mbele tusijekuwa tunarudi hapa Barazani kila siku, mimi sina nia mbaya anifahamu vizuri. Mhe. Mwenyekiti, naomba nipate maelezo.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mwenyekiti, naomba niseme kwamba na sisi pia tuna imani sana Mhe. Miraji na kama walivyokuwa wananchi wake wa Jimbo la Chumbuni wana imani na yeye na sisi hivyo hivyo tuna imani naye na tunaelewa nia yake safi, wala hilo halina shaka. Lakini naomba niseme hivi kuhusu Idara, kifungu cha 7, Kifungu cha 9 ni marekebisho ya 7(2)

nimekitolea maelezo mwisho wa Kifungu 7(2) baada ya (a), (b), (c) na (d) zile Idara zimetajwa. Kifungu cha 7(2) zinasema kwamba Wakala inaweza kuanzisha Idara nyengine au vitengo kama itakavyoona inafaa Wakala. Wakala ni Mkurugenzi pamoja na watendaji wenzake yaani *collective responsibility* itafanyika hapo.

Na kwa upande huu mwengine suala lake Mhe. Mraji kwa sababu *collective responsibility* tayari inafanyika, mimi nahisi hakuna haja ya ku-*involve* wizara, *although powers* hizi kama sasa hivi mimi ndio Waziri zitakuwa zinaletwa kwangu mimi *powers* hizi, lakini nahisi hapana tumuachie ili tuweze kufikia malengo yetu kwa sababu malengo yetu huko mbele tunataka kuelekea *authority* kama wenzetu hawa wakishajiweza vizuri kifedha, wakishaweza kusimama miguu yao vizuri, hawa watakuwa ni *authority* kamili baadaye. Kwa sababu wenzetu wote sasa hivi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ni *authority* kasoro sisi tu. Sasa hii ni *transition* kutoka kwenye Wakala kuelekea kwenye *authority*.

Naomba sana Mheshimiwa utukubalie, tutakuja tena Barazani wakati tunataka kufanya Mamlaka kamili ya *authority* yaani kwenda huko kwenye *food and drug*, mamlaka yao kamili ya *authority* lakini kwa sasa hivi...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa zungumza na kiti, umeshaeleweka zungumza na kiti, naomba ukae Mheshimiwa.

Mhe. Miraji nafikiri Waziri sidhani kama atakuwa na maelezo zaidi ya hayo aliyoyaeleza, kwa sababu ameshaeleza vizuri sana. Sasa kama unataka kwa sababu ametumia neno tufanya *collective responsibility* hapa, huu Mswada sote sisi tunaupitisha pamoja na wewe.

Na hilo ambapo unalolizungumza unasema wewe ndo unahisi hivyo. Sasa utanifanya mimi nipigishe kura, mpige kura tukubaliane kwamba tuendelee na hivi ambavyo Mswada wenyewe ulivyo sasa hivi tuachane na mabadiliko unayoyataka.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, mimi sizungumzi na Mhe. Mahmoud kama majibu yote katoa peke yake, nazungumza na Serikali.

Sasa hii ni mara yangu ya tatu, naomba sina tatizo naomba nieleweke isipokuwa katika maelezo yangu kama mnanifahamu vizuri Mkurugenzi huyu wa Wakala majukumu ya Kamati ukimwachia, majukumu ya Idara ukimwachia, mimi nilisema yale ya Idara Mhe. Waziri ainuke akubali basi

kiingizwe kipengele yabarikiwe na kamati, idara inapata muda mrefu tusiyapeleke majukumu yote kwa Mkurugenzi huyu anaweza akaja akatufikisha sipo, mkaja mkarudi humu tumetunga Sheria siyo alau iwe inashirikisha ile taasisi yake mwenyewe, maana Bodi hii ya pale pale.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, nitakuja kukumbukwa kama Mhe. Waziri anahisi haina haja Mkurugenzi tumuachie tueendelee, mimi sina tatizo.

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru Mhe. Mraji tunaendelea.

Kufungu 7	Kuongeza vifungu vipya vya 5A na 5B pamoja na marekebisho yake
Kufungu 8	Marekebisho ya Kifungu cha 6

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru lakini Mhe. Waziri ametoa maelekezo katika kifungu cha 8, cha marekebisho ya Kifungu cha 6 (2) (c), hapa kwenye uzoefu kwa kazi angalau kwa kipindi cha miaka 7 amelitolea ufafanuzi. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme tena bado kwamba ushauri wangu atauona unafaa. Sisi hapa Zanzibar kiwango chetu cha kugombea Urais miaka 40 unaruhusika. Sasa katika *level* ambayo Mheshimiwa ameiweka mtu aliyekuwa na shahada ya pili, uwe na uzoefu wa miaka saba, bado ni Mkurugenzi tu hajafika hata Waziri, bado unamuwekea mikwala tena miaka 7, basi si angalau 5. Nilikuwa nashauri hapo Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Sarahan, Mhe. Waziri alilijibu vizuri sana nina wasi wasi kwamba ulikuwa hupo wakati analijibu hili. *(Makofi)*

Mhe. Waziri kama unaweza kumjibu mjibu kwa ufupi sana naomba.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, jibu ndio kama hivyo ulivyolieleza, nilitolea jibu la kutosha kwamba wasiwe na wasi wasi wapo vijana wenye miaka saba *experience* na wana *masters degree*, mpaka sasa hivi Zanzibar wako zaidi ya saba hao vijana wenyewe.

La pili, mtu hawi mzee siku hizi mtoto anamaliza *masters* miaka 24 mpaka 25, ukiweka *working experience* ya miaka saba ni 32. Kwa hivyo 35 anaingia anakuwa mdogo kuliko Rais wa Zanzibar umri wake wa kugombania urais umeshanifahamu. Kwa hivyo Mheshimiwa naomba atukubalie sana hapo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naendelea mimi kutoa yale ambayo niliyasema kifungu hicho cha 8(b) ambacho kinazungumza Shahada ya Pili kama alivyozungumza mwenzangu.

Kwanza hapa pana Mwanasheria Mkuu, pana Waziri wa Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora; tunayo Sheria mama ambayo mara nyingi Sheria ya Utumishi haitakiwi kukinzana na Sheria ambazo tunakwenda nazo. Watendaji wetu hawa tunavyowatafuta tunaanza na *degree* ya mwanzo na zile kurugenzi zenyewe.

Sasa kuja kutunga Sheria nimo humu ndani kama Mwanasheia Mkuu hajanipa tafsiri nyengine inayoniruhusu kufanya hivi, kupingana na Sheria mama, siwezi kukubaliana na kifungu ambacho kiruhusu *degree* ya pili kwa sababu ya ule u-*special* wa maelezo aliyozungumza Waziri hau-*matter* kama tunavunja Sheria mama ya Utumishi Serikalini.

Sheria ipo Namba 2 ya Mwaka 2011 kama sijakose kidogo, sasa turudi nipate maelezo hayo. Sheria mama inatwambia watumishi hawa wanapatikana kwa *level* ya *degree* na kuendelea. Sasa leo huyu anakuja kutupa taasisi ambayo inapokea *degree* ya pili na mtumishi hajatoka kwenye Sheria ya Utumishi. Naomba maelezo.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, nishukuru pale alipokuwa Mhe. Waziri alipokuwa akijibu vizuri tu, naye nimpongeze kwa kazi nzuri ambayo alikuwa amefanya. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nimemsikiliza Mhe. Miraji Khamis Mussa na hoja yake ya Shahada ya Kwanza na ya Pili. Mhe. Waziri amezungumza hili na amelitolea ufafanuzi. Kwanza nikubaliane na Mhe. Miraji kwamba ukisoma Sheria ya Utumishi wa Umma kwenye baadhi ya maeneo ambayo yanatakiwa ajira, basi *minimum* kinachoaanza kuwa na Shahada ya Kwanza. Lakini kama amemsikiliza vizuri Mhe. Waziri wa Afya alipokuwa akifanya majumuisho amesema kwenye hii na sisi tunafuata *Regional Boards* ambazo nazo pia kuna utaalamu wake ambao unatakiwa na utaalamu wa hawa watu wanaosimamia vyombo hivi wawe na Shahada inayoanzia ya Pili. Hivyo ndivyo Mhe. Waziri amesema. Nadhani ni busara kukubaliana kwa sababu na sisi kama nchi ni *signatory* kwenye hii mikataba ambayo tunai-*sign*. Sasa kwa sababu hiki ni kiwango ambacho kimewekwa, mimi nadhani hoja hii iliyokuwepo isimame kama ilivyo na hoja ambayo Mhe. Miraji Khamis ameitoa itaendelea kutumika kwenye zile ajira nyengine ambazo zinatakiwa mtu basi angalau awe na Shahada ya Kwanza.(*Makofi*).

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, naanza kupata tabu sana na tunapoacha Sheria ya humu ndani ambayo tumeitunga wenyewe, hii tunaikiuka kwa sababu kuna eneo limeshaweka vigezo. Sasa tunapozungumza Sheria ya Utumishi Serikalini na ndio Sheria mama lazima tufuate hii, tunapokuja kufanya hizi teuzi kwani imetukataza kumteuwa mtu wa Shahada ya Pili. Lakini hapa iendelee kusomeka isipingane na Sheria mama, kwa sababu tukitunga Sheria hii tukisema twende kwenye Shahada ya Pili tushakinzana na Sheria mama iliyopitishwa na chombo hiki.(Makofi).

Mhe. Mwenyekiti, sasa si wakati wa kwenda kama Mwanasheria Mkuu alivyosema kwamba twende kwa busara, hatuwezi kwenda kwa busara kwa kukiuka Sheria ya nchi tuliyotunga wenyewe. Nataka twende kwenye mantiki nimalizie kunako hili, mimi naomba sana tuibadilishe iwe ianze *degree* ya kwanza, maana yake hatutakatazwa kumchagua mtu mwenye *Professor*, mwenye PhD, mwenye hiyo digrii ya pili kama alivyosema, lakini sisi tufuatane na Sheria mama ilivyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye eneo hilo hilo nilipoinuka nilianza na hoja ya mwanzo na hoja nyengine ya ziada ambayo ilikuwa inanipelekea kwenye Ufamasia. Sasa naomba uniruhusu kuwa tumalizane na hii au niende na huko kabisa kwa sababu nina maneno mawili kwenye kifungu hicho. Uniruhusu wewe maana nisije nikakaa ukaninyima haki ukanihesabia muda niliosimama.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji Khamis Mussa tunamaliza hii kila kifungu tunakipitisha, ikiwa mtu ana hoja ndio atasimama kwa kifungu kile, huwezi kwenda kifungu chengine wakati umesimama wakati huu, sema hicho ambacho umesimamia tumalizane nacho halafu utakwenda kwenye hicho kifungu ambacho unataka kusema.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Nadhani Mhe. Mwenyekiti, hujanifahamu vizuri. Kifungu ninachozungumzia ni (b) kina kesi mbili. Kesi ya mwanzo kwa Sheria ya Utumishi kwenye kifungu hicho kwa Shahada ya Pili. Kesi ya pili ni Ufamasia. Waziri kajibu vizuri na nilikuwa namsikia, kesi mbili tofauti ndio maana nikasema nikae mimi kwa kesi moja, tuizungumze moja moja lakini ikimaliza tuzungumze ya pili, lakini kifungu hicho hicho cha (b) sitaki...

Mhe. Mwenyekiti: Viseme vyote kabisa.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Haya. La pili katika majibu ya Waziri nilikuwa namsikiliza kwa makini akatueleza Sheria nyingi ambazo zinatulazimisha kwenda kwenye Ufamasia. Hii hapa alii-*quote* katika maelezo yake, *Africa*

Union Model Law. Kifungu cha 10 alikizungumza ndani ya Baraza hili na naomba nikisome, hicho kifungu cha 10 alichosema kinaturuhusu kwenda katika utaratibu wa kwenda kwenye Ufamasia hakiruhusu. Kwanza mimi hapo napinga na yeye alisema kinaruhusu, uruhusu watu kwa ujumla wake kifungu cha 10(a) naomba Mwenyekiti nikisome.

Kifungu cha 10(a) kinasema kwamba:

"The head of agency or authority shall be appointed by appointing authority on the recommendation on the board shall be hold suitable qualification in medicine pharmacy, nursing, veterinary medicine or public health"

Hakimzungumzi mtu mmoja. Hii ni *Africa Model Law* ya mambo haya tunayoyazungumza na ameki-*quote* humo kinatupeleka kwahala moja. Sasa kama zilivyo sifa hizi ndio maana nazungumza jana tusiwanyime fursa tukaandaa matabaka. Kwa sababu hata hizo Jumuiya tunazoishi nazo zinaturuhusu.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, kwenye jambo hili naomba Mhe. Waziri anijibu yote mawili kwa pamoja na mimi kwenye hili tukielekea huko, nasema kabisa tupige kura nishindwe nijue nimeshindwa lakini nitetee madaktari wengine wenye .....*(Makofi)*

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, labda kwanza nianze hili la kufuata Sheria hizi za kimataifa ambazo na sisi kama nchi wakati mwengine huwa tunazifuata. Kila nchi kuna utaratibu wake na kuna taratibu za aina mbili. Kuna nchi ile sheria ilivyo ya Kimataifa inaridhia kama ilivyo, inapotoka inapotiwa saini na wakuu wa nchi inapoletwa kwenye nchi husika basi ile nchi huridhia kama ilivyo. Lakini kuna nchi kama sisi tunapotia saini ile mikataba inapokuja kwenye nchi yetu inabidi tu-*domesticate*, inabidi tuitungie Sheria na unapoitungia Sheria huna maana ufuate kama kilivyokuwemo na ndio maana tuna-*domesticate.*

Mhe. Mwenyekiti, wale wengine wao wameamua kufuata kama ilivyo na Sheria ya Kimataifa inaruhusu hivyo ufuate kama ilivyo, lakini wengine kina sisi tuna *domesticate.* Maana yake tunachukua ile na tunatizama kipi ambacho kina maslahi na sisi ndio tunaamua kukitungia sheria. Sasa inawezekana Mhe. Miraji ametaja hiyo *Model Law* akataja kwa Mafamasia, akataja na nani, sawa ndio ilivyo lakini sisi wakati tunatunga sheria tunatizama kipi ambacho sisi kitatuvusha kwa wakati huu ambao tunao, na ndio maana *qualification*

tukaweka hizi na hatujachukua zote ambazo zipo. Sasa huu ni utaratibu ambao kisheria unakubalika, *otherwise* tungeamua kuchukua kama ilivyo ile tukaifanya ndio sheria ya nchi yetu. Lakini hapana, sisi inabidi tutizame yale ambayo yanatufaa na ndio yale tunayoyatungia sheria.(*Makofi*).

Kuhusiana na elimu nirudie kusema Mhe. Mwenyekiti, kama Mhe. Miraji angesoma kifungu cha 70 cha Sheria ya Utumishi wa Umma angeona katika sifa ambazo zimetajwa haikuwekwa kiwango cha elimu ambacho mtu huyu anatakiwa kuwa nacho, kwa sababu kuna ngazi nyengine inategemea na elimu ambayo mtu anatakiwa kuwa nayo. Na ndio maana kifungu kikawacha wazi kama inapotokea kutunga sheria na kuamua kuchagua mtu basi ile kazi na ile sifa ambayo anatakiwa awe nayo ndio i-*determine* kwa wakati ule, ndio kifungu cha 70 kinavyosema. Sasa nadhani nimefafanua vya kutosha zaidi ya hayo nadhani Mhe. Miraji ametoa *option* Baraza nalo pia lina uamuzi wake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji unasimama mara ya mwisho.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, la mwanzo unaninyima haki kwa sababu vitu vyangu vilikuwa viwili, cha shahada ya pili na fani ya sayansi Famasia.

Mimi naomba Baraza hili lijue kama tunaishi na wafanyakazi wa kada tofauti kwenye Bodi hii na wakati huo huo zile Sheria za Afrika, ukienda *EAC* hata hawa *TFDA* pia Sheria zao zipo, kuna sheria za Uganda. Mimi nimepitia sheria nyingi karibu saba kwa Mswada huu mmoja. Kwa hivyo, ningeliomba Mhe. Mwenyekiti, kada hizi ambazo hazikatai na sisi Baraza liridhie, Mhe. Waziri aridhie twende. Mapendekezo mnafanya nyie huko mbele mtachagua hao Wafamasia mpaka weshe, lakini na hao wengine angalau Sheria ya nchi iwataje mtakuwa mnaunda tabaka ambalo si busara wakati haitukatazi sisi kuwapa uongozi hawa. (*Makofi*).

Baraza hili tunajadili sheria mbele ya kiongozi wetu mkuu Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunamuundia tabaka kweli, na Mawaziri mkubali tu msielekee huko, maana hapa ma-*nurses* wanatusikia…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa hoja yako imeshafahamika…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Hapa watu Wafamasia wanatusikia lakini watu wa *public health* wanatusikia, wewe Waziri ndio unaoishi nao, kwa sababu unawaundia tabaka sasa hivi. Mhe. Mwenyekiti, si nafasi yangu ya mwisho niseme…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Miraji mimi nazungumza…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, si nafasi yangu ya mwisho niseme…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nazungumza, nikizungumza wewe unanyamaza na unakaa kitako ndio utaratibu wetu.

Mheshimiwa nasemaje hili ambalo wewe unalitaka Mhe. Waziri tayari ameshaelezea kwa nini libakie hivi hivi, lakini Mhe. Mwanasheria Mkuu tayari ameshaelezea kwa nini libakie hivi hivi na hoja hii kila mtu anaona kwa nini hapa panatakiwa watu ambao tayari wawe na *profession* fulani, huwezi kumuweka mtu mwenye *degree* ya kwanza hususan wepesi wa ile *degree* yenyewe, anatakiwa mtu mzito. Sasa Mheshimiwa hili sio la kujengea hoja na kukataa kupitisha hiki kifungu, mimi sioni uzito wa hoja yako.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: *Degree* ya kwanza…

Mhe. Mwenyekiti: Umeshamaliza sasa hivi siwezi kukupa ruhusa tena Mheshimiwa, tumemaliza…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Sasa Mwenyekiti…

Mhe. Mwenyekiti: Tunaendelea…

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Mhe. Mwenyekiti, hapana kutokubaliana na kifungu…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa kaa kitako, nataka kupiga kura sasa.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walipiga kura)

Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada ubakie kama hivi ulivyo naomba wanyooshe mikono. Naomba kura zihesabiwe, wanaokataa. Naomba kura zihesabiwe. Wanaokubali wameshinda. Tunaendelea.

(Kura ilipigwa na walioafiki mswada wameshinda)

Kifungu 8	Marekebisho ya kifungu cha 6 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 9	Marekebisho ya kifungu cha 7 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 10	Marekebisho ya kifungu cha 12

Kifungu 11	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 13A pamoja na marekebisho yake
Kifungu 12	Kufutwa kwa kifungu cha 14 pamoja na marekebisho yake
Kifungu 13	Kuongezwa kwa vifungu vipya cha 15...

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi sina swali isipokuwa nahitaji ufafanuzi kwa Mhe. Waziri, hiki kifungu cha 13 kinarekebisha kifungu cha 15A, 15B na 15C. Kifungu cha 15A kinasema uwazi na ubadilishaji wa taarifa naomba nikisome.

> "Wakala ataanzisha mfumo wa usimamizi kwa kuzingatia mapendekezo ya mashirikiano ya pamoja ya kikanda ili kuleta ubora na uwazi katika utekelezaji wa kazi",

Lakini Kifungu cha 15B kinasema:

> "Mtu hatoruhusiwa kutoa kwa mtu mwengine au taasisi yoyote taarifa aliyoipata katika utekelezaji wa kazi au wajibu wake chini ya sheria hii".

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba nimuulize Mhe. Waziri. Hapa tulisema kwamba kuna taarifa kwa mfano mimi niko jimbo ama mwananchi aliona kuna sehemu kumeingizwa madawa kinyume na sheria, ama kuna mchele mbovu umeingizwa kinyume na sheria. Jee, mtu yule sasa asitoe taarifa mpaka amsubiri yule labda wakala au mjumbe wa bodi ndio aje? Hapa mimi nilikuwa nataka nijibiwe.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naona lilitolewa ufafanuzi hili lakini naona nirejee tena tu kwa sababu ametaja vifungu viwili, ametaja kifungu cha 15A nadhani hilo halina tatizo moja wakala itaanzisha mfumo wa usimamizi.

Kifungu cha 15B mtu hatoruhusiwa kutoa kwa mtu mwengine au taasisi yoyote taarifa aliyoipata katika utekelezaji wa kazi au wajibu wake chini ya sheria hii inayohusiana na kazi au jambo lolote linalomuhusu mtu yeyote au kutumia taarifa hiyo kwa manufaa binafsi au kwa faida ya mwajiri wake. Hii inakusudia kwa wafanyakazi hawa wakala wenyewe, ni wafanyakazi wa wakala kwa sababu mle Mhe. Mwenyekiti, kuna taarifa nyingi za siri, kuna *trade business*, kwa sababu leo kama umeleta kontena wewe tuseme mfano mheshimiwa la kuku wabovu nikishatoa taarifa zako mimi zile za siri, wewe biashara yako ndio imeshavunjika. Hata ukitaka kuleta kuku wazima mara ya pili ushalipa lako la kuleta, sitaki kutaja majina lakini umeshalipa jina lako la kuleta

matatizo. Kwa hivyo, ndio maana hii inamdhibiti mfanyakazi aliyekuwemo ndani kwa sababu hivi vitu ninavyo hapa mimi nimeletewa, hizi *documents* zipo hapa baadhi yake ni siri. Kwa hivyo, inamlinda yule mfanyakazi wa wakala. Ahsante mheshimiwa.

Mhe. Ali Bakari Khamis: Tuendelee Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 13	Kuongezwa kwa vifungu vya 15A, 15B na 15C pamoja na marekebisho yake
Kifungu 14	Marekebisho ya kifungu cha 20
Kifungu 15	Marekebisho ya kifungu cha 27
Kifungu 16	Kuongezwa vifungu vya 60A, 60B na 60C pamoja na marekebisho yake
Kifungu 17	Kuongezwa kifungu kipya cha 61A pamoja na marekebisho

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru katika kifungu cha 61 nilipochangia nilisema kwamba kifungu cha 61 kinampa mamlaka Waziri akishakugundua kwamba bidhaa zina madhara na pia anakuwa ameshakubaliana na Bodi kuwa bidhaa hii ina madhara, ukisoma Sheria mama ile ndio inasema hivyo 61, lakini kifungu cha 61A kinasema kwamba:

> “Kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 61(1) cha sheria hii, *(ambacho Kifungu 61 ndio kile kipo kwenye Sheria mama)* wakala anaweza kuelekeza kwamba bidhaa za tiba ziondolewe katika soko na ziharibiwe kwa mujibu wa masharti ya sheria inayohusika na kwa namna ambavyo imeelezwa katika kanuni zilizotungwa chini ya sheria hii”.

Sasa kama Waziri tayari na Bodi yake wameshakubaliana kama bidhaa hizi ni mbovu na hazifai. Halafu kifungu cha 61A kinasema wakala inaweza kuelekeza, kwa hivyo haimshurutishi Wakala kwamba ameshagundua kuwa bidhaa hizi ni mbovu ziteketezwe "anaweza". Kwa hivyo, yeye atakavyoamka ata-*decide* kwamba bidhaa ni mbovu nikitaka nita-*order* ziteketezwe nisipotaka haziteketezwi. Nadhani kifungu kimshurutishe Wakala kwamba akishajua kuwa bidhaa hizi mbovu na hazifai, basi sheria moja kwa moja ielekeze kwamba bidhaa zile ziwe *destroyed*. Kwa hivyo, badala ya kuweka Wakala inaweza kuelekeza isomeke, "Wakala itaelekeza", kwa sababu tayari weameshagundua kwamba hizi bidhaa ni mbovu na hazifai kwa matumizi ya binadamu.

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimshukuru sana tena sana, sana Mhe. Wanu kwa kuyaona haya na naweza kusema amekwenda *deep* kidogo.

Kifungu hiki hata mimi katika majadiliano huko Wizarani niliwahi kukiuliza na maelezo ya kifungu hiki naomba nikitolee.

Naomba nimjibu Mheshimiwa kwamba kifungu hiki kimewekwa kama *provision* wakati mwengine nitachukua mfano wa hivi karibuni uliotokezea ulimwenguni, zilitolewa simu za *Samsung Galaxy* baadae ikagundulika kwamba betri yake ina *chemical* hatarishi ambayo ukipanda kwenye ndege au sehemu nyengine inaweza kuripuka. Simu zile zote kiwanda kikaruhusu zirejeshwe haraka iwezekanavyo na *regulation* ya hayo yamefanyika. Kwa hivyo, kifungu hiki naomba Mhe. Wanu atukubalie kina *provide provision* kama ile dawa imeshasambazwa Tanzania nzima, imeshaingia madukani ikaja kugundulikana *defect* yake ile dawa baada ya miezi mitatu au miezi minne au mitano kuweko dukani, wakala anaweza baada ya kupokea *defect* kutoka *industry* kusema kwamba *recall this medicine*, akaenda kwenye maduka na kuzitoa kwenye *shelves* kwenda kuziteketeza. Kwa hiyo, kifungu hiki mbali ya kile kifungu cha sheria mama kilichopo hiki kina-*provide additional provision* kwa ajili yaku-*recall* zile dawa kuziondosha dukani. Nadhani atakuwa amenifahamu mheshimiwa. Ahsante.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru Mhe. Waziri wa ufafanuzi lakini hicho kifungu mama najua kama hii ni *proviso* ya kifungu cha 61(1), lakini hicho kifungu mama tayari bidhaa zishakuwa hazifai kwa matumizi ya binadamu mnasubiri mpaka kiwanda kiitishe kwamba bidhaa hizi hazifai huku wangapi watakuwa wameshaathirika. (*Makofi*).

Mimi nadhani madhali wakala imeshakuwa *certisfied* kwamba hizi bidhaa hazifai apewe *mandate* ya kuamua kwamba bidhaa hizi hazifai na ziteketezwe moja kwa moja na sio "anaweza", wanaweza wakamfuata watu huko wamuhonge au wafanye nini abadilishe maamuzi. Nadhani sheria ielekeze moja kwa moja bidhaa hazifai ziteketezwe. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tena nijaribu kutoa ufafanuzi mzuri zaidi, nafikiri Mhe. Wanu hakunifahamu.

Naomba kutoa ufafanuzi hivi, wakati mwengine inatokezea na ishawahi kutokezea nchi nyingi dawa inatolewa na *industries* yaani kiwanda kile cha dawa kishakuwa *approved* wamefata *process* zote dawa inatolewa, inakuwa

distributed ulimwengu mzima, ishawahi kutokezea kwenye kampuni ile sitaki kuitaja dawa lakini ile ya kuondosha gesi tumboni. Dawa zile zinasambazwa ulimwengu mzima baadae *industry* au kimataifa huko wenyewe wanagundua, hapa sisi kila kitu kinapata *approval* zinafaa, zimekubaliwa, zimethibitishwa, zimeingia nchini kwa usalama wote. *Industry* yenyewe inatuma barua jamani eeh! naomba mzi-*recall* hizi dawa kumetokea *industrial defect.*

Kosa lilotokea kwenye *industry*, nimetoa mfano wa simu za *Samsung* imetokea *industrial defect* katika betri yake tu *Samsung*, simu zote zile zikarudishwa duniani na wanakupa *Samsung* nyengine mpya na pesa ya fidia wanakulipa. Sasa ninachotaka kusema dawa hizi zinaingia kwa *approval* zote nchini lakini ikitokea ile *industry effect* na *industry* ile imetoa taarifa zile dawa zimeshasambaa katika soko baada ya miezi ya sita imetoka taarifa ile, ni wajibu wetu na wajibu wa Wakala kurudi kule kuchukua. Sasa tukimuwekea *blank statement* hivi hivi, ukiwa na kisasi au chochote anaweza kwenda kuchukua akasema hizi hazifai, lakini akiwa na *evidence* kutoka *industry* ya kusema kwamba hizi ni *defective goods.*

Mhe. Mwenyekiti, natoa mfano mwengine tulishawahi kuletewa nyama sisi hapa kutoka Makka hii inayochinjwa ya mbuzi, na mimi mwenyewe nilikula mmoja wapo. Ile nyama baada ya kuletwa hapa iligaiwa mote lakini tukaharisha kama ngisi wakati huo nazungumzia miaka kama 20 iliyopita. Ile nyama kila aliyekula tukaja kuuliza…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda ameshafahamu…

Mhe. Waziri wa Afya: Naomba kidogo…

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nafikiri hicho unachokielezea unaendelea kueleza kile kile ambacho tayari umeshakielezea. Sasa mheshimiwa naomba ukae turudi kwa mtoa hoja.

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Mwenyekiti, kama ambavyo Mhe. Wanu alivyosema, ukisoma ile Sheria mama yenyewe utaona kuna makatazo ambayo yamewekwa, lakini ile *loophole* ambayo imeonekana na ambayo nadhani ndio Mhe. Wanu anaielezea kama pamoja na yote ambayo yameelezwa kwenye sheria ile, Wakala ilikuwa haikupewa mamlaka ya kusema sasa bidhaa hizi sasa ziwe *destroyed*. Sasa anachosema Mhe. Wanu mimi nadhani iko sahihi, kama lazima hapa iwe *shall* na isiwe *may*. Kama sasa baada ya yale yote kuonekana sasa Wakala na kama alivyofafanua Mhe. Waziri kama ile bidhaa ukiona haifai

na ulishairuhusu sasa wewe ulazimishe iondoke ndani ya duka usiibakishe.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Kifungu kimekubaliwa.

Wajumbe: Ndio.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri hoja yako imekubalika kwa mujibu alivyozungumza Mhe. Mwanasheria Mkuu kwamba kutafanywa marekebisho badala ya kuwa *may* itakuwa *shall*, nafikiri kwenye Kiingereza, nafikiri ni hivyo kama una hoja nyengine zaidi.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na wewe kabisa kama hoja yangu imekubalika, lakini na mimi mtoa hoja nina haki ya kusimama ya kusema kwamba nakubaliana au sikubaliani.

Mhe. Mwenyekiti: Haya sema.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee kiroho safi.

Kifungu 17	Kuongezwa kifungu kipya cha 61A pamoja na marekebisho yake
Kifungu 18	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 73A
Kifungu 19	Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 93A pamoja na marekebisho yake
Kifungu 20	Kuongezwa kifungu kipya cha 119A pamoja na marekebisho yake
Kifungu 21	Marekebisho ya kifungu cha 123
Kifungu 22	Kuongezwa kifungu kipya cha 124A...

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi kwanza nimshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na ufafanuzi ambao ameutoa wakati anajibu kifungu hiki. Kiuhalisia amenipa *termination* mpya hiyo ya *plea bargaining* ambayo nilikuwa siijui lakini kwa kuwa tunaruhusika kuingia na kompyuta mpakato nika-*search* haraka haraka katika *American Bar Association* nikaona kwamba hata makosa ya jinai yanaruhusika kusikilizwa nje ya Mahakama kama yule anayeshitakiwa anakubali kwamba lile kosa amekubali, kwa hivyo hata ikisikilizwa nje ya Mahakama inakuwa iko sawa, hilo namshukuru sana Mhe. Waziri na namshukuru kwa elimu ambayo amenipa.(*Makofi*).

Lakini katika kifungu hiki kulikuwa kuna hoja ambayo nimejibiwa na Mhe. Waziri kuhusu Mkurugenzi kushauriana na Bodi wanapogundua hiyo ilikuwa sio hoja yangu, nadhani walichanganya labda ilikuwa ya Mheshimiwa mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hoja yangu ya pili ilikuwa katika kifungu 124A(1) kuna neno “Kurugenzi Mtendaji”. Nikasema kwamba hakuna kitu kama hicho katika Sheria hii "Kurugenzi Mtendaji" na isipokuwa lile neno lisomeke “Mkurugenzi Mtendaji” kama linavyo-*appear* kwenye tafsiri.

Mhe. Waziri wa Afya: Nimekubali Mheshimiwa.

Kifungu 22	Kuongezwa kifungu kipya cha 124A pamoja na marekebisho yake
Kifungu 23	Marekebisho ya jadweli

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru tena wewe binafsi pamoja na uongozi mzima pamoja na Waheshimiwa Wawakilishi wote kwa michango yao mizuri sana ambayo imeimarisha Sheria yetu.

Mhe. Naibu Spika, sasa ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali pamoja na marekebisho yake yote, sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ameshatoa hoja niwaulize wale wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.(*Makofi*).

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2016

(Kusomwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba niseme jambo dogo tu kabla sijasoma…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nenda moja kwa moja kwa sababu muda hamna.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya 2016 usomwe tena kwa mara ya tatu. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mhe. Waziri ametoa hoja wale wanaokubaliana na hoja, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupitishwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwashukuru sana kwa kufanikisha kupitisha Mswada huu na sasa hivi tumebakisha dakika 20 kwa saa ile ninayoitizama mimi kule mbele. Na bado tuna ratiba yetu ya leo inatutaka leo tumaliza kujadili ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Kwa hivyo, nitamuomba Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atuongezee dakika 10 tu tuweze kumaliza Mwenyekiti aisome tumalize.

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakipinga hoja ya Mhe. Naibu Spika kwa kupiga kelele)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa jioni muda hautotosha mpaka tumalize, hautotosha. Waheshimiwa Wajumbe, nawahoji lakini ripoti hii tunaimaliza leo jioni nataka niwaambie hivyo, Waheshimiwa nawaomba sana tumalize ripoti

hii leo jioni ndio ratiba yetu inavyosema Waheshimiwa, ratiba yetu inasema tunamaliza leo basi tutamaliza saa 4 ya usiku hapa. (*Kicheko/Makofi*).

Waheshimiwa Wajumbe kwa maana hiyo nafikiri nyote mmeridhia kurudi jioni tuanze jioni na kamati. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa kwa utulivu wenu pamoja na ushirikiano mzuri ambao mmefanya kuhakikisha kwamba Mswada huu umepita vizuri.

Baada ya kusema hayo nasitisha kikao mpaka saa 11:00 jioni leo hii, ahsanteni.

(Saa 6:42 mchana Baraza liliahirishwa mpaka saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

TAARIFA ZA KAMATI

Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa Mwaka 2016/2017

Mhe. Omar Seif Abeid: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawaklishi ya Mwaka wa Fedha 2016/2017.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu muweza wa yote, kwa kutuwezesha sote kuwa na afya njema na kukutana tena katika Mkutano huu wa Tano wa Baraza la Tisa. Ni ukweli usiopingika kuwa, huu si uwezo wetu bali ni wake yeye *Allah Subhanahu Wataala,* ambaye ametujaalia kuuona tena mwaka huu wa 2017, kwani ni wengi ambao hawakubahatika kuushuhudia mwaka huu, lakini pia wapo ambao wameushuhudia wakiwa ni wagonjwa vitandani.

Hivyo basi, sisi tunaoendelea kupata neema ya uhai na uzima hatuna budi kusema "*Alhamdulillah*", na pia kuwaombea wale waliokuwa wagonjwa kupata nafuu. Aidha, hatuna budi kuendelea kumshukuru Allah *Subhanahu Wataala*, kwa kuendelea kulibarikisha taifa letu kwa kuwa na amani, kwani kila uchao tumekuwa tukiona na pengine kusikia machafuko mbali mbali na umwagikaji damu na jinsi gani inavyoendelea kutokea katika mataifa ya wenzetu. Ni vyema basi tukaendelea kuidumisha amani hii kwani kama tujuavyo hakuna mbadala wa amani na amani ikishatoweka ni vigumu kuirudisha. Kwa msingi huo

nawasisitiza wananchi wenzangu kuilinda amani tuliyonayo kwa ajili ya manufaa ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako tukufu, kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimsmia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka wa fedha 2016/2017, kwa niaba ya Kamati yangu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maneno hayo machache ya utangulizi, sasa naomba nijielekeze katika lengo la kuwepo kwangu hapa. Lakini kabla ya kuendelea na chochote, napenda kutamka kwamba, huu ninaouwasilisha ni muhtasari wa Ripoti ya Kamati. Hivyo, ripoti yote kwa ujumla wake ambayo tayari Wajumbe wameshakabidhiwa kabla, sambamba na muhutasari huu naomba uingie katika "*hansard*" za Baraza.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa imeundwa kwa mujibu wa Kanuni ya 106 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi na kufafanuliwa pamoja na majukumu yake katika jadweli la kwanza la kanuni hizo ambapo majukumu yenyewe ni kama yafuatayo:-

i. Kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati yaliyotolewa katika ripoti ya kamati ya mwaka uliotangulia

ii. Kufuatilia utekelezaji wa sera na mipango ya wizara husika kwa kadri Spika atakavyoelekeza na kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizozitoa hapa Barazani.

iii. Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi kwa Wizara husika.

iv. Kuchunguza na kufuatilia mapato na matumizi ya kila mwaka ya serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

v. Kuchambua mapendekezo ya serikali kuhusu makadirio ya wizara husika ya mapato na matumizi ya kila mwaka.

vi. Kushughulikia Miswada ya Sheria itakayokabidhiwa kwake na Spika.

vii. Kuchambua ahadi zote za wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekelezaji wa ahadi hizo.

viii. Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ilitekeleza shughuli zake za kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya kamati, ahadi za serikali, kazi za kawaida na za maendeleo, ukusanyaji wa mapato na matumizi pamoja na kufanya ziara katika Wizara za Serikali ambazo zipo chini ya kamati hii ambazo ni kama zifuatazo:-

- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
- Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Kwa ujumla, kamati imefanya kazi kwa takriban wiki sita, kwa muda wa wiki zote hizo kamati imeweza kufanya kazi zake katika idara na taasisi zilizo chini ya wizara hizo kwa upande wa Unguja, Pemba na Dar – es –Saalam Tanzania Bara.

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwa mashirikiano yao, yaliyopelekea leo hii kuwasilisha ripoti hii ya mwaka 2016/2017. Naomba kuwatambua na kuwataja kwa majina Wajumbe hao kama hivi ifuatavyo:-

1.	Mhe. Omar Seif Abeid	Mwenyekiti
2.	Mhe. Panya Ali Abdallah	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mjumbe
4.	Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Mjumbe
5.	Mhe. Mussa Ali Mussa	Mjumbe
6.	Mhe. Mtumwa Suleiman Makame	Mjumbe
7.	Mhe. Simai Mohammed Said	Mjumbe

Aidha, kamati ilishirikiana na makatibu wawili katika kazi zake nao ni:-

i.	Ndg. Maryam Rashid Ali	Katibu
ii.	Ndg. Kassim Tafana Kassim	Katibu

OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeundwa na idara na taasisi zifutatazo:-

- ❖ Idara za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni:-
    - Ofisi ya Faragha ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais,
    - Idara ya Uendeshaji na Utumishi,
    - Idara ya Mipango Sera na Utafiti,
    - Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ, SMT, Utafiti na Masuala ya Muungano,
    - Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam,
    - Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa,
    - Idara ya Watu wenye Ulemavu,
    - Ofisi kuu Pemba,

- ❖ Taasisi zilizochini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ni:-

    - Baraza la Wawakilishi,
    - Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi,
    - Tume ya Uchaguzi Zanzibar,
    - Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa,
    - Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Dawa ya Kulevya,
    - Wakala wa Serikali wa Upigaji chapa Zanzibar,
    - Tume ya UKIMWI na
    - Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu.

TUME YA KITAIFA YA URATIBU NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Kitaifa ya Uratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya inahusika katika vita ya kitaifa dhidi ya usafirishaji, usambazaji, uuzaji na utumiaji wa dawa za kulevya. Kushamiri kwa biashara ya madawa ya kulevya ni kitu kinachowaumiza sana vijana wengi ambao ndio nguvu kazi ya taifa letu.

Pamoja na kazi nzuri sana inayofanywa na Tume hiyo kwa kuzipatia ruzuku nyumba za kurekebishia tabia (*Sober house*) na kutoa elimu kwa umma juu ya athari ambazo zinapatikana kwa watumiaji wa madawa ya kulevya. Kwa hivyo,

tunatoa wito kwa serikali kuongeza nguvu maradufu kwenye mapambano ya uingizaji, usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya na tunaiomba serikali zoezi hili liwe endelevu.

Ni wazi kuwa Tume inafanya kazi nzuri sana lakini bado inakabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo kwa namna moja au nyengine inarudisha nyuma jitihada kubwa zinazofanywa na Tume. Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa vitendea kazi kama vyombo vya usafiri kwa ajili ya ufuatiliaji wa majukumu yake, kukosa mashirikiano ya karibu baina ya wana jamii na vyombo vinavyohusika na kusimamia suala hilo kama vile Polisi, Mahakama pamoja Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Sererika, na kubwa zaidi ni kule kunakotajwa kuwa ni kukosa meno ya kisheria kwa tume hii kunakosababishwa na mapungufu ya kisheria ya tume, ambako pia kunapelekea tume kushindwa kusimamia kesi zinazohusiana na dawa za kulevya na hivyo kupelekea kuzorota kwa uendeshaji wa kesi hizo na kuchukua muda mrefu, hatimae kuishia njiani au kutolewa hukumu ambazo hazilingani na uzito wa makosa yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imeliangalia zaidi tatizo hili la dawa za kulevya kwa upana wake, kwa kushirikiana na watendaji wa Tume na kufanya ziara katika maeneo mbali mbali ambayo ndio milango mikuu ya kuingia nchini, ikiwa ni pamoja na Bandari na Viwanja vya Ndege. Pia katika ziara hizi, Kamati yangu ilibaini kuwa, hakuna udhibiti wa kutosha wa uzuiaji wa kuingiza dawa za kulevya kwa upande wa viwanja vya ndege. Hivyo ni rahisi kutumika katika uingizaji wa dawa hizo, kama ilivyoelezwa katika ripoti ya kamati hii kwa mwaka 2016/2017.

Kwa ujumla Kamati imeshauri ipasavyo ili kupunguza changamoto za Tume ikiwa ni pamoja na kuipa uwezo zaidi Tume kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo kama inavyoonekana katika ripoti hii.

TUME YA UCHAGUZI ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, kamati imeridhishwa na namna Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inavyoendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku, katika kuhakikisha inatoa huduma bora na endelevu kwa wananchi wake wa Zanzibar. Miongoni mwa chanagamoto zilizobainika na kamati katika Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar ni pamoja na ufinyu wa majengo ya ofisi kwa ajili ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Kwa sasa jengo la Tume hiyo kwa upande wa Unguja linatumika kwa Wilaya tatu kwa wakati mmoja na kupelekea kukosa utulivu wakati wa utekelezaji wa majukumu yake.

Changamoto nyengine ni kukosa ghala la kuhifadhia vifaa vya uchaguzi na usalama wa mdogo wa jengo la Ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar kunakosababishwa na kuwepo wazi eneo la ofisi, kuchakaa kwa magari mengi yanayotumika katika shughuli za Tume na changamoto nyengine kubwa ni ile ya dhana na mawazo potofu ya baadhi ya wana jamii kuamini kuwa Tume hiyo ni ya chama fulani cha siasa jambo ambalo si sahihi hata kidogo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pamoja na mambo mengine, Kamati imeshauri wizara husika, kutafuta namna ya kuwapatia ofisi za Tume ya Uchaguzi Zanzibar kwa kila Wilaya, japo kwa kukodi majengo ya watu binafsi.
Kwa mnasaba wa changamoto ya jengo na ofisi ya Tume, Kamati yangu inatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Rais wa Zanzibar, Dkt. Ali Mohammed Shein kwa ziara yake aliyoifanya katika Ofisi ya Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar tarehe 13/02/2017 na kuahidi kwamba majengo ya Tume yatafanyiwa maboresho makubwa kabla ya kufikia uchaguzi wa mwaka 2020. Hivyo, Kamati yangu inawaomba watendaji wa Tume kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wakiamini kwamba changamoto zao tayari zimepatiwa ufumbuzi.(*Makofi*).

WAKALA WA SERIKALI WA UPIGAJI CHAPA ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, kamati imeridhishwa na kufurahishwa sana na hali ya Kiwanda cha Uchapaji kwa sasa, kutokana na maboresho makubwa yaliyofanywa na kuekezwa katika miundombinu ya kiwanda hicho. Kiwanda kimepatiwa mitambo ya kisasa yenye uwezo mkubwa kama vile *folding mashine, web set off* mambo ambayo yanahitaji wataalamu wenye ujuzi katika uendeshaji wake, jambo ambalo bado ni changamoto kwa kiasi fulani kwa kiwanda hicho.

Mbali na uwekezaji huo mkubwa, kiwanda pia kinahitaji mtaji mkubwa na wa kutosha kuweza kujiendesha, *"Running Capital"* kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya kila siku ya kiwanda hicho na kuhimili hali ya ushindani wa kibiashara. Jambo jengine ni ukosefu wa ghala la kutosha kwa ajili ya kuhifadhia bidhaa, ambalo linaendana na uwezo wa uzalishaji wa kiwanda hicho. Changamoto nyengine ni ucheleweshaji wa malipo ya huduma zinazotolewa na kiwanda hicho hususan kwa taasisi za serikali kwa kulimbikiza madeni kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Spika, ili kupunguza makali ya changamoto hizo, kamati imeshauri Wakala wa Serikali wa Upigaji chapa kuchukua wataalamu kutoka kwenye

makampuni binafsi, ndani na nje ya Zanzibar ili kufidia pengo la ukosefu wa wataalamu wanaohitajika kiwandani hapo. Pamoja na kuwatengezea mazingira mazuri kwa kuwapatia maslahi mazuri na motisha nyengine kwa watendaji hao, ili waendelee kutoa huduma bora kiwandani hapo.

Kamati pia imeshauri kuharakishwa kwa ujenzi wa ghala jipya la kiwanda cha upigaji chapa, ambalo litakuwa na nafasi ya kutosha inayoendana na ukubwa wa kiwanda hicho.

Mwisho kabisa ili kuongeza wigo wa ushindani katika soko, kamati imeshauri kufanyike zoezi maalum la kukitangaza kiwanda hicho kwa umma, kwa lengo la kuongeza wateja na uelewa juu ya ubora na huduma zinazotolewa kwa sasa, sambamba na serikali kutoa tamko maalum kwa taasisi zake zote na kuzitaka kukitumia kiwanda hicho kwa ajili ya machapisho na kazi zote zinazohusu uchaopishaji ili kukipa nguvu kiwanda hicho na kukabiliana na ushindani wa kibiashara.

IDARA YA KUKABILIANA NA MAAFA

Mhe. Naibu Spika, kamati inaipongeza Kamisheni ya Maafa kwa jitihada inazochukua katika kukabiliana na maafa ya namna mbali mbali yanayotokea katika visiwa vya Unguja na Pemba. Lakini pamoja na kazi kubwa iliyofanywa na idara hii, bado idara imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbali mbali ambazo zimekuwepo kwa muda mrefu sasa. Changamoto hizo ni pamoja na ukosefu wa ghala la kuhifadhia vifaa vinavyotumika wakati yanapotokea maafa kwa upande wa Pemba, ufinyu wa bajeti na ukosefu wa eneo maalum lililotengwa kwa ajili ya wahanga wa maafa mbali mbali ya kimazingira, kama vile mafuriko kwa sasa. Mara nyingi yanapotokea maafa hutumika madarasa ya skuli kuwahifadhi waathirika wa majanga, jambo ambalo kwa upande mwengine linaathiri ufanyaji kazi wa sekta nyengine kama sekta ya elimu, kwa kuwakosesha watoto muda wa masomo yao, kwa sababu ya madarasa hizo kutumika na wahanga hao.

Kwa hivyo, kamati imeshauri kutazama namna ya kupata fedha na kuipa kipaumbele cha bajeti, ujenzi unaoendelea wa ghala la maafa liliopo Unguja na kuanza kwa ujenzi wa ghala jipya kama hilo kwa upande wa Pemba. Sambamba na kutafutwa eneo maalum ambalo pia litaekewa miundombinu ili kutumika endapo kutatokea maafa ya kijamii, ili kuepuka usumbufu na kuleta ufanisi zaidi katika idara hii.

TUME YA UKIMWI

Mhe. Naibu Spika, Tume ya Ukimwi imeundwa kwa lengo kubwa la kuunga mkono na kuongeza nguvu katika vita dhidi ya maambukizi ya Virusi vya UKIMWI. Pamoja na taarifa nzuri juu ya jitihada za serikali za kuunga mkono tume, kamati iligundua kuwa bado idara inakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti ambayo inalingana na taasisi nyingine, sambamba na changamoto kubwa ya kuwanyanyapaa waathirika wa Virusi vya UKIMWI wakiwa kazini, hali ambayo imekua ikijitokeza hata katika Idara na Taasisi za Serikali, Mashirika ya Umma na ya watu binafsi.

Kamati katika kuona kwamba kunahitajika kutanua wigo mkubwa wa uelewa, imeishauri Tume ya UKIMWI Zanzibar, kulipa kipaumbele suala la utoaji wa elimu na kuhamasisha umma, juu ya athari za virusi vya ukimwi, na kamwe kamati inatoa wito kwamba; wasibweteke kutokana na takwimu kuonesha kwamba kumepungua kwa kiasi kikubwa maambukizi ya Virusi vya Ukimwi hapa Zanzibar.

IDARA YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SMZ, SMT, NA MASUALA YA MUUNGANO

Mhe. Naibu Spika, idara inaenedelea kutekeleza majukumu yake ya kuratibu shughuli za idara kwa kupitia Kitengo cha Uratibu wa Miradi, inayosimamia miradi mbali mbali ukiwemo mradi wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), ambapo kwa sasa mfuko huo unaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskni chini yaani (TASAF III).

MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI (TASAF III)

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, pamoja na kazi nyengine ilipata maelezo pamoja na kujionea utekelezaji wa mradi huu wa TASAF III ambao umejikita katika kunusuru kaya maskini, ambapo kamati ilipatiwa taarifa kuwa, jumla ya kaya 204 kwa Unguja na Pemba (Unguja 126 na Pemba 78) zinaendelea kunufaika na mpango huu, kwa hupatiwa ruzuku kwa ajili ya kujikimu pamoja na ruzuku za masharti ambapo pamoja na mambo mengine, kaya inatakiwa kutimiza na kutekeleza masharti ya afya na elimu ili iweze kunufaika na mpango huo.

Aidha, kamati inatoa pongezi kwa serikali kupitia mpango huu wa kunusuru kaya maskini, kwani walengwa wamekuwa wakinufaika sana, kupitia ajira za muda mfupi, ambazo zinatokana na miradi mbali mbali inayoibuliwa kwa

walengwa, kama vile miradi ya uchimbaji wa mabwawa ya maji kwa ajili ya kilimo, n.k. Ni wazi kuwa kupitia mpango huu wananchi ambao ni walengwa wa mradi, wananufaika katika kujipatia kipato, kuwasomesha watoto na kuwapatia huduma za afya na hata Bima ya afya, jambo ambalo ni muhimu sana kwa ya jamii yetu katika maisha kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu katika mzunguko wa mwisho wa kazi za kamati ulioufanywa kabla ya kuwasilisha ripoti hii, ilipata nafasi ya kufika katika kijiji cha Kivule kilichopo katika kata ya Soga, wilaya ya Kibaha mkoani Pwani, na kujifunza mambo mengi kuhusiana na mpango huu wa kunusuru kaya maskini, yaani TASAF III. Kwa ujumla walengwa wananufaika na mradi huo kwa kiasi kikubwa, na kupitia ruzuku wanazopatiwa wamejiendeleza kwa kuanzisha miradi midogo midogo kama vile ya ufugaji wa mbuzi, kuku na bata pamoja na kuekeza fedha zao katika ushirika maalum wa vikoba.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imefurahishwa sana na maendeleo ya mpango huu, na kwa upande wa Tanzania Bara, hivyo tunawaomba waratibu wa TASAF kwa upande wa Zanzibar, kuiga yale mambo mazuri ambayo ni maendeleo ya wenzetu, ili na sisi Zanzibar wananchi wetu waweze kujiendeleza kupitia mpango huu. Pamoja na hatua kubwa za kimaendelea zilizopigwa katika mpango wa TASAF III, kupitia mpango huu wa kunusuru kaya maskini, kumekuwa na baadhi ya changamoto ambazo ni pamoja na kuwasajilli watu wasiokuwa na sifa na kuwaacha wale wanaostahiki. Kwa kuliona hili na kwa ajili ya utekelezaji bora wa mpango huu, kamati yangu inaagiza kufanyika kwa uhakiki wa kina kwa walengwa wa mpango huu, kwa lengo la kuwabaini wale wote wanaonufaika ambao hawastahiki katika mpango huo na badala yake kuzinyima fursa kaya ambazo zinastahiki kuingia katika mpango huu na kunufaika kama serikali yetu ilivyokusudia.

OFISI YA RAIS, NA MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi hii ina muundo ufuatao:-

a. Ofisi ya Faragha
b. Idara ya Mawasiliano Ikulu
c. Idara ya Ushirikiano wa Kimataifa na Uratibu wa Wazanzibari wanaoishi Nje ya Nchi
d. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
e. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
f. Idara ya Usalama wa Serikali (*GSO*)

g. Idara ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Sera na Maamuzi ya Serikali
h. Ofisi ya Baraza la Mapinduzi
i. Ofisi ya Afisa Mdhamini – Pemba

OFISI YA FARAGHA

Mhe. Naibu Spika, ofisi inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku, ikiwa ni pamoja kutoa huduma za faragha kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Barazi la Mapinduzi. Licha ya ofisi hii kuhusika na kumuhudimia Kiongozi Mkuu wa Nchi, pia imekua na changamoto mbali mbali zinazoikabili katika utekelezaji wa majukumu yake.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti inayokusudiwa kukarabati na kuenedeleza nyumba zinazotumika kwa Mhe. Rais wa Zanzibar, ambazo kamati imebaini nyingi zao kutokua na hadhi inayoendana na hadhi ya Mhe. Rais kwa sasa, hasa ile ilioko kule Laiboni Dar es Salaam, pamoja na usalama mdogo katika baadhi ya nyumba hizo.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine ambayo ni ile ya kimazingira ambayo ni pamoja na kuwepo kwa athari kubwa za mmong'onyoko wa ardhi, changamoto ambayo inaonekana kuwepo takriban katika nyumba zote zilizo chini ya ofisi hii. Sambamba na hilo, kamati inapongeza kwa juhudi kubwa zinazoendelea za matengenezo makubwa ya kuzuia athari za mmong'onyoko wa udongo katika Ikulu ya Mkoani, na nyumba zilizoko Chake Chake, ni vyema matengenenzo haya yakaendelea katika nyumba zote zenye athari hiyo zilizo chini ya ofisi hii, ili kuepuka madhara makubwa zaidi, pamoja kusisitiza juu ya suala la usafi katika maeneo yanayozunguka nyumba za mapumziko za Mhe. Rais.

IDARA YA USALAMA WA SERIKALI (*GSO*)

Idara inaenedelea kutekeleza majukumu yake ya kila siku katika kuhakikisha usalama wa serikali, kupitia upekuzi (*vetting*) ya watumishi wa umma na shughuli ambayo inahitaji kuwa endelevu ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wake.

Idara ya Usalama wa Serikali ni muhimu sana kwa ajili ya Usalama wa Serikali yetu, licha ya umuhimu wake, bado imekua na changamoto kadhaa ambazo zinakwamisha juhudi za idara hiyo. Miongoni mwa changamoto hizo ni uchakavu wa jengo linalotumika kwa sasa na idara hii, ambalo kwa ujumla haliendani na hadhi na unyeti wa idara husika pamoja na unyeti wa shughuli

zake, ufinyu wa bajeti uliokithiri na kuzorotesha utekelezaji na ufuatiliaji wa majukumu ya idara, na ukosefu wa vitendea kazi vya msingi ikiwa ni pamoja na vyombo vya usafiri kwa ajili ya ufuatiliaji wa majukumu yao ya kila siku.

Mhe. Naibu Spika, kamati yangu imeshauri kulifanyia ukarabati mdogo jengo la *GSO* linalotumika kwa sasa, ili liweze kuwa na hali nzuri na lenye kutazamika, wakati ambapo wizara inakusudia kufanya ukarabati mkubwa unaokusudiwa kufanywa katika majengo yaliopo maeneo hayo ya Ikulu. Aidha, kamati pia imeagiza yafanyike marekebisho ya sheria inayosimamia kuwepo kwa *GSO* Zanzibar, ambayo kimsingi ni moja kati ya changamoto zilizopo katika idara hii kwa sasa.

IDARA YA MAWASILIANO IKULU

Mhe. Naibu Spika, idara inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha inamuunganisha Kiongozi Mkuu wa Nchi na jamii, kwa upatikanaji wa taarifa mbali mbali, na habari zilizo sahihi na zinazokwenda na wakati. Idara hii ni yenye umuhimu mkubwa katika kuhakikisha inajenga, inaboresha na inalinda taswira nzuri ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Pamoja na utekelezaji bora wa kazi zake za kila siku, lakini bado kumekua na changamoto kubwa zilizobainika katika idara hii, ambazo ni pamoja na mabadiliko ya haraka ya TEHAMA, ukilinganisha na kiwango na uwezo wa kukabiliana na mabadiliko hayo kwa idara husika, hali inayopelekea kuwa nyuma ya muda katika maendeleo ya tasnia ya habari.

Aidha, kamati imebaini changamoto nyengine ambayo ni kuwepo kwa muamko mdogo kwa baadhi ya viongozi wa kisiasa katika kuwaelezea wanachama wao na wananchi kwa ujumla, kuhusu utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi, na mafanikio ambayo yamefikiwa katika uongozi wa awamu hii, iliyo chini ya Dkt. Ali Mohammed Shein Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine pia kuna changamoto ya kukosekana kwa fursa ya kutosha na muda kwa vyombo vya habari kwa ajili ya kuandaa, kuonesha na kutangaza vipindi maalumu kwa kila wiki, kwa ajili ya uelewa wa wananchi kufahamu mafanikio tuliyoyapata na kuwaeleza wananchi wetu tulipotoka na wapi tulipo sasa, na nini hasa dhamira ya Rais wetu na dhamira ya serikali yake kwa jumla dhidi ya wananchi wake. Changamoto nyengine ni kukosekana kwa huduma za kimtandao kwa baadhi ya maeneo na kusababisha

kuzorota na kuchelewa kwenda hewani kwa taarifa na vipindi muhimu vinavyomuhusu Mhe. Rais na ofisi yake kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, kwa ujumla kamati imeshauri idara kuchukua hatua za makusudi na za haraka, kutoa taarifa kwa umma kuhusiana na upotoshwaji wa ukweli wa mambo yanayomgusa Mhe. Rais, kupitia vyombo vya habari kama vile TV na Redio. Ni vyema kuandaa vipindi vinavyohusiana na taarifa za Mhe. Rais kwa kila wiki. Kufanya hivyo, kutalinda na kuonesha uwezo na hadhi ya Rais wetu ambaye ndio kiongozi mkuu kwa taifa hili.

Sambamba na hilo kamati pia imeshauri kutokana na mabadiliko ya TEHAMA, idara ielekeze nguvu zake zaidi katika kutumia njia mpya za upokeaji na utumaji wa habari yaani *New Media* kama mitandao ya kijamii, ikiwa ni pamoja na "*facebook"*, na "*Twitter"* ambayo ina watumiaji wengi hususan vijana, yenye mawanda mapana na isiyohitaji gharama kubwa.

OFISI YA BARAZA LA MAPINDUZI

Kamati imepata fursa ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambayo kwa kiasi kikubwa imekua ikitekeleza majukumu yake bila kuwepo kwa changamoto za kibajeti, ambazo zingekwaza utekelezaji wa majukumu yake kinyume na taasisi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, changamoto pekee iliyopo kwenye ofisi hii kwa sasa, ni kukosa eneo la kutosha na lenye nafasi kwa ajili ya uwekaji wa maktaba inayokusudiwa kutengenezwa katika Ofisi za Baraza la Mapinduzi, ili iweze kutumika kwa Waheshimiwa Mawaziri wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

Kutokana na mabadiliko ya haraka ya ulimwengu katika masuala ya TEHAMA, kamati imeshauri zoezi la kuanzisha maktaba katika Ofisi za Baraza la Mapinduzi lifanyike sambamba na kuanzishwa kwa maktaba ya kielektroniki "e-*library*", ili kuwawezesha Waheshimiwa Wajumbe kutumia huduma hizo katika muda na mahala popote wanapoihitaji kutumia huduma hiyo.

OFISI YA AFISA MDHAMINI – PEMBA

Mhe. Naibu Spika, ofisi inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi, kwa upande wa Pemba kwa ufanisi mkubwa lichya ya kuwepo

changamoto mbali mbali. Miongoni mwa changamoto za ofisi hii zinalingana na changamoto zilizopo katika taasisi nyingine zilizo chini ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ambazo ni pamoja na kuwepo kwa athari kubwa za mmong'onyoka kwa ardhi katika majengo ya ofisi, licha ya kufanyika kwa ukarabati mkubwa katika miaka ya hivi karibuni.

Changamoto nyengine ni kukosekana kwa maegesho rasmi yaliyojengwa kwa ajili kuhifadhia magari ya Viongozi Wakuu, ambapo kamati imeshauri kutengwa kwa eneo maalum katika eneo la ofisi na kujengwa kwa maegesho maalum ya kuhifadhiwa magari ya viongozi hao.

MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA SERIKALI

1. Kamati inapendekeza kuundwa kwa kamati maalum itakayojumuisha Wabunge na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, ili kufuatilia mambo mbali mbali yanayohusiana na Muungano na Miradi ya TASAF, ambayo inatekelezwa kwa pande zote za Jamhuri ya Muungano.
2. Katika kuhakikisha kwamba vita dhidi ya Dawa za kulevya inaendelea, ulinzi na upekuzi uimarishwe katika njia kuu za kuuingilia katika nchi yetu, kwa maana ya Viwanja vya Ndege na Bandari kuu, lakini pia kudhibiti bandari bubu ambazo zinaweza kutumika katika uingizaji na usafirishaji wa dawa za kulevya.
3. Kamati inapendekeza kuanzishwa kwa mfuko maalum wa kuchangia fedha za maafa ambao utakuwa endelevu kwa ajili ya kuhudumia maafa yanapotokezea, kuliko kusubiri hadi maafa yatokee ndio watu wachangie fedha, na misaada kwa ajili ya maafa na majanga mengine.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi kukushukuru tena kwa kuniruhusu kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, pamoja na kuwashukuru Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa usikivu wao, nawaomba waijadili, waiboresha na hatimae kuipokea ripoti hii

Mhe. Naibu Spika, katika kuona kunakuwa na utekelezaji mzuri zaidi wa majukumu ya kila idara zinazosimamiwa na kamati, tumetoa maoni, ushauri na maagizo mbali mbali, ambayo tunaamini yakitekelezwa yatazisaidia sana taasisi zetu. Sambamba na hilo tunachukua fursa hii kwa niaba Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa ofisi hizi muhimu, kwa mashirikiano yao

waliotupatia katika kutekeleza majukumu ya kamati. Ni imani yetu kwamba bila ya mashirikiano yao, basi tusingeweza kupata ripoti kama hii hapa leo.

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua nafasi hii maalum kumshukuru Mhe. Naibu Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mashirikiano yake aliyotuonesha katika wakati wote wa ziara yetu tulipokuwa kule Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: (Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa): Mhe. Naibu Spika, samahani. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Waheshimiwa majadiliano yanaanza, nina wachangiaji saba mpaka sasa hivi. Nitaanza na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, atafuata Mhe. Mohamedraza Hassanali, na baada ya hapo atafuata Mhe. Masoud Abrahman Masoud.

Waheshimiwa Wajumbe, naomba sana muda muutumie kama vile Kanuni inavyotuambia. Naomba sana kwa sababu wachangiaji watakuwa wengi. Mkitumia muda mrefu wengine watakosa nafasi ya kuchangia. Kwa hivyo, nawaombeni kila mjumbe atakayeanza kuchangia atachangia kwa muda wa dakika 15 tu, ahsanteni.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Bismillah Rahman Rahim. Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu utaanzia kwenye Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, kwenye suala la Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Kudhibiti Madawa ya Kulevya. Mhe. Naibu Spika, kwa maoni yangu mimi, bado Zanzibar suala la madawa ya kulevya lipo na tena lipo sana na mpaka hadi sasa hivi. Nafikiria kama kuna awamu iliyopita nyuma na sasa hivi basi mimi naweza kusema bado kazi haijafanyika vizuri. Kama kazi imefanyika basi kazi iliyofanyika ni kidogo. Suala hili sijui kwa nini inatokea kwamba mpaka hii leo suala hili halijapungua au halijakaa katika mstari uliokuwa mzuri.

Nafahamu kwamba suala la madawa ya kulevya ni zito, lakini uzito wake unachangiwa kwamba lina watu wazito. Sasa kwa maana hiyo suala kama hili kutibika pia ni zito.

Mhe. Naibu Spika, mimi ningeomba sana kwenye suala hili tujitolee, hakuna kuogopa hakuna kutishika na wenye majukumu ya kufuatilia suala hili basi wajitolee muhanga, lakini kwa njia ya kiistaarabu na inayokubalika. Kwa sababu tumeona kwamba mfano mdogo wenzetu wameanza na utaratibu ya kutumbua masuala haya ya madawa ya kulevya lakini walikosea utaratibu na wakaenda sivyo na badala yake wakafahamu.

Lakini kwa upande wetu wa Zanzibar kutokana na nchi yetu ni ndogo na hali tunaiona basi ningeomba *system* itumike mtu hata kama mmeshamjua aitwe, ahojiwe, amechunguzwa amekamatwa mtoeni kwenye TV. Lakini mwanzo kuja kuadhirishwa mtu pengine atakuwa hana kosa amedhaniwa tu, halafu akaja akachunguzwa mkaja mkasema kwamba mmemkamata hana kitu itakuwa ni tatizo na itakuwa ni aibu kwa serikali kwamba imebahatisha.

Suala hili limeshatokezea kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa, mnamjua mwanzo kazungumza vitu kawataja baadhi yao, wapo ambao aliowatumia na kuna ambao amewadhania ambao sio wauzaji, lile ni tatizo. Na hapa Zanzibar ifikie hatua tutumie akili zetu kwenye *system* ambazo tunazo wenyewe kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuna mambo sio ya kuiga kuiga. Maana yake nimegundua kuna baadhi ya viongozi wakiona mwenzao kapiga marufuku kwa hivi na yeye huku anaiga, kataja hivi na yeye huku anataja, kiongozi utumie akili yako mwenyewe. Mfano mdogo mimi nampongeza sana Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, s*ystem* anayokwenda nayo ni yake mwenyewe kwa akili aliyojaaliwa na Mwenyezi Mungu, hamfuati mtu.(*Makofi*).

Kuna baadhi ya Wawakilishi hapa na kuna baadhi ya viongozi walizungumza Mhe. Rais eti na yeye atumbue kama anavyotumbua Mhe. Joseph Pombe Magufuli. Hicho kitu hakiwezekani, kila mmoja ana elimu yake na ana uongozi wake. Mhe. Dkt. Shein ni mzoefu katika serikali hii kuliko baadhi ya viongozi waliyokuwepo Tanzania. Nafahamu Rais wetu wa Tanzania ni kiongozi nambari moja kwa Tanzania na yeye Mheshimiwa kwa *protocol* ni mtu wa tatu, lakini ana hekma, anajua nini anachokifanya na anakwenda kwenye masuala ambayo yanatakikana. Lakini ukiangalia viongozi wengine wapo kwenye kuvamia wanataka sifa matokeo yake wanafeli.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa masuala haya ukiangali yote kwenye kifungu namba 2, 3, 4, na changamoto zinazokabili Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya, ufinyu wa bajeti, ukosefu wa vyombo vya usafiri kwenye kutafuta masuala hayo na kutokamilika kwa kesi ambazo za watu wanaokamatwa na madawa ya kulevya. Hii inaonesha dhahiri kwamba ndani ya serikali au ndani ya vyombo inaonekana kwamba kuna watendaji wana-*support* madawa ya kulevya na ndio maana masuala haya yanakwama. Kwa sababu hii inaonesha dhahiri, hivi kweli taasisi kama hii au idara kama hii tumeshaona haya madawa ya kulevya muhimu tunaambiwa bajeti haitoshi, gari hawana. Hivi kweli hebu tuambieni nyinyi wenyewe Waheshimiwa Mawaziri mliokuwepo mbele, gari mnazotumia ni milioni mia mbili, mnashindwa kutoa gari ya milioni ishirini kwenda kufanya kazi kwenye masuala haya. (*Makofi*).
Mhe. Naibu Spika, hapa tupo na ndio maana nikasema tutakuja kuangamia humu ndani na hatutofika popote. Leo tupo tayari tujifurahishe sisi, tutembee na magari mazuri, kuna Wawakilishi Wajumbe wenzangu wanatembea na gari ya milioni nane tu hapo nje na wameridhika. Lakini nyinyi Waheshimiwa Wakubwa mliokuwepo mbele wenye wizara hizi kwa ujumla kwa sababu hii ni Wizara ambayo imebeba Mawaziri wote inawasimamia Mawaziri wote, kwa ufupi nyote mimi nasema na najiamini kwamba mnachokifanya sio sahihi. Kwanza muacha kutembea na magari mazuri mnunue gari hizi za madawa ya kulevya. Kama kuna bajeti haijatimia na nyumba mbovu, uzeni magari yenu kajengeni nyumba hizo ili watu waache kutumia madawa ya kulevya na masuala mengine.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, leo mtu anakamatwa na unga unaona hasa huu unga, mnakuja kuambiwa baada ya wiki ule uliokamatwa unga wa kupimwa wa kuuzwa. Inasikitisha sana lakini mimi namuomba Mhe. Rais kwa kushirikiana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais watu wameamua kufanya kazi, wafanye kazi kihaki lillahi. Dawa za kulevya wanajua wapi zinauzwa na Zanzibar ni ndogo na laiti humu ndani ingekuwa kuna pombe au bangi masuala mengine tuseme tuanze kuchunguza humu ndani ya ukumbi, basi robo inakwenda na maji. Hiyo ni dhahiri tunazungumza ukweli, ninazungumza ukweli, humu ndani mimi sitaki kumdhania mtu lakini kila mmoja anajua Zanzibar unga wapi unauzwa, ukenda Nungwi kumechafuka, Mjini kumechafuka, watu wanajulikana hasa wanaouza unga lakini wanaachiliwa. Sijui kwamba watu wanaogopwa nini, mmepewa madaraka msiogope.(*Makofi*).

Mhe Naibu Spika, mimi ningekuwa si Mwakilishi ningemuomba Mhe. Rais anichague kile kitengo niwe ni Polisi wa yale masuala ya madawa ya kulevya na kama inawezekana hivyo mimi Mhe. Rais namuomba aniteuwa na uwakilishi wangu nitafanya kazi hiyo. Lakini hivi tunavyokwenda tutafeli

lazima tuwe wawazi, tuwe wakweli, ifike wakati vitu ambavyo havina maana tuweke pembeni tufanye vitu ambavyo vyenye maana. Madawa ya kulevya yameuwa watu, leo ukiangalia kesi zote za madawa ya kulevya mtu anakamatwa na kete moja, kakamatwa na bangi na wanaokamatwa wote ni wavutaji sio waletaji. Mhe. Naibu Spika, wa kukamatwa ni waletaji, wasambazaji na wauzaji sio wavutaji, wavutaji tunawaonea tu, wavutaji ilikuwa ni kuwakamata na mkawapeleka Mahospitali kuwaachisha unga sio muwaweke ndani. Sisi tumetembea kwenye jela waliokamatwa karibu asilimia 99 ni wavutaji, mnawaonea, ifike hatua muwaachie, muwatibu, mnazidi kuwakandamiza.

Mhe. Naibu Spika, ilisemekana kipindi cha nyuma kuna Mapolisi walikuwa wanaingiza unga kuwapa wafungwa wanaovuta unga ndani katika watu waliokwenda kutembelea huko waliowahoji wafungwa, hili ni tatizo. Lakini kama nilivyoeleza hili suala linasikitisha. Kwanza hawa walioandika mimi ninawapongeza sana hii hotuba kwa sababu wamekuwa wawazi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakuomba dakika 20 kwa sababu hapa naona kwa hali hii Wizara hii nzito dakika 15 hasa mnatuonea hatufiki kokote, na ndio maana tunazungumza masuala mengine hata hayafahamiki tunaripu ripua, kwa sababu dakika hazitoshi ingekuwa mnatupa dakika zetu tungekwenda kidogo kidogo tukafahamika, haya ni matatizo. Mimi Mhe. Naibu Spika, naomba sana kwa jambo hili Mhe. Waziri yupo wa Wizara husika kama kuna masuala ya magari uzeni kajengeni hivi vitu, tembeleeni na gari aina ya *Corolla* kama tunavyotembelea sisi Wawakilishi. Sisi tuko radhi lakini leo magari ya ghali, uwezo hatuna. Maana kwamba haijatimia bajeti kwamba serikali bado haipo vizuri kibajeti haijaweza kukamilisha hili, sasa haya magari yametumika vipi, haya mabilioni ya fedha. Mimi nataka uje unambie gari zenu za Mawaziri bilioni ngapi mmetumia kununua gari mje mnijibu, halafu tuangalie katika suala hili la madawa ya kulevya kwa nini wameshindwa kufanywa wakati pia wanasaidiwa kwenye suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMT na SMZ. Mhe. Naibu Spika, wizara husika lazima ikae na Serikali ya Tanzania sisi tupo kwenye Muungano tunaupenda muungano, lakini zile *consulate embassy* zote zipo Dar Es Salaam, kwa nini msende mkaomba *consulate* zikaletwa Zanzibar. Leo unakuta *consulate* ziko Kigoma hazipo hata mji Mkuu wa Dodoma. Kuna Balozi ndogo zipo Kigoma kwa nini zisiwe Zanzibar. Kama tunapendana kweli sisi tunapenda muungano, tunaipenda Tanzania na kama na wao wanatupenda Balozi ndogo ziletwe Zanzibar ziwepo, Balozi kubwa zibakie Dar-es-Salaam. Hapa kuna Rais wawili, tuna Serikali ya Mapinduzi yenye kuheshimika, bila ya

Serikali ya Mapinduzi, Tanzania isingekuwepo na Chama cha Mapinduzi kingekuwepo. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, leo tunakaa tu *consulate* iko Kigoma wakati Zanzibar tuna serikali kamili hapa, tuna nchi yetu hii, tuna viongozi wamekamilika lakini cha ajabu ndiyo hicho.

Jambo jengine kuna balozi zimewekwa huko vichochoroni, *Consulate of Finland* sijui *Sweden*. Tunaomba sana wizara yako itenge maeneo maalum ya Balozi ndogo sehemu zenye hadhi, leo hadhi ipo kwenye Shirika la Umeme, nyuma kule kuna Balozi ndogo nne.
Mhe. Naibu Spika, suala jengine nakwenda kidogo kidogo kwa kuwa hili suala refu na dakika kidogo. Mheshimiwa kwa kuwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yeye ndiye kiongozi wa Wizara zote na ndiye mtendaji, mshughulikiaji, msimamizi, nakwenda kwenye Wizara ya Ardhi. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alitoa kauli ya kwamba atafuta ardhi za watu Zanzibar nzima wasiojenga na waliojenga *foundation* hatojali nani wala nani atafuta.

Mhe. Naibu Spika, mimi ninachotaka kukizungumza kwamba kauli ile imeteteresha uchumi wa Zanzibar, imeumiza wananchi wote Zanzibar na duniani na wao ndio wanaomiliki. Leo ukisema Zanzibar watu wafutiwe ardhi wengine maskini mmetegemea nini. Mheshimiwa Mzee wetu Karume aligawa viwanja watu wajenge wanyonge na mishahara yao midogo. Hebu nambieni mshahara laki moja na nusu mtu atajenga kwa miaka mingapi, sisi Wawakilishi hatujajenga. Leo Mhe. Waziri anasema kwamba ardhi atazifuta, atazifuta kwa sheria ipi, kwa kipengele kipi, kafyatua tu hajafaya sheria, kajifurahisha kwenye TV anaumiza nchi. Hilo suala haliwezekani. Leo Wazanzibari wanakosha nguruwe huko, siku za baridi wanapigwa na baridi mpaka wanaparalaizi, kuna watu wanafanya kazi nzito, lakini...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakisha dakika 5 malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana, lakini mimi nataka nije nijue kwa nini kauli hii ikatoka na kama Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inathamini wanyonge, Waziri huyu kwa nini katoa kauli hii ya kwamba atafuta ardhi na yeye kama nani akawafutie watu ardhi wakati watu wapo wameshaanza kujenga *foundation* zipo na watu wapo.

Mhe. Naibu Spika, leo serikali inatakiwa ishukuru wananchi wamehamia kwenda Ulaya kwa pesa zao wenyewe kwa sababu ajira ngumu maisha magumu, leo watu wameshahangaika miaka ishirini wamepigwa na barafu sio

kwao, leo huku wanalia, wengine wameumwa kwa kusikia taarifa yake yeye. Mimi namuomba Mhe. Waziri kwanza aombe radhi kwa suala hilo halafu vile vile afute kauli yake kabisa. Sisi Wazanzibari tunapendana na hilo suala likijalikifanyika akija akafutiwa mtu ardhi hakutolalika humu ndani, nazungumza dhahiri. (*Makofi*)

Mimi nazungumza dhahiri suala hili likifanyika kwa wananchi wanyonge....

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nimuombe tu Mhe. Mjumbe, kwenye Kanuni ya 59 suala la ardhi sio mjadala wake sasa, aelekeze kwenye hoja husika. (*Makofi*).

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, lakini cha kusikitisha kwamba hapa inayozungumzwa ni Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye ndiye Kiongozi wa Wizara zote. Mimi namshangaa sana Mheshimiwa Mwakilishi wa Jimbo la Paje, kwamba anazungumza mambo yaliyokuwa ya utumbo, ushanifahamu. (*Kicheko*/*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir malizia, malizia. Mheshimiwa nenda kwenye hoja yako, malizia, nenda kwenye hoja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, haya mambo *nonsense....(Kicheko/Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir kaa kitako.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Aah**!** Mimi sijasema kitu.

Mhe. Naibu Spika: Endelea na hoja yako, malizia**.**

(Hapa Waheshimiwa Wajumbe walikuwa wakizungumza na kufanya ukumbi kuwa na zogo)

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi naomba dakika zangu nimalizie, subirini mbona hivi! Naomba dakika nimalizie, sisikii mimi kuna zogo.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa! Waheshimiwa! Waheshimiwa naomba tumuachie Mhe. Nadir amalize.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, mimi nimezungumza mapema na inaonekana kwamba yeye kishapewa *offer* zake hazifutwi, ndio maana anaingilia ingilia mambo ya watu, tafadhali asiniingilie ninapochangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nina haki na mimi nimeshazungumza na litakalokuwa na liwe, hilo suala kalifanya na lipo.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa nimekwambia usijibu endelea.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, suala la Watu wenye Ulemavu ukiangalia kwenye changamoto halikadhalika hili suala halipo kabisa, bajeti ndogo vifaa hawana tunategemea nini watu wenye ulemavu hatuwasaidii. Mbona sisi tunajipa kila kitu watu wenye ulemavu tumewatupa. Hichi kwa kweli kinasikitisha.

Mhe. Naibu Spika, nimekuomba mapema kwamba dakika kidogo, watu wamepiga makelele dakika tatu na dakika tatu, zangu hutaki kunipa hata sifahamu, dakika tatu nzima wamepoteza Wawakilishi na Mawaziri humu ndani kwa kelele. Mimi ningeomba dakika zangu uniongezee Mheshimiwa, hata sijui nichangie nini sasa hivi. (*Vicheko*)

Mhe. Naibu Spika, mimi sasa hivi nitakwenda kwenye Ofisi ya Rais sasa hivi maana ya Balozi siimalizi ni refu, nangojea kwenye bajeti.

Mhe. Naibu Spika: Una dakika mbili tu za kumalizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye Idara ya Mawasiliano ya Ikulu.

Suala alilolifanya Mhe. Rais ni zuri, mambo yanaonekana lakini bado utangazaji haupo vizuri, watu hawajaelimishwa, watu hawafahamu hasa Mhe. Rais Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inafanya nini. Mhe. Naibu Spika, leo kwenye masuala ya matusi anayotukanwa Rais watu wote wanaona, lakini kwenye masuala anayofanya vitu vya maana havionekani sana, kwenye makompyuta Mhe. Rais anatukanwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatukanwa na hakuna hata hatua moja iliyochukuliwa. Kwa nini zile *website* zisifungwe na watu wasikamatwe? Hatujapewa taarifa mpaka leo, Mhe. Naibu

Spika, Waziri wa Habari hajatupa taarifa, tunaomba mnaohusika nyote haya masuala muyasimamie.(*Makofi*).

Jengine nakwenda hivyo hivyo kwa kuripua ripua kwa sababu dakika hakuna, Idara ya Usalama Ikulu tunaona changamoto zake kwamba nayo inasikitika. Kama Idara hii ya Usalama hatujawawezesha hatujawapa vitu wanavyotaka nchi hii itakuwa na usalama, wanajitahidi kwa mujibu wa uwezo lakini hapa inaonekana kwamba wamelalamika au wameona hao watendaji waliokwenda kwamba hali ni mbovu. Naomba sana kwa watu wa Usalama wa Taifa, usalama uliokuwepo wa nchi waimarishiwe na wao bajeti yao ili mambo yaende vizuri ya nchi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na wale wote niliowambia nafikiri wamefahamu, hotuba hii naiunga mkono asilimia 80, nangojea nije nijibiwe masuala yangu magari ya Mawaziri, kauli ya Mhe. Waziri aliyotoa nije nijibiwe na nyengine zote nilizouliza.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mohammedraza Hasanaali Mohamedali, akimaliza atafuata Mhe. Masoud Abrahman Masound.

Mhe. Mohammedraza Hasanaali Mohamedali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii, sote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutupa pumzi ambao tuliokuwepo hapa.

Mhe. Naibu Spika, niichukue nafasi hii kumpongeza Waziri muhusika pamoja na Kamati hii iliyotuletea taarifa ambayo imetupa hekma busara na usikivu. Kwanza tukubaliane sote kwamba Serikali ya CCM inayoongozwa na Rais Dkt. Ali Mohamed Shein Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Rais wa Zanzibar. Serikali ya CCM tokea Mapinduzi imefanya mambo mengi ya sana elimu, barabara na mambo mengi na kupiga vita mambo yote ambayo yanakwenda kinyume na maadili ya Wazanzibari na Watanzania.

Mhe. Naibu Spika, mimi niombe tu Wizara inayohusika pamoja na Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya niipongeze. Lakini vile vile niombe tu Ofisi hii kubwa ambayo inasimamia pamoja na hii Kamati hizi ahadi za Viongozi wa Kitaifa. Kama tunavyojua serikali imeshafanya mambo mengi, changamoto zipo tunatakiwa sote tushirikiane kwa pamoja kuziondosha changamoto hizi ili tuweze kufanikiwa kutekeleza ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi. Mimi

nimesimama hapa kwa niaba ya Chama changu cha Mapinduzi kwa jimbo langu la Uzini na nimesimama hapa kwa niaba ya Chama. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa miaka mingi niliyokuwa nimekuwepo hapa kwa uzoefu wangu nilikuwa nakumbushia tu Wizara zinazohusika kwamba Kamati hii kubwa imezungumza suala la ahadi za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na msaidizi wake Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar mzee wangu Balozi Seif Iddi, hizi ahadi ningeliomba Wizara zinazohusika zingeliweza kutekeleza ahadi. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kuna ahadi nyengine sisi kama Wawakilishi tulikuwa tayari kuzisaidia lakini Wizara zinazohusika kwa bahati nzuri sio kwa nia mbaya waliwezae kutusaidia kwa kusema wao wanaweza kufanikisha.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo mimi nikumbushie tu kwamba huyo Rais wetu wa Zanzibar kwa muda huu anateremka kilima, hapandi kilima. Hivyo ninachoomba zile ahadi ambazo alizozitoa pamoja na Makamu wake wa Pili wa Rais. Mimi ahadi kwa upande wangu wa jimbo la Uzini kwa Mhe. Rais ni mbili. Moja ni kituo cha Afya cha Umbuji na moja Skuli ya Pagali ya kuweza kuezeka. Kwa hivyo ili niombe wahusika najua kutokana na uchumi wetu na kutokana na hali ya bajeti lakini naomba ni vizuri kabla ya Rais huyu kuteremka kilima kumaliza ahadi hizi zingeliweza kutekelezwa katika hii ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi, ili Mhe. Rais kwa hekma zake, busara, mpenda wananchi wote bila ya kujali rangi, kabila na Dini zikaweza kumalizwa. Lakini vile vile nigusie kwa upande wa pili kama alivyoahidi Mhe, Naibu Spika, kwa upande wa barabara za Uzini kuanzia Matola, Pagali, Ndondongwe na sehemu nyengine nilitakiwa kutoa michango ya kuweza kusaidia kama ninavyosema Serikali hahe hoi, inachopata ndio inachotumia. Sisi wafanyabiashara tutapoweza kulipa kodi zetu tutapoweza kuchangia Serikali, Serikali ndio itaweza kurejesha fedha zile au maendeleo yale katika jimbo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nikumbushie tu kwamba ni mwaka wa nne Kiongozi Mkuu wa Baraza la Wawakilishi, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais pamoja na Mawaziri wenzake ilitolewa ahadi hapa kutekelezwa barabara hizi ambazo tuko kwa makubaliano ya Jimbo la Uzini, basi ningeliomba kwa hekma, busara na usikivu wa Mawaziri wakaweka kipa umbele katika kipindi hiki katika utekelezaji mzima wa Ilani ya Chama lakini na ahadi (*commitment).* Kwa hivyo niombe tu kwa heshima zote Wizara inyohusika ni wizara kubwa Ofisi ya Rais basi iweze kukamilisha na sehemu nyengine. Kwa hivyo hayo ni maeneo ambayo nimeona niyagusie kwa sababu ni Kamati kubwa inayosimamia Viongozi Wakuu, sisi ndio wajibu wetu, mimi nimekuja hapa

kwa niaba ya wananchi, hivyo tuwe tunatekeleza vitu ambavyo tuvipe kipa umbele.

Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, tutakuja tena hapa mimi nitapiga buti puu! haiendi, tutapiga kura tutajigawa, kwa hivyo naona haisaidii kwa sababu sasa hivi tuko wenyewe kwa wenyewe ni Serikali ya CCM. Kwa hivyo ule ukasumba waliokuwa nao lakini tuko wenyewe humu ndani. Mimi naona sioni sababu, uwezo tunao, nia tunayo na tutekeleze kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala la pili la hii Tume ya Uchaguzi. Mimi niisemee tu Wizara inayohusika hii Tume ya Uchaguzi ikafanya utaratibu mzima wakati tunapokwenda kwenye uchaguzi wa mwaka 2020. Najua Mhe. Naibu Spika, hii mikutano yetu miwili kama inakuwa mikubwa, iwe siku maalum Chama fulani kimepata kufanya mkutano. Kwa hivyo kama Chama kinafanya mkutano Makunduchi, *obvious* watu wa Nungwi, watu wa Kiwengwa wote wataelekea Makunduchi. Lakini tukifanya mikutano kwa siku moja vyama viwili vikubwa, Makunduchi ikawa na wanachama, Nungwi kuna na wanachama mikutano, Mheshimiwa kuna hali dalili ya mvua mawingu kama amani kupotea kwa sababu kila mmoja ataona kwamba si wakamilifu. Unajua Mhe. Naibu Spika, si kila anayepepesuka mlevi, lakini inaweza kuwa gari ikajazwa mawe, matokeo yake ile amani ikapotea na sisi tunaona tunathamini sana wananchi wetu wasipatwe na nini.

Kwa hivyo, niishauri Tume ya Uchaguzi ambayo imeguswa ikatizama katika kampeni mkutano uwe mmoja, wa pili uwe siku ya pili ili amani yetu tuendelee kuwa nayo ili sote tuendelee kupendana, kwa sababu mtu wa Nungwi lazima atakwenda Makunduchi. Na hiyo siku itayokuwa mkutano Nungwi kwa Chama chengine, yule wa Makunduchi lazima atakwenda Nungwi. Hivyo hapa kuna njiani ile magharibi kumeingia kiza. Kwa hivyo nitoe tu maoni yangu kwamba hii Tume waipokee kwa nia nzuri katika jambo lote hili ambalo litaweza kutusaidia alhamdulillahi maisha na Wazanzibari.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, nije kwenye haya madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni janga kubwa sana ni janga ambalo dunia nzima imekabiliana nalo. Mhe. Naibu Spika, ni vizuri hata viongozi wa Dini mbali mbali wakawa wanahamasisha pamoja na sisi wenyewe tunahamasisha katika kulizungumza sana hili. Kwa sababu hili janga sio Kur-an wala si Biblia inayoruhusu na hili janga ambalo ni zito sana katika taifa letu hasa kwa upande wa Zanzibar. Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Zanzibar ninachosema kwa sababu tumezungukwa na bahari, tungelikuwa Serikali yetu ni hii

tuliyokuwa nayo na ukisema Zanzibar visiwa lazima tuwe na boti za kisasa. Kwa sababu mimi ninaamini wapiganaji, wasomi, watu wenye uwezo, Usalama wa Taifa, Jeshi la Wananchi, Polisi, JKU, Mafunzo, KMKM wana hekma na wana uwezo. Wazanzibari tunajuana Mhe. Naibu Spika, tuko kidogo lakini mimi ninaamini zana za kufanyia kazi na hii yote itatokana na bajeti. Kwa hivyo ni vizuri tukatafuta msaada kwa wenzetu wa kuweza kutusaidia katika vita hivi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakiri kwamba hivi vitu tusipotizama vinaweza kutuathiri kwa sababu mimi mwenyewe pale *ZAT*, kama Mwenyekiti wa *ZAT* ipo *record* Serikalini, walikamatwa wafanyabiashara na madawa ya kulevya zipo ripoti yamekamtwa yameingizwa, siku ya pili yameondoshwa na wale wakakimbizwa nchini. Sasa Mhe. Naibu Spika, na hili naona alitizame kwa sababu *record* zipo pale *airport*. Hili jambo lazima tuwe makini sote na mashirikiano ya pamoja.

Mhe. Naibu Spika, hili si suala la Serikali, hili si suala la vikosi ni suala letu sisi pamoja. Lakini mimi imani yangu kwamba wenzetu baadhi ya Mawaziri kutembea kwenye *Sober House* na kuingiza bajeti za kuzijenga hizi *Sober House*. Mhe. Naibu Spika, mimi naona kwamba tuna-*encourage something*, tunaingia kwenye *Sober House* kuwatakia pole. Kwa hivyo mimi ninafikiri imefika wakati tukakamate papa ili tuone janga hili linaweza kuondoka, hili janga letu sisi sote, ni janga ambalo linataka hekma na mimi ninaamini Mhe. Naibu Spika, kutokana na kisiwa chetu cha Zanzibar sote tunajuana.

Mhe. Naibu Spika, lakini vile vile visiwa hivi viko mbali na kubwa ni zana za kufanyia kazi. Kwa hivyo tuwaombe Serikali yetu ya Muungano kwa sababu Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje watufidie tuone ni jinsi gani wanaweza kuchangia kwa sababu ile Wizara ni kubwa. *Obvious* tunaziona Wizara ya Ulinzi, Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje zinapata misaada mingi sana kwa kutumia jina la Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, hilo imefika wakati, *we have to sit*, tuna tatizo. Kwa hivyo mimi naamini kama Wizara hizi zitashirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, tunaweza na uwezo tunao. Mhe. Naibu Spika, mwaka 1979 Hayati Mwalimu Nyerere alisema uwezo tunao, nia tunayo na tutamuondosha nduli Iddi Amin. Ile alimainisha kwamba Serikali zote mbili na tuliweza kufanikisha na nguvu zetu za wananchi, wapiganaji walikwenda mbele ya haki lakini Tanzania ikaendelea kuwa na amani na Zanzibar ikashiriki kikamilifu, tena kwa vitu vingi sana na tukapoteza

wanajeshi wetu. Lakini kwa sababu ya muungano wetu wa udugu wetu tukaweza tukafanikisha. Kwa hivyo Hayati Mwalimu alivyozungumza vile alizungumza kwa Serikali mbili na aliona kwamba Wazanzibari na Watanzania wameliunga mkono.

Kwa hivyo mimi nitoe wito kwa ndugu zetu hasa kwa mpendwa wetu Rais wa Jamhuri ya Muungano na Mwenyekiti wa Chama, Mzee wangu Mzee Joseph Pombe Magufuli pamoja na Rais wa Zanzibar wakae pamoja na Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais. Mimi ninaamini Zanzibar ni ndogo tukipata vifaa au waturuhusu sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, Wizara ya Ulinzi tukachukue *part* yetu tukaombe uwezo huo upo Mhe. Naibu Spika, kwa Zanzibar. *We can, I can assure*, tutapata bomu wapo majirani zetu ndugu zetu nchi za *gulf*, Marekani, Ufaransa, Oman Abu Dhabi tunao tutakwenda kuwaambia kwamba bwana hili janga ni kubwa kwa watoto wetu, kwa wajukuu zetu. Kwa hivyo lazima tu-*determine* kwa sababu Mheshimiwa muungano huu ni wa nchi mbili huru, hakuna Rais mkubwa wala mdogo. Kwa hivyo naona kwamba katika misaada mingi inayokuja tunaijua, lakini lazima wafike pahala ile Zanzibar ionekane katika mazingira. Kwa sababu Mheshimiwa hali ya umaskini, leo unamwambia kuna tukio la wizi tu umetokea kwa mfano umetokea wizi sehemu fulani, hawa ndugu zetu wa Polisi ni wazuri kwa Mungu na wana uwezo. Lakini mafuta hamna ni hali kwa sababu ya bajeti, inabidi utumie gari yako. Kwa hivyo uhalifu mwingi Mhe. Naibu Spika unatokana si kwa watu wetu wazembe, si kama watu wetu hawana uwezo, si kama Wazanzibari hawafahamu lakini zana za kufanyia kazi.

Mhe. Naibu Spika: Muda wako umekwisha.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Naam**!** Umekwisha?

Mhe. Naibu Spika: Eeeh!

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Basi Mhe. Naibu Spika, naomba nikae kitako niunge mkono kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Uzini naunga mkono asilimia mia moja na moja. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa anayefuata Mhe. Masoud Abrahman Masound baadae atachangia Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia Ripoti ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niwapongeze Kamati kwa kuandaa taarifa nzuri ambao sote tuliosikiliza na wale waliokuwa wanaangalia vyombo vya habari huko na taarifa yetu moja kwa moja inasikika ni taarifa nzuri na ya kupendeza sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze moja kwa moja na Idara ya Kukabiliana na Maafa. Sasa hivi viongozi wote wa Zanzibar inapofikia kuanzia mwezi wa tatu na mwezi wa nne tunakuwa na wasi wasi wa kunyesha kwa mvua kubwa za Masika. Mvua kubwa za Masika zinaponyesha viongozi wote wa Serikali tunakuwa na wasi wasi kwa sababu tuna uhakika kuwa mvua ikianza kunyesha kubwa baadhi ya meneo yatapata mafuriko na yakipata mafuriko janga hilo linakuwa ni la Serikali na linaanza kwenye viongozi, sisi tuliomo ndani Waheshimiwa Wawakilishi, Halmashauri na Shehia pamoja na watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa jana na mwaka juzi Serikali kwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ilifanya kazi kubwa ya kuhakikisha zile familia ambazo zilipata matatizo waliweza kuzisaidia kwa kushirikiana na viongozi wa majimbo na viongozi wengine ambao walitoa misaada yao. Mhe. Naibu Spika, lakini hili litakuwa linaendelea kila mwaka. Kamati imetoa ushauri lakini niombe sana na mimi kwa mchango wangu, niombe sana mimi jana niliitwa kwenye eneo langu la Shehia ya Bububu, kuna eneo linaitwa Kisimamajongoo. Eneo hilo kila mwaka huwa linajaa maji na kuna nyumba nyingi sana eneo hilo. Niiombe Serikali kabla ya mvua za Masika kunyesha, yale maeneo ambayo yako hatarishi basi twende tukayaangalie mapema ili kama kuna uwezekano yapate kufanyiwa marekebisho kwa kutumia vyombo mbali mbali vya kitaalamu ambavyo vinaweza vikatushauri maji yale yanaweza yakatoka kwenda maeneo mengine yoyote.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye miradi ya Mfuko wa Jamii wa *TASAF*. Kwanza niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kazi kubwa ambayo inayofanya ya kuwasaidia wananchi wake ambao wana kipato cha chini. Lakini niseme miradi hii baadhi huona kuwa ni miradi ya kilimo, hii ya kuwasaidia wazee, wanasaidia vikundi mbali mbali. Lakini kuna baadhi ya maeneo wanaposaidia kwa nia nzuri tu Serikali inatoa lakini kile ambacho kinalengwa kufikia mwananchi hawa wataalamu hapa juu wanakuwa wanakichukua.

Mhe. Naibu Spika, mfano kama unatakiwa usaidiwe mradi wa ufugaji kuku. Suala la mwanzo linaloanza ni kujenga banda. Kwa hivyo lile banda ambalo unategemea kujenga wataalamu wanakwenda wao kununua miti hatua ya

kwanza. Lakini hatua ya pili zile kamba za kujengea ende mtaalamu akanunue. Lakini hatua ya tatu yale mafunzo ambayo wanayatoa kwa wale ambao watakabidhiwa wale kuku au kitu chengine, mafunzo wanayatoa pengine siku tatu au siku nne ya ufugaji. Mhe. Naibu Spika, zile fedha ambazo zilikuwa apewe yule mlengwa kama ilikuwa shilingi elfu kumi basi inamfika elfu mbili. Na lengo la Serikali imfike ile pesa ikiwa nyingi ili apate kujiendeleza, hatma yake unakabidhiwa kuku 20 na unaambiwa dawa ujitegemee wewe mwenyewe. Mhe. Naibu Spika, wananchi wetu kwa kweli uwezo wao ni mdogo na tunahitaji tuwasaidie na kile tunachowasaidia ili kiweze kuwasogeza mbele.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ambalo nilitaka nilizungumze ni suala zima la Wakala wa Upigaji Chapa. Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na kilio cha muda mrefu lakini Serikali baada ya kutengeneza bajeti zake tulifanikiwa kununua vifaa vya kisasa. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna tatizo ambalo bado linaonekana mpaka leo la kusuasua ile *speed* ya kufanya kazi bado ni ndogo sana. Kwa hivyo Kamati yetu ilipokwenda kuna vitu wamevigundua pamoja inaonekana pesa zao za *overtime* inakuwa kidogo ni tatizo kuzipata, lakini pia kuna watu wana malimbikizo ya madeni. Niiombe Serikali iweze kuwalipa pesa zao za *overtime* ili wafanye kazi vizuri lakini pia na wale ambao wanadai pesa pengine za likizo, basi wapewe mapema ili wafanye kazi kwa nguvu zaidi na kupata moyo wa kufanya kazi kwa ujasiri.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye sherehe na maadhimisho ya kitaifa. Hapa kidogo pana masikitiko. Baadhi ya Waheshimiwa maana yake sio sote, baadhi ya Waheshimiwa tunaondoka kwa mikazo tunakwenda kwenye uwanja wa Amaan. Mimi mwenyewe yalinifika nilitoka siku hiyo Dkt. Ali Mohamed Shein ndio mgeni kwenye fainali ya Kombe la Mapinduzi, mimi bahati nzuri mechi zile tokea zinaanza na wenzangu wapo akina Mhe. Abdalla Diwani tulishiriki mwanzo mpaka mwisho.

Mhe. Naibu Spika, lakini siku ya mwisho kwa sababu kulikuwa kuna tiketi ambazo zilikuwa zinatolewa bure kwa viongozi wakuu na viongozi wale wa kitaifa baadhi yao, basi lile eneo ambalo anakaa Mhe. Rais pamoja na viongozi wakuu, Mhe. Waziri wa Habari mwenyewe alikosa nafasi ya kukaa, mpaka akaonewa huruma na Waheshimiwa Wawakilishi waliona nafasi zao ndogo waache wampishe yeye Mhe. Waziri.(*Makofi*).

Kwa hivyo niiomba tu na unaowaona wamekaa pale labda itakuwa ni wafanyabiashara au vijana tu kapewa tiketi na baba yake au na mama yake au mtu yeyote aliyekuwa yuko juu katika Kamati hizi ambazo za maadhimisho. Kwa kweli linasikitisha na viongozi wakubwa wanasikitika sana kuona ile

hadhi yao kama Mhe. Mwakilishi au Mbunge anakaa pembeni anaambiwa akae kwenye jukwaa la “e” wakati sehemu ile ya *VIP* walizopangiwa hawapati nafasi za kukaa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuna hili la Tume ya Uchaguzi. Mimi kwanza niipongeze Tume ya Uchaguzi kwa kazi yake nzuri ambayo inafanya, lakini Mheshimiwa hapa kuna tatizo la wafanyakazi. Wafanyakazi wapo wengi ambao hawajaajiriwa mpaka leo. Lakini pia hao walioajiriwa maslahi yao hawapati ipasavyo. Hivyo niiombe Serikali au waliokuwa hawajaajiriwa waajiriwe, pale patakapopatikna bajeti yao lakini pia na yale maslahi ya wafanyakazi nao wapatiwe ili wafanye kazi kwa ufasaha zaidi.

Mhe. Naibu Spika, suala la madawa ya kulevya wenzetu Tanzania Bara sasa hivi ndio kila siku tunasikia linazungumzwa kwenye vyombo vya habari. Lakini na hapa kwetu Zanzibar lipo kama walivyothibitisha wenzangu na tunaliona. Lakini Mhe. Naibu Spika, dawa hizi siwezi kusema kuwa zinapita kwenye Uwanja wa Ndege wala Bandarini kwa sababu Zanzibar maeneo mengi yana bandari bubu. Kwa hivyo niiombe Serikali ifanye kazi ya ziada kuhakikisha madawa ya kulevya hayaingizwi Zanzibar. Kwa sababu sasa hivi vijana wetu ambao ndio nguvu kazi na viongozi wetu wa kesho tunaowategemea, ukiwaangalia huko mitaani kwa kweli hali sio nzuri, inasikitisha na kwa Serikali tuseme ni aibu. Kwa sababu kuna vikosi maalum ambavyo vinapatiwa fedha, kuna walinzi wetu wanapatiwa mishahara lakini bado kazi haifanyiki vizuri.(*Makofi*).

Niiombe Serikali iongeze bidii sana kwa sababu hapa vijana wetu na watu wazima bado tunapata tatizo kubwa. Hapa wenzangu walisema kuna ma-*sober house* mengi yanajengwa sasa hivi. Lakini mimi Mhe. Naibu Spika, napata wasi wasi kuwa hizi dawa za kulevya hata huko *sober house* zinapelekwa na hao wauza unga, kwa sababu kule tayari wameshakusanywa wote wako pamoja wavuta unga, kwa hivyo wanapelekewa pale inakuwa rahisi kwenda kuuza. Kwa hivyo niombe sana serikali ma-*sober house* tuendelee kuwa nayo lakini na elimu tuzidi kutoa na hasa kwenye Shehia.

Mhe. Naibu Spika, maana yake sasa hivi, juzi moja nilikaa pahali na vijana, mara kapita kijana mmoja kavaa kanzu kajivisha na kilemba na vespa, akanambia kijana yule sasa hivi anakwenda kuuza unga Ndagaa, sasa kwa lile vazi la heshima ambalo kavaa huwezi kufikiria kwamba anakwenda kuuza unga. Lakini kwa sababu labda ulinzi hauko vizuri na yeye anatumia nafasi ile ile. Niombe askari wetu wa ulinzi na usalama wafanye kazi ili tuondoe hili janga ambalo limetukabili hapa Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwenye ahadi za viongozi, mimi nilikuwa Diwani vipindi vitatu katika Jimbo la Dole. Mhe. Rais alikuja kwenye jengo la Hospitali ya Mbuzini ambalo tulisimamia Halmashauri ya Wilaya ya Magharibi kwa wakati huo, na akaahidi kuwa hospitali ile itajengwa na itakuwa hospitali ya Wilaya. Nimuombe Waziri wa Afya niiombe Serikali, Mbuznii sasa hivi kumekuwa nusu ya mji ijengwe hospitali ile ili tukamilishe ahadi ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti kwenye suala la maafa kuna kitu nilikisahau. Mhe. Mwenyekiti kwenye eneo langu la Kizimbani kuanzia mwaka niliokuwa sijazaliwa sitini kwendea mbele Serikali iliamua kuweka Kituo cha Utafiti katika eneo lile, lakini wale walioajiriwa kwa wakati ule walikuwa ni watu wa maeneo mbali mbali waliamua kuja kuhamia Kizimbani, na Kizimbani lote nusu na robo ni eneo la utafiti lakini walipohamia walijenga nyumba zao kwa wakati ule hawakuhamishwa au hawakuzuiwa kujenga walijenga katika maeneo hayo ya utafiti.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, wakati huo kulikuwa na minazi ilikuwa midogo lakini sasa hivi minazi ile imekuwa mikubwa kwenye maeneo yote yale ya Kizimbani na kwa wakati huu ulikuwa watu walijenga vijumba vyao vya udongo, lakini sasa hivi wameshajenga nyumba zao kubwa na za kudumu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sababu ya kusema maafa kila inapotokezea upepo kila baada ya miezi mitatu, kila baada ya miezi sita, kila baada ya mwaka tunapata kesi za nyumba zimepigwa na minazi kule ni kesi kubwa na wengine wanapata ajali mpaka wanalazwa hospitali. Kwa hivyo niiombe serikali Waziri wa Kilimo, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo kwa wakati huo aliwachukua wananchi wa Kizimbani akawapeleka Mahkamani mpaka leo kesi zipo kwa sababu wameamua kuukata mnazi uliopo eneo hilo la utafiti.

Mhe. Mwenyekiti hili ni tatizo na nimuombe Waziri wa Kilimo kwa kupitia maelezo haya ambayo nayatoa sasa hivi twende Kizimbani tukaiangalia hiyo hali, kwa kweli tutakuja kupata msiba mkubwa na Serikali kwa wakati huo Serikali kwa kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa imeshatoa misaada mingi kwa waathirika ambao nyumba zao zinapigwa na minazi. Kwa hivyo, tusisubiri tukaja tukapata watu ambao watapigwa majumba yao na minazi wakatoka roho hatma yake tukaja tukatoka hapa kama Serikali kwenda kutoa mkono wa pole kwa wananchi, bora tuzibe ufa kuliko kujenga ukuta. Niiombe Serikali kwa zile nyumba zote ambazo labda kuna minazi iliyokuwa imeshakuwa mirefu na imeshakuwa mibovu itoe ruhusa minazi ile ikatwe ili kuwahami wananchi wetu, hawa ni wapiga kura wetu ni wananchi wetu ambao wanaishi katika jimbo langu hawana matatizo ya aina yeyote.

Mwisho ...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Masoud malizia dakika moja.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Mwisho niombe tu Mhe. Mwenyekiti, kuhusu suala la Tume ya Ukimwi Zanzibar.

Tume ya Ukimwi Zanzibar inafanya kazi nzuri na ya kupongezwa lakini Mhe. Mwenyekiti, sisi tulitakiwa tuzibe ufa tusisubiri kujenga ukuta. Vile vile viashirio vya kupata maradhi ya Ukimwi sisi kama viongozi au serikali inaonekana kidogo tunaiachia. Kwa sababu sasa hivi kwenye Shehia nyingi wanalalamika kupitia madisko ambayo yanapigwa kila siku kwenye Shehia zetu na ukilalamika sana unaambiwa..., kwa sababu madisko haya yanapigwa zaidi kwenye mabaa na mabaa yaliyo katika mitaa ukisema unaambiwa uende Mahkamani, ukienda Mahkamani kesi siku zote wanashinda wenye mabaa hawashindi wale wananchi ambao wanakwenda kuyapinga *(Makofi)*

Kwa hiyo niiombe Serikali kwenye hili ili kupunguza maambukizo wa virusi vya Ukimwi baadhi ya maeneo tusikubali kupiga madisko ya kila siku.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika: Mhe. muda wako umekwisha

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika nakushukuru kwa kunipa nafasi naomba kuwasilisha.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. mchangiaji anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuata Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baadae Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa fursa hii ili na mimi kuchangia machache kwenye ripoti hii ya Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende moja kwa moja kwenye michango kwa kuwa walioleta nafasi ya michango ni wengi nianze na kuwapongeza Kamati kwa kazi ngumu ambayo walioifanya kupitia katika Wizara mbali mbali na kuona kwamba kuna changamoto ambazo zinahitaji kutekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze na Tume ya Madawa ya Kulevya. Mhe. Naibu Spika katika ripoti yao ya Kamati tumeona kwamba kuna ufinyu ya bajeti. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Tume ya Madawa ya Kulevya ni muhimu hapa kwetu Zanzibar na mimi napendekeza kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kupitia bajeti ijao mwaka 2017/2018 iwape kipa umbele iwazongee bajeti.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na hali halisi ambayo inaonesha kwamba madawa ya kulevya yamekithiri hapa Zanzibar, lakini kwenye ripoti yao ya Kamati nilivyoisoma kumekuwa na taarifa ya kwamba kutomalizika kwa kesi ambazo za waliokamatwa kwa wafanya biashara ya madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, kumeonesha kwamba kuna taarifa ambayo wanasema kwamba kuna kuibiwa kwa vielelezi ambavyo vya hawa washitakiwa, nilitaka kujua kwamba hivi vielelezo vilivyoibiwa, vimemeibiwa Mahkamani au Polisi. Mheshimiwa pia kukaa kwa muda mrefu wa kesi hizi ambazo zinakuwa kwamba hazimaliziki kwa wakati. Mhe. Naibu Spika, nimeona kwamba kuna mapungufu ya sheria ambayo inasimamia hii Tume ya Madawa ya Kulevya. Kwa hivyo ningependa kwamba yatizamwe mapungufu haya na pia yafanyiwe marekebisho. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Tume ya Ukimwi. Mhe. Naibu Spika tunaona kwamba Zanzibar bado maambukizo mapya ya Ukimwi yanazidi kuongezeka, lakini pia Kamati imeona kwamba yapo maeneo ambayo yanafanywa biashara za ngono. Mhe. Naibu Spika, kweli ni maeneo hayo yapo hata katika Jimbo langu la Kiwengwa katika maeneo ya Kiwengwa pia yapo na maeneo haya yanasababishwa na ongezeko la mabaa. Mhe. Naibu Spika, maeneo mengi ya mabaa yanasabishwa na biashara ya uuzaji wa ngono.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kumekuweko kwa unyanyapaa kwa waathirika hawa wa VVU. Mhe. Naibu Spika, tuone kwamba suala ya unyanyapaa linasababisha ongezeko kubwa la VVU kwani kwamba mtu anaponyanyapaliwa anaweza akatoka akaenda kuambukiza na wengine na maongezeko yanakuwa makubwa.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamiii yaani TASAF. Kama walivyotangulia kusema wenzangu Mhe. Naibu Spika, Mhe. Rais wetu wa Zanzibar alikuwa na nia safi ya kuhakikisha kwamba kaya maskini basi zinapatiwa fursa ili kuwezeshwa kwa ajili ya kuwa na maendeleo mazuri kama wengine.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, cha kushangaza kwamba kuna changamoto kubwa ambapo waliofikiwa na mfuko huu wengi zaidi ni watu ambao wanajiweza, na wale

ambao kaya zao ziko maskini wameweza kuachwa kutokana tu na kwamba huyu mtoto wa Sheha, huyo mke wa Sheha na kuacha wale ambao wanaathirika zaidi katika kaya maskini. Mhe Naibu Spika, naomba sana kwamba miradi hii au mradi huu wa TASAF ambao unaosaidia kaya maskini basi uchunguzwe kwa kina pesa zile, yaani matumizi na kufuatilia wale walengwa ambao wanaopatiwa fedha hizi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa Idara ya Watu wenye ulemavu. Mhe. Naibu Spika, tunafahamu kwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais inasimamia Idara ya Watu wenye ulemavu. Mhe. Naibu Spika, kuna malalamiko kwamba watu wenye ulemavu wana kosa fursa ya kupata mikopo katika Taasisi mbali mbali ambazo zinaweza kutoa mikopo kwani kwamba wanaambiwa kwamba mikopo wao hawaruhusiwi kupewa mikopo katika taasisi hizo, kwani mikopo yao ipo katika Wizara hiyo Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Nilitaka kujua kwamba watu hawa wenye ulemavu hii fursa ipo na kama ipo basi wapewe mikopo nafuu ili na wao waweze kujitoa katika hali ya umaskini, kwani kuna walemavu ambao wanaweza kufanya shughuli zao kama kawaida na kuna walemavu ambao wengine hawawezi kufanya shughuli zao.

Mhe. Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii *(Makafi).*

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa mchangiaji anayefuatwa na Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baada ya hapo atafuata Mhe. Simai Mohammed Said akifuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kunipa fursa hii kuchangia ripoti Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Niende moja kwa moja katika suala la Idara ya Uratibu wa SMZ na SMT. Nimesema kwamba nisimame hapo kwa sababu hapo ndio panapo matatizo Wazanzibari tunayoyapata, naomba sana Serikali ilinisikilize najua mbele mnazungumza. Nakwenda juu ya suala la *Double Taxation* wananchi wetu wanalalamika baada kupitisha sheria ya *VAT* kwamba ilipwe katika sehemu inayomaliza *destination,* matumizi imekuwa wafanya biashara wanalalamika kulipishwa *VAT* mara mbili, wanalipishwa *VAT* Tanganyika wanalipishwa Zanzibar. Sijui hizi sheria mlizipangapanga vipi mpaka ikawa hatua kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, najua tarehe 13 mlikaa viongozi wakuu kuzungumzia mustakabali mzima wa changamoto au kero za Muungano. Jee, suala hili ufumbuzi wake umefikia vipi. Wafanyabiashara wetu wengi wao wanasikitika

na suala hili, unapokwenda kusema subiri ufumbuzi unapatikana lakini mpaka dakika hii bado na tumebakisha miezi mitano au sita tuingie katika mwaka mpya wa fedha, mwaka wote huu wa 2016/2017 watu wanaumia kiasi hiki. Naiomba sana serikali katika wanaoratibu shughuli hizi basi tutafute ufumbuzi wa watu wetu ili wasilalamike.

La pili juu ya jambo la *temporary transportation,* Wazanzibari tunanyanyasika. Kuna fursa ya kutumia *form* ya *C35* ambayo inatumika katika *borders* zote za *East Africa or SADC,* hii *C35* ambayo inamuwezesha mtu au mwana jumuiya kuingia upande wa pili akiwa na usafiri wake kama gari akatumia kule mpaka siku ambazo anataka kutoka anatoka nayo. (Makofi).

Lakini kwa Zanzibar kwenda na gari Bara imekuwa haramu kulikoni, iweje nafasi ile nitaipata mimi kwa sababu mimi Mwakilishi naweza kuomba nikaandikiwa barua pengine nikenda. Jee, kuna pingamizi gani ambalo linawafanya Wazanzibari wasiwe na fursa wa kutumia *form* ya *C35* ambayo ipo *around the world* katika suala la *temporary transportation.* Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hili suala limekuwa kero la muda mrefu, nyinyi mnajua wa mbele mkitaka kwenda magari yenu yako kule yanakusubirini au pengine mnaondoka nayo. Sisi wanyonge na wapiga kura wetu wanataka kutumia fursa hiyo wanataka kwenda *crater* kule wende Tarangire, wende Mwanza wakaangalie hali halisi ya nchi yao wanasindwa, hiyo ni kero zaidi ya kero.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Muungano mzuri tunaupenda sana lakini hizi zinaitwa kero changamoto naomba sana zifike *time* ziwe hazipo. Mzanzibari anapojisikia kwenda upande wa pili wa Muungano basi aende katika meli ya *Sea Link* alipe gari yake, aende na *documents* pale kama *custom* awasilishe apewe *realize* atoke na gari lake, anaenda Mbeya, Morogoro, Tabora siku zake tano sita anarudi, anarudi anakwenda zake bandarini anakabidhiwa vitu vyake anapakia gari anakuja nayo Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hiyo ndio raha ya Muungano au matunda ya Muungano ambayo sasa hivi Wazanzibari wanayataka, kama magari mazuri Zanzibar yapo au wanayo lakini imekuwa haramu kuyapeleka Tanzania Bara kwa ajili ya kutembea mnatunyanyasa sana katika hicho. Nilitaka kusema hili kwa sababu ni *field* yangu, nimeshafiri nimeshakwenda Kenya, Rwanda, Burundi vitu vyote nawasilisha pale kwenye *border*. Iweje kwa Zanzibar iwe haramu naomba sana Waheshimiwa hili suala linakera na tunaka haraka iwezekanavyo lipatiwe ufumbuzi wake, walizungumza katika suala la uratibu hizi changamoto.

Mhe. Naibu Spika, sasa nakwenda kwenye suala la madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya nafikiri wachangiaji wote waliozungumza wamechangia kweli madawa ya kulevya, madawa ya kulevya ni tatizo nathubutu kutamka ni janga la kitaifa na serikali pengine inaona haya tu ya kusema kwamba tumeshindwa kuratibu hili suala kwa sababu wauzaji wanajulikana au baadhi ya wasafirishaji wanajulikana, hatua gani iliyochukuliwa mpaka dakika hii hakuna. Mhe. Naibu Spika, wao wenyewe Serikali wanashindana kwa kufunga kifaa pale *Airport* tu kwa ajili wanatakapomkamata mtumiaji madawa ya kulevya, akatoe madude yake pale ije ionekane inashindikana mpaka leo, toka siku kile kifaa kilopelekwa *Airport*. Sasa sijui kuna kitu gani hapa. Taasisi zenyewe za kiserikali zinakiukana katika suala zima la kuthibiti au kuratibu madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni kweli janga tukiuliza hapa miongoni mwetu familia zetu wamo ambao watumiaji na tunajua na faida yake inazalisha waathirika wa Ukimwi na wendawazimu.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, wendawazimu wengi sasa hivi wametokana na madawa ya kulevya au hao waathirika wa Ukimwi wengi sana wametokana na madawa ya kulevya na sisi tukikaa hapa tunasema tunayalaani wee! tumeunda Kamati ya Kuratibu na Kudhibiti bado, hayadhibitiwa wala hakujaratibiwa bado madawa ya kulevya yapo na yanaingizwa na watu wanajulikana. Sijui Serikalina ina hofu gani kuwachukulia hatua. Naomba taratibu zipo, sheria zipo zifuatwe basi taratibu ili kuweza kuwadhibiti.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, na alisema mmoja kwamba tushazoea kuiga, waanze wenzetu sisi tufuatie sasa tusione haya katika hicho lakini tutafute njie nzuri au utaratibu mzuri ya kuweza kuyadhibiti madawa ya kulevya ili kuweza kuunda Taifa la Zanzibar lenye wenye vijana wenye akili na walioepukana na maradhi.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala la maadhimisho ya kitaifa itifaki na huku wenzetu wameshazoea kuna udhalilishaji wa watoto. Mimi nazungumzia kwamba kuna udhalilishaji wa Wawakilishi. Wawakilishi mkiondoa nyie mstari wa mbele na nyuma yenu, wa nyuma sote tumekuwa tunadhalilishwa nchi hii, hatuna thamani hata siku moja mtu anajulikana yule Mwakilishi wa Jang'ombe, yule Mwakilishi wa wapi lakini thamani yetu kama Mwakilishi katika watendaji wenu au katika vyombo vyenu mnavyovisimamia hawaheshimu Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, nimezungumza mwanzo narejea tena hapa mwenzangu alisema juu juu tu alitoa mfano kwenye Kombe la Mapinduzi na mimi pia kule yalinikuta, hata niseme hata huyo Waziri wa Nchi Afisi ya Rais alidhalilishwa katika mchezo wa Yanga na Simba, alishindwa kuingia uwanjani mtu kakaa

mlangoni tu alishindwa kumpitisha eti hana tiketi. Yale ni mashindano ya sherehe za Mapinduzi, sasa mashindano na kumdhalilisha kiongozi wa nchi vipi. Yule ni Waziri chini ya Ofisi ya Rais wa Serikali ya Mapinduzi ambayo ni mashindano yake, lakini kutokana kwamba na kudhalilishwa imekuwa kawaida, basi hajulikani huyu nani, huyu nani watu wote wanaonekana sawa sawa. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nawaombeni sana mujaribu kuwa wakali katika watendaji wenu, nilizungumza juzi Afisi Kuu na leo nafasi yake imekuwa hapa, Ofisi ya Makamu ndio wenye jukumu hilo, tunawaombeni sana heshima yetu kama Wawakilishi tunaitaka. Sisi tumetoka majimboni tumegombea na watu kumi na tano, saba, kuna wengine wamepigwa viwembe humu wameshinda Uwakilishi. Sasa iweje ile heshima ya Uwakilishi mtu asiwe nayo, anataka ajitanue kama yeye ni Mwakilishi. Kwa hivyo kafanya kazi kubwa sana kupeperusha bendera ya Chama chake na hatimae kuchaguliwa. Naomba sana Waheshimiwa hilo likae kwenye akili zenu.(*Makofi*).

Hata ukienda katika maofisi yenu baadhi ya Mawaziri basi anathamini Afisa wake kuliko Mwakilishi wa Jimbo. Jamani mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni, sisi ni Wawakilishi kama nyinyi, wenzetu mko mbele kama Mawaziri na Manaibu Waziri, sisi huku nyuma ni Manaibu Waziri wa akiba na Mawaziri wa akiba pia, lolote kwa Mwenyezi Mungu linaweza likatokezea, kesho na keshokutwa pengine Rais akasema fulani hayumo leo akatoka mtu nyuma akaja mbele. Kwa hivyo, ile heshima kidogo tunaomba iwepo kwa Wajumbe wenzenu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nitazungumzia katika suala la uchapaji. Mmesifu kwamba kuna mitambo mipya imeboreshwa lakini cha kusikitisha hadi hii leo lile Gazeti letu la Zanzibar Leo linachapishwa Tanganyika. Mhe. Naibu Spika, tunapoteza pesa nyingi sana kule wakati tuna *Press* pale, mmesifu hapa Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais alisema kwamba kuna mitambo mipya na itakuwa gharamu na hatokubali kuona taasisi yoyote ya serikali inachapisha majalada yake au vitabu vyake nje ya Zanzibar wakati *Press* tunayo, yaani uchapaji

Mhe. Naibu Spika, kulikoni hadi hii leo magazeti ya Zanzibar Leo yanatoka Dar es Salaam, saa tatu unasubiri boti pale ndio linakuja na wametwambia kwamba wana mitambo mizuri na ya kisasa. Kidogo akili yangu hapo haikai vizuri naomba sana Mheshimiwa kulikoni hata iwe kwamba magazeti yale basi yachapishwe Tanganyika na wakati mliratibu mkasema kwamba mnayo mitambo, mnavyo vifaa vya kisasa vya kuchapisha hayo masuala yote. Kama hakuna uwezo wa wafanyakazi basi mngeajiri watu wenye uwezo kuweza

kufanya kazi, kulikoni mpaka leo hii tumefunga mitambo kwa pesa nyingi sana pale lakini baada ya kuchapisha karatasi zetu za Baraza la Wawakilishi na taasisi nyengine tunashindwa kuchapisha magazeti. Kwa hivyo, nitaiomba sana Waheshimiwa viongozi hili suala lichukuliwe kwa hali ya juu sana ili kuweza kutatua matatizo hayo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda katika Idara ya Mawasiliano Ikulu. Mhe. Naibu Spika, tunaona au tunajifunza kwa mazuri, kwa hivyo wenzetu kule Tanganyika kinachotokea baada ya dakika tu tunaona vitu. Mhe. Rais kafanya hivi, sisemi kwamba wakopie hapana, lakini kilichokuwa kizuri kinafaa kuigwa. Mhe. Naibu Spika, zile taarifa za serikali zisiwe siri kupita kiasi mpaka tena mtu usikie baada ya masaa, kwa wenzetu likitokeza tu kushafanyika kitu kule uteuzi, katumbuliwa mtu jibu, kafanya nini tunaona dakika tano tu kitu kimekuja angani. Sasa sijui Zanzibar tunaogopa nini katika kuyafanya hayo na kwa sababu lile jambo ni zuri sana ambalo tunaona kwamba lina manufaa kuwapa habari watu wetu.

Mhe. Naibu Spika, nitarudi nyuma katika suala la Baraza la Wawakilishi. Nimesema niseme hivi wenzangu walioandika ripoti hii wameshindwa kuzungumza ukweli kwamba Baraza la Wawakilishi mmekuwa wabaya wakutupatia semina Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Wenzetu sasa hivi akina mama *Alhamdulillah*, UWAWAZA imewasaidia sana wanaonekana wachangiaji wazuri, wasemaji wazuri na wauliza maswali wazuri lakini kwa akina baba imekuwa haramu, ndio maana ikapelekea mpaka pengine tukawa tunatishwa tunaambiwa tunakiuka Kanuni au taratibu. Kwa hivyo, naliomba sana Baraza la Wawakilishi kwamba litupatie semina, semina bado si za kutosheleza juu ya masuala mbali mbali na ndio maana kuna watu wengine wanagwaya hata kuchangia Miswada wanatoka nje ya *point*, kwa sababu hilo mmelikalia nyinyi kama viongozi. Naomba sana Ofisi yako Mhe. Naibu Spika, kwamba suala la semina kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lazima tulipate.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, wenzetu wanasaidiwa sana na Jumuiya yao ya UWAWAZA na wamekuwa sasa hivi *Alhamdulillah* wakali, wazuri wanakutolea Kanuni kila wakati, ukikosea tu uombe radhi. Sasa nafikiri na sisi akina baba tungepata kwa sababu hatuna ile jumuiya yetu humu Barazani imekuwa kama mnatupinda. Kwa hivyo, naomba sana Baraza la Wawakilishi ilichukue hili suala kuweza kutupa semina ya kutosha ili na sisi tuweze kuja kujenga hoja nzuri zaidi Barazani na kuepukana na yale yote ambayo yasiyofaa kuzungumzwa hapa ni kuitia dosari serikali yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nilitaka niseme hayo machache tu na baada ya hapo nathubutu kusema kwamba naunga mkono ripoti hii naomba kila la kheri *in shaa Allah* mwanzo mzuri.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Simai Mohammed Said atafuata Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na baada ya hapo atafuata Mhe. Bahati Khamis Kombo.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nianze kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Tunguu ambao wao ndio wamenifikisha hapa mimi leo kuwa msemaji wao lakini pia mtetezi wao.

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati yetu ambaye na mimi pia ni Mjumbe kwa hotuba nzuri aliyoitoa leo na kila neno alilokuwa analitoa alikuwa analitoa ndani ya moyo wake huku akisoma. Kwa kweli wengi hapa nyuma naamini mliguswa sana na yale ambayo aliyokuwa anayawasilisha.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia vile vile nichukue nafasi hii mimi nitapita juu juu tu mengi yangu nimeshayatoa kwenye Kamati na hapa nipo kuyasemea kidogo kwa sauti zaidi au pia yale ambayo niliyasemea lakini labda naamini yataweza kusaidia kwa njia moja au nyengine.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitaanza moja kwa moja na Idara ya Sherehe na Maadhimisho. Ni kweli katika kipindi hiki inawezekana mengi yaliyozungumzwa hapo mwanzo juu ya mapungufu au mawazo yaliyotoka kutoka kwa Wajumbe ambao wenzangu waliozungumza, lakini pia yapo mazuri ambayo serikali yetu imeyafanya. Kwa kweli nichukue fursa hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa sherehe nzuri mara hii ambazo hata wageni waliokuja wameona, Mji ulichangamka na zaidi sherehe hizi sasa tunaanza kuzigeuza sio kuwa ni za kiserikali, wananchi wenyewe sasa wanaanza kuzikamata kwao. Tumeona pale Maisara na siku ile pia nimpongeze Mwakilishi mmoja nilimuona Mhe. Abdalla Maulid Diwani akicheza na akinguruma juu ya *stage*, hiyo ni dhahiri kabisa kwamba wananchi na Wawakilishi wote walishiriki kwa pamoja katika sherehe hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo ningependa kutoa ushauri juu ya Idara ya Mawasiliano Ikulu. Nimekuwa nayazungumza mengi ndani ya Kamati na

wamenisikiliza au mawazo haya pia wameyachukua. Lakini moja ambalo Mjumbe aliyepita amelizungumza. Suala la uteuzi wa Mhe. Rais mara nyingi hutoka wakati wa jioni, utasikia saa mbili na robo, saa moja usiku kwenye taarifa ya habari kwamba Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi… Lakini wakati ule vyombo vyote vishapelekwa na watu wameshaandika taarifa zao kwenye magazeti na maeneo mengine, unakuta siku ya pili ule uteuzi hata ukiangalia gazeti hata moja hulikuti.

Kwa hivyo, mimi nashauri wale watendaji wa Mhe. Rais pamoja na wasaidizi wake wote nawashauri kwamba unapotoka uteuzi uzingatie na muda wa vyombo vya habari, kwa sababu mwisho wa siku utakuta unaanza kuwalaumu waandishi wa habari kwamba hawaja-*cover* ile *story*. Ndiyo maisha uteuzi anaofanya Mhe. Rais utakuta kwenye Zanzibar Leo, upate mara moja moja utakuta kwenye *Daily News* lakini magazeti mengine hayaandiki kwa sababu ile *story* tayari inakuwa imeshapitwa na muda. Kwa hivyo, tujitahidini sana kwamba uteuzi unaotoka kwa Mhe. Rais juu ya watu mbali mbali pamoja na nyinyi pia Waheshimiwa Viongozi mlioko huko mbele kwa watendaji wenu basi ufanyike wakati wa mchana ili tayari huku katika ma-*groups* ya *whatsApp* watu wanaanza kusherehekea waandishi wanakuja kumalizia.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili nataka nizungumze kwenye masuala ya Muungano. Kwanza niipongeze Serikali kwamba tayari kwenye vikao vyenu nimepata fununu kwamba mmekubaliana hasa watendaji ndani ya Serikali ya Muungano itakuwa asilimia 70 kwa 30. Hili jambo kwa kweli ni la kuwapongeza sana limekuwa linapigiwa makelele muda mrefu, kwa hivyo hongereni sana.

Lakini pia nataka nizungumzie kwenye hizo sherehe zetu za kitaifa. Mhe. Naibu Spika, sisi tuna siku tatu muhimu sana Watanzania katika sherehe, tunayo tarehe 9 ya 1961, tarehe 12 Januari, 1964, halafu pia tunayo tarehe 26 April, 1964. Wakati mwengine tunapata na mshangao pale ambapo viongozi wetu wanakuwa hawashiriki katika hizi sherehe. Nafikiria mmenifahamu, hizi siku tatu zote nilizozitaja za hii miaka ni siku muhimu sana, na sana sisi sote wananchi tunaangalia viongozi wetu wa kitaifa na hasa katika sherehe za Mapinduzi. Kwa hivyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba viongozi wetu wote wa Kitaifa wanakuwepo katika siku hizi.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia nataka nizungumzie suala la *Private Office* ya Mhe. Rais. *Private Office* ya Mhe. Rais ni sehemu moja muhimu sana. Mimi naamini leo Mwakilishi hapa akipiga simu kwa ofisi ya *Private Office* kutaka kuonana na Mhe. Rais basi inawezekana atachukua mwaka mzima hata jibu

asipewe. Lakini siasa zote ambazo tunazitengeneza huku chini za kumsaidia Mhe. Rais pamoja na serikali yetu panakuwa pana hofu. Na hapa nataka nishauri Rais akiendelea kufichwa fichwa sana anabakia kuwa Rais wa serikali, lakini Rais ni wa wananchi na Chama chake bado kipo ndio kilichomuweka pale na wananchi ambao ni viongozi na watu maarufu katika maeneo wanapenda kuonana naye na kuzungumza naye. Kwa hivyo, ni vizuri katika kumtengenezea siasa ya Rais na wananchi wake hasa kutoka chini basi Rais azidi kuunganishwa, na pale hata Mwakilishi katika jimbo husika akitaka kumuona Rais isiwe tabu.

Mhe. Naibu Spika, mimi Rais anakaa katika jimbo langu makaazi yake siku za *weekend* makaazi yake binafsi, lakini niseme ukweli hadi leo mimi napita pale nje ya geti lake wala sijawahi kuingia labda Madiwani wangu. Na kweli *appointment* nimewahi kuomba na nishawahi kusema mpaka kwenye *caucus* ya chama, wala sina nia ya kwenda kuomba chochote, kwenda kujitambulisha tu kama mimi ndiye Mwakilishi wako niko hapa kama kuna lolote Rais wangu niko tayari kulitenda kwa ajili yako. Najua ni Rais anaweza kufanya mambo mengi lakini ndio ukarimu na utaratibu tulivyofundishwa sisi, na wengine pia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ndugu zangu kutoka Pemba wana hamu ya kuonana na Mhe. Rais tunakuwa tunazungumza wakati mwengine, lakini hata ukipeleka wana hofu kwamba hata ukitaka kumuona hawatafika. Kwa hivyo, mimi nashauri sana mambo haya yawekwe sawa sio lazima kwamba mtu awe anaomba omba omba sana, lakini naamini wenzangu wana hamu ya kuonana na Mhe. Rais kuna vitu wanataka kuzungumza naye kuna vitu wanataka kuzungumza wao wenyewe na mtu mwengine asisikie. Kwa hivyo, ni vizuri Rais akatengenezewa mazingira yake juu ya Wajumbe wa Baraza na hii ni sehemu yetu sisi tutakuwa pamoja. (Makofi).

Mhe. Naibu Spika, sehemu moja nyengine nataka niizungumze kwenye masuala ya Ukimwi. Hili ni janga lipo wengine wanataja kwenye masuala ya vilabu wamezungumza lakini kuna jambo hatulioni, mitandao, *internet*. Leo mtu yeyote akifungua kwenye simu hii kwenye *website* au mitandao ukitaka kuangalia maeneo yenye uchafu unaangalia bila ya wasi wasi, tena una-*download video* unamtumia mtu mwengine. Lakini wataalamu tunao wa kuweza kuzizuia hizi *website*, sio mitandao yote hii mitandao ambayo inahusiana na masuala ya ngono, ambayo watoto wetu hawastahiki kuangalia. Hata hao vijana leo ukisimama njiani anayeuza *CD* unamwambia vipi unazo hizo, anakwambia zipi, unamwambia zile basi anakutolea kwenye begi au sehemu kwa nyuma unazipata. Sio kama nimenunua nimeshajaribu kufanya hivyo na Mhe. Waziri tulikuwa pamoja siku nilipofanya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. (*Makofi*).

Kwa hiyo, niseme tu kwamba katika masuala haya maeneo kama haya sisi kama Wawakilishi tunafanya utafiti mwingi sana, na nampongeza sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, nilimsikia siku moja anamwambia Waziri mwenzake hawa wanafanya utafiti Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, wakati mwengine wakisema wanasema ukweli. Kwa hivyo, masuala haya ya ngono mnavyoangalia nyinyi msikae mukawalaumu hawa watu kwenye Tume, lakini muangalia katika malezi. Leo mtoto ana miaka 17 au 15 saa sita za usiku anafanya nini nje, inakuwaje wazee hamuwakemei huko mitaani tunawaachia. Mtoto anakwenda skuli ana miaka 14 ana simu ya kisasa inakuwaje anaificha kwenye begi, ijapokuwa haionekani anaizima lazima utaratibu wa malezi utumike. Mimi nimekuwa nasema siku zote *parental guidance* ndio njia pekee, mimi nilikuwa na miaka 10 ikilia honi tu niko nyumbani nafanya *homework* juu ya meza pale kwetu Shangani.

Mhe. Naibu Spika, haiwezekani mtoto wa miaka 10 mpaka saa 4 za usiku kuwa yuko Forodhani, uko mitaani unafanya nini, kiasi utakuta ndio watoto wanaharibiwa hatujui kwa nini. Sasa haya mitandao pia tuangalie maeneo ambayo iweze kufungiwa kwani wataalamu wapo tuzifunge, vijana tunao tena wako wengi sana, mimi wengine hata kwa majina ninawajua, naweza kupeni majina wakaweza kuwasaidia na njia gani ya kufanya. Ifungeni tena namjua tuna Waziri mmoja Mhe. Waziri wa Afya anajua mambo haya amefanya kazi anayajua kabisa masuala haya kuwafungia. Kwa hivyo, mimi nashauri haya muyazuie ili vijana wetu mengine kila kitu kinakwenda kwa muda, tufanye mambo kwa mpango akifika miaka 18 tena huko kidogo anaitwa ni *as adult* unakuwa muda ni muafaka.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine nataka nizungumze suala kwenye Wizara yetu ya Muungano. Mimi kama Simai Mpakabasi ningefurahi kwenye Wizara hii ya Muungano najua mamlaka haya hayapo kwa Mhe. Rais wetu wa Zanzibar, na sisemi kwa hivyo lakini ningefurahi kama Mzanzibari na Mtanzania nafasi za kisiasa wakati mwengine na nyinyi mzisemee huko. Mhe. Naibu Spika, inapendeza kwenye Wizara ya Muungano kwenye nafasi za juu pawe na sura ya Muungano, tunahojiwa huko nje tunasemwa na wenzetu lakini ni vizuri pakapendeza. Haya ni mawazo yangu, lakini haya nazungumza na wengine pia.

Mhe. Naibu Spika, mengine nimetaka nishauri Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, hivi Rais wetu kuonana na wawekezaji, wakulima kuna tatizo gani. Ikulu ni ya Rais wetu lakini hata sisi pia tunapenda watu wetu maarufu huko nje wanaotuunga mkono wakae naye. Rais kualikana na hizi jumuiya zote zipo nimeshazungumza na nikatoa mawazo mara nyingi, hivi mwisho wa mwaka

kuitwa wawekezaji ambao ni *the biggest* hapa ni wawekezaji wa masuala ya utalii, kukaa nao hao wazungu, wawekezaji wazalendo mkapiga chai unampa matumaini kuna tatizo gani.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipokuwa Mwenyekiti wa Wawekezaji sekta ya utalii tumemualika Mhe. Makamu wa Pili wa Rais alikuja kwenye *function to dinner,* muulize mwenyewe siku ile watu walifurahi wakajenga matumaini na wengine walitokwa na machozi kuona kwamba tayari serikali kwa mujibu wa huu mfumo wa *Public Private Partnership* wanakwenda kwa mapenzi haya wanakuwa pamoja. Lakini kwa muundo uliokuwepo sasa hivi tusipokuwa makini wawekezaji wanaonekana kuwa na njia mstari ule kule, serikali iko huku. Kwa hivyo, tuwavute karibu zaidi tuwapende na haya niliyazungumza pia nafikiria jana au juzi katika masuala haya. Mimi huku ndiko nilikotoka sio kama nilikuwa ni mfanyabiashara mkubwa, lakini katika hizi jumuiya nimeshiriki sana, ndio maana natoa ushauri huu na huu utawasaidia hata nyinyi Mawaziri kuwafanya karibu katika mambo mengine ambayo serikali hii mmeazimia kuyafikisha hasa katika utekelezaji wa Ilani yetu kuelekea mwaka 2020.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia mimi labda niseme tu kwamba Kamati yetu sisi ina mambo mengi sana na naamini mkiangalia madawa ya kulevya yamezungumzwa, kuna Ofisi ya Rais imo humu, Makamu wa Pili, kuna masuala ya maafa, kuna mambo mengi sana. Hii Kamati yetu ilipata changamoto. Kwa hivyo tunajipongeza sana kwa kazi nzuri tuliyoifanya Kamati yetu. Pia tunapongeza watendaji wa serikali jinsi gani wametupokea vizuri hasa Ofisi ya Makamu wa Pili na Ofisi ya Rais pia kwa pamoja wametupa mashirikiano mazuri. Kuna changamoto nyingi ambazo zipo ila tutambue kuna nyengine pia hapa unaweza ukazizungumza lakini twende kwa utaratibu kwa sababu hizi ni Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kuna umakini wake unaweza kutoa ushauri lakini pia uangalie na lugha zetu tunazokwenda nazo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nikushukuru sana wewe kwa nafasi hiyo na jambo moja tu la mwisho nimesahau samahani. Mwaka mzima tumeona viongozi wengi wa kitaifa wakija katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sisi pia Wazanzibari tungependa tuone viongozi wa kitaifa wanapofika Tanzania Bara kwenye safari zao basi na hapa Zanzibar sio vibaya, tumemuona Mfalme wa Morocco alikuja hapa kwenye mapumziko yake na akizunguka Mjini na alipapenda kiasi kwamba alirudi tena mara ya pili. Mimi naamini wanapokuja hawa viongozi kutoka nchi tofauti tunakuwa tunaandikwa sisi Zanzibar katika magazeti ya kwao ambapo kwetu sisi pia kwa utalii na kwa

kuitangaza nchi inatusaidia sana, kwa sababu ni vizuri kwenye nchi yako ukaandikwa as *positiveliy*, *political* unapata marafiki wapya, *social* ni nzuri kwa nchi, uchumi wako unapata kuzungumziwa vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo nikushukuru sana kwa busara zako na kwa kuniona mimi. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Simai Mohammed Saidi. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na atafuata Mhe. Bahati Khamis Kombo na ajitayarishe basi Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu jioni hii kuwa katika Baraza lako tukufu kuchangia ripoti ya kamati hii.

Lakini nikushukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Pia niipongeze Kamati pamoja na Mwenyekiti kwa hotuba yake aliyoitoa kwa ufasaha mkubwa. Vile vile nataka niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa kunichagua kuwa katika Baraza lako tukufu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi yake nzuri na pia niwapongeze wote Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi yao nzuri, na kama tunavyojua Ofisi hii ina kazi kubwa katika nchi yetu ndio inayoratibu kazi zote za serikali yetu, kwa hiyo nawapongeza sana. Vile vile nataka nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, ni mtu makini sana namshukuru kwa kazi yake nzuri na umakini wake mkubwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika ukurasa wa 9 wa ripoti hii ya Kamati kwenye Idara ya Uratibu na Shughuli za SMZ hasa katika suala la *TASAF*. Kama tunavyojua *TASAF* ni mkombozi wa kaya maskini zinasaidia sana wananchi wetu, lakini mimi niseme katika Unguja na Pemba *TASAF* imeweza kusaidia karibu watu 204 Unguja 126 na Pemba 78.

Mhe. Naibu Spika, niwashukuru *TASAF* kwa kazi yao nzuri na wanajitahidi sana kusema ukweli, lakini mimi nisikitike kidogo, hawa *TASAF* wanapokabidhi miradi kwa Wizara husika mara nyingi inakuwa miradi hii mengine inakwenda lakini kuna mengine haiendi inakufa.

Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano mmoja mzuri, kule Pemba tulikwenda na Kamati na mimi pia ni Mjumbe wa kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Tulikwenda kwenye mradi mmoja kule Micheweni wanakolima wananchi, bahati mbaya au nzuri kuna sehemu maji ya chumvi yanaingia, *TASAF* wamejenga bonde lile kwa mabilioni ya fedha. Sasa kuna mlango mdogo tu ambao unaingiza maji ya chumvi yanaingia kwenye mazao ya wakulima. Sasa hivi wakulima kule hata kulima hawawezi tena kwenye shamba la Micheweni, yaani imekuwa kama upande mmoja imewatia hasara kubwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukitizama ule mradi mimi napongeza *TASAF*, kazi iliyokuwepo ku-*repair* ule mlango ni ndogo tu, lakini maji yanapita yakijaa huku yanapita kwenye ule mlango uliokuwa pale. Kwa hivyo, mimi naomba sana Wizara husika inayopewa hii miradi ishughulikie kwa sababu fedha nyingi sana zinapotea. Ukitizama ninawashukuru sana wanaotusasidia fedha hizi, ukitizama kama hapa wahisani wetu *USA* Marekani wametusaidia karibu Dola milioni kumi za Kimarekani kwenye mradi huu wa *TASAF*, ukitizama Bill Gates wa Marekani katusaidia karibu Dola milioni nne, Serikali ya Tanzania imetoa karibu Dola bilioni 60.5 katika mradi huu na wengine pia nawashukuru sana wafadhili. Lakini hii miradi wakija wenyewe kutizama kama hao wahisani watavunjika moyo kwa sababu inakuwa haifuatiliwi na haishughulikiwi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, mimi naiomba serikali inapokabidhi miradi ya *TASAF* basi wao waishughulikie wapoteze hata fedha kidogo kwa kuijali miradi kwa sababu fedha nyingi zinatumika kwa wahisani. Kwa hiyo, mimi niombe sana waiangalie miradi hii ya *TASAF* inasaidia kaya zetu maskini, kuna wananchi wamefaidika sana kwenye miradi hii.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi niseme kuna baadhi ya viongozi au wanasiasa sijui wanasema kwa madhumuni gani na hii sio hapa tu Pemba au Unguja mpaka Tanzania Bara kwa ujumla, kwa sababu mimi Mjumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa Zanzibar, Baraza la Wawakilishi lakini kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pia niko kwenye Kamati ya Utawala wa Serikali za Mitaa, hii *TASAF* pia iko huku na huku mimi ninayo. Kwa hivyo, nimepata bahati kutembelea mpaka Mikoani kuangalia miradi ya *TASAF*.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nashukuru sana lakini nasema kuna baadhi ya viongozi hasa wanasiasa wanapita kuwaambia wananchi kwamba hizi fedha msichukue ni pesa za *freemason*, hizi pesa ni mashetani, hizi pesa zinatoka sehemu mbali mbali lugha tofauti wanawadanganya. Mimi nawaomba sana

hawa wanasiasa, wanaolengwa ni kaya maskini. Sasa leo ukiwadanganya wananchi wetu kuwa pesa hizi ni za *freemason*, kwa kweli inawatia unyonge na wananchi wengine wanaamini pesa hawachukui, unajua Zanzibar Pemba na Unguja mimi nashukuru Dini imetukaa, tunaamini sana dini lakini wanapotoshwa kwa mambo ya uongo, hizi pesa wanatoa Marekani, wanatoa Serikali ya Tanzania bilioni 60 kwa msaada leo unawaambia pesa za mashetani. Kwa hiyo, mimi naomba sana tabia hii waache na serikali iwachukulie hatua viongozi kama hao wanaowadanganya watu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa mapokezi makubwa sana ya Kamati ya Bunge ilipokuja Zanzibar na Pemba kutembelea mradi huu wa *TASAF*, kwa kweli tulipata mapokezi mazuri nimshukuru sana na mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Utawala wa Serikali za Mitaala, kwa kweli Wabunge wamefurahi na wamesema watakuja tena kuangalia miradi ya *TASAF* iliyokuwa Unguja na Pemba imefanya kazi vizuri sana. Kwa hivyo, nimshukuru Mhe. Waziri kwa kazi yake nzuri ya kusimamia miradi ya *TASAF*.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niingie tena katika ukurasa wa 9 katika Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ na SMT. Kamati yako Mheshimiwa ilipata bahati ya kwenda kutembelea Dar es Salaam kuna baadhi ya sehemu zetu hasa kwenda kuangalia nyumba ambayo anafikia Mhe. Rais, faragha pale Dar es Salaam. Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwa ufupi lakini nataka niseme ile nyumba kwa kweli imechakaa na ni nyumba ya muda mrefu, kwa hadhi ya Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na tunavyompenda ile nyumba ifanyiwe matengenezo makubwa iweze kufikia hadhi ya Rais wetu kufikia pale.

Mhe. Naibu Spika, ile nyumba ile tulikwenda kuiangalia kama Wajumbe wa Kamati kwenda kuiona kuna mambo mengi yanataka kubadilishwa pale. Kwa hivyo, mimi naomba tufanye haraka nyumba hii itengenezwe iwe na hadhi ya kisasa iende na hadhi ya Mhe. Rais wetu. Ukitizama hata ule uchakavu wa jengo, paa lake pia sio zuri, hata mandhari ya bustani sio mazuri, ukipita nje unaweza kumuona Rais kwa ndani. Kwa hivyo mimi naomba sana tuangalie hili suala kwa undani na kwa haraka hata kiusalama pia haipendezi kwa hali ilipo na Mhe. Rais anafikia pale akienda. Hivyo mimi naomba sana tuiangalie kwa haraka sana, hata ukiangalia miundombinu yake ya maji, umeme haiko katika hali nzuri.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee tena katika ukurasa huo huo wa 9 Idara ya Uratibu na Shughuli za SMZ na Muungano. Kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri kijana Mhe. Januari Makamba, Waziri wa Muungano kwa juhudi zake

kubwa na kwa kutaka Zanzibar kutatua hasa hizi kero za Muungano. Mimi nimpongeze sana na nimshukuru sana Waziri huyu na Mwenyezi Mungu amjaalie nguvu tuweze kufanya naye kazi kutatua hizi kero zetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, bahati nzuri Kamati yako ilifika kwa Waziri kuzungumza naye Ofisi ya Makamu wa Rais kule Muungano Dar es Salaam kwenda kuzungumza na Waziri kwa baadhi ya changamoto za Muungano. Mimi nataka niseme kwamba Waziri ana nia nzuri sana na mimi mmoja nimezungumza naye na Wajumbe wa Kamati kuna mambo muhimu sana tuyaangalie.

Juzi kipindi hiki cha ripoti za Kamati za Bunge kuna Mjumbe mmoja kasema ndani ya Bunge la Jamhuri kitu ambacho mimi mwenyewe sijafurahi, anasema Zanzibar inadaiwa shilingi bilioni 124 za umeme na *TANESCO*. Mhe. Naibu Spika, sawa tunadaiwa bilioni 124 za TANESCO wanatudai, ZECO wanadaiwa, lakini tutizame kuna mambo hapa lazima tuyaangalie na sisi Zanzibar tunataka tupate vianzio vya fedha, fedha hizo tutazitoa wapi kuwalipa wenzetu wa Tanzania Bara. Kwa hivyo, mimi naomba kitu kimoja, kuna mambo wafanyabiashara wetu wanachukua mizigo hapa wanapeleka Dar es Salaam mizigo midogo midogo, wafanyabiashara hawa watu wetu maskini, wanyonge ndio ajira yao, wakifika Dar es Salaam pale wanaambiwa walipe ushuru, mizigo yao inamwagwa chini wanaambiwa hapa bidhaa hizi mlizochukua ulipe ushuru, fedha zile pengine haziendi serikalini lakini wanachukua watendaji pale.

Mhe. Naibu Spika, mimi namuomba sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hilo suala tuliangalie kwa undani kabisa. Tukiangalia Zanzibar mfumo wake kibiashara ukichukua mzigo kama nchi yoyote ukileta Zanzibar kontena, lile kontena ukilipeleka Tanzania Bara bei yake inakuwa rahisi, ukilileta hapa Zanzibar bei yake inakuwa iko juu. Sasa ukitizama mzunguko uuchukue hapa mzigo huo uupeleke Tanzania Bara tena kuna *difference* nyengine ile pale, ushuru ulipe pale. Mhe. Naibu Spika, itafika wakati Zanzibar biashara itakufa hapa, lazima tuliangalie hili suala vizuri sana ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu na pia ni ajira kwa upande wetu na pia serikali inahitaji fedha.

Mhe. Naibu Spika, tunadaiwa huko, mfano mdogo nimetoa tunadaiwa shilingi bilioni 124, Mjumbe anasema ndani ya Bunge tunadaiwa, kwa kweli kitu hicho mimi sijafurahi nacho na tuangalie hivi vianzio vya mapato. Sisi tunategemea utalii hapa Zanzibar, sasa utalii ukikataa hapa kesho tutapata vianzio vya mapato? Tutabakiwa na biashara sasa biashara soko la Zanzibar lazima mzigo ukija hapa hawa wafanyabiashara wadogo wadogo wasibughudhiwe kule Bara

wakipeleka. Kwa sababu watu wanakuja kununua mzigo hapa wanapeleka Bara lakini wanasumbuliwa pale Bandarini, lazima katika Muungano wetu huu mmoja ataathirika na mmoja atafaidika. Kwa hivyo, naomba sana Muungano wetu huu ni wa kihistoria, wa kidugu lazima tutizame na tuuenzi tusichafuane kwenye mambo madogo madogo ikawa mtu anapata sababu ya kutuchafua kwenye serikali zetu mbili hizi na Muungano wetu mzuri huu wa kidugu na wa kidamu, ukichafua kwa mambo madogo madogo kama haya Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hizi kero ziangaliwe.

Mhe. Naibu Spika, kwa mfano sasa hivi ukitizama kuna Mhe. Mjumbe alisema hapa, hilo suala ninamuunga mkono kweli, ukichukua gari ya Zanzibar ZNZ ukipeleka Tanzania Bara unaambiwa ulipie ushuru, kama umelipa shilingi milioni tano uongeze kule shilingi milioni kumi gari ile. Sasa Mjumbe anakwenda Tanzania Bara kutembea na gari yake kwenda Arusha Ngorongoro wiki mbili tu anarudi.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, mimi nakupa mfano gari ya Kenya inakaa Dar es Salaam pale karibu mwezi au miezi miwili, gari ya Malawi, gari ya Zambia inalipishwa mpakani Dola 50 tu inaingia, lakini gari ya Zanzibar inakuwa tatizo. Sasa hili naomba liwekwe sawa tupate kufanya vizuri kama mtu anakwenda na gari yake anataka kutembea kurudisha basi atiwe kwenye *system* baada ya wiki mbili airejeshe na kama akitaka kuibakisha pale basi upangiwe ushuru uwe mdogo kidgo kulinganisha na gari kuteremsha Bara.(Makofi).

Mhe. Naibu Spika, jana nilikuwepo *TRA*, bahati nzuri nikauliza swali zuri, sasa hivi ushuru huu unaolipia hapa *difference* ukiwa na gari yako unaipeleka unalipia Zanzibar, sawa lakini ushuru ukiuangalia wanaangalia ku- c*ompare* na ushuru wa Bara, kama gari umeteremsha Bara shilingi milioni mia moja ushuru, hapa umelipa shilingi milioni 40 uongeze shilingi milioni 60, haiwezi kuwa sawa, soko kubwa la gari litakuwa liko kule lakini hapa Zanzibar lazima kwa sababu tuna *price* yake na hiki kisiwa lazima ushuru uwe mdogo. Ushuru wa hapa ukipitisha lazima uwe mdogo, ukienda kule ulipie gari unaweza ukaiuza gari kwa bei yako na faida ukapata. Ukitizama hata ushuru Hong Kong na China ni tofauti, ukienda Hong Kong ushuru wao unakuwa mdogo ukitoa mzigo pale na ukitoa kule China ushuru wao unakuwa mkubwa. Kwa hivyo, lazima tuangalie sisi ni kisiwa tuweze kuwasaidia wananchi wetu ili mtu aweze kusafirisha mzigo wake kwenda kule bila ya kusumbuliwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe mfano, mimi ni Mbunge wa Jamhuri kupitia Baraza la Wawakilishi lakini mimi nina gari Bara ya ZNZ natumia namba yangu ya uzalendo ya Zanzibar, lakini unakuta kama sijatia bendera mimi

Dodoma sifiki Mhe. Naibu Spika. Sasa nasema hii gari inatoka Zanzibar jamani haina tatizo lakini kama itabidi ukitoka kilomita mbili au tatu askari anakukamata gari weka pale kama hujajitambulisha vizuri gari huipati tena. Naomba sana Muungano huu sio kugombana ni Muungano wa kidugu, wa kidamu kama nilivyosema mwanzo. Kwa hivyo, naomba hizi changamoto ndogo ndogo tusisahauliwe hasa kwenye gari za Zanzibar, wananchi wanataka kwenda kustarehe na magari yao kule wapewe fursa, kizazi cha sasa kinachokuja hakitoelewa kumwambia gari yako usiende nayo Bara, wakati hii ni nchi moja Muungano tunatumia *passport* moja lazima tushirikiane kwa nyanja tofauti, tuwe na haki za huku lakini tunaweza kutumia hata kule haki zetu za Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mimi nashukuru Muungano sina tatizo nao naupenda kwa nia njema na nia safi, lakini haya mambo ya kero kidogo Mheshimiwa naomba yaondoshwe. Namshukuru Mhe. Waziri wetu wa Muungano, Mhe. Januari Makamba kuna mambo karibu tisa yameshatatuka lakini mimi sitaki kuyasema hapa sio sehemu yake mimi nikayasema. Lakini naomba vyombo vya habari baada ya muda mutoe zile kero za Muungano zilizotatuka, kwa sababu huko nje tunapata matatizo makubwa hasa tukifika kwenye uchaguzi mwaka 2020, *agenda* kubwa inakuwa mtu Muungano, *agenda* kubwa kero ya Muungano, agenda kubwa mizigo Bara, kwa nini mtu haulizwi jimboni mpinzani maji hamna, hiki hamna anasema kero hizi za Muungano tu, inatupata sisi wagombea wa siasa. Hizi kero za Muungano ziondoke twende kwenye mambo mengine, huu Muungano wetu utaendelea kudumu kwa maisha na maisha kwa sababu tumeshachanganya mpaka damu sisi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi namshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya hata Bunge la Katiba alizungumza mambo mazuri sana kuhusu Zanzibar. Pia nampongeza sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi alizungumza mambo mazuri sana kwenye Bunge la Katiba hata wale Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano kuna baadhi hawafahamu historia ya Zanzibar, hawajui kabisa kama Zanzibar imetokea wapi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Umebakiwa na dakika mbili malizia Mhehsimiwa.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante, hawajui kabisa kama Zanzibar imetokea wapi. Kwa hivyo, naomba sana hii elimu pia wale Wabunge wa Jamhuri waipate kama Zanzibar ilikuwa imetoka moja, mbili, tatu mpaka kufikia hapa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kidogo kwenye suala la madawa ya kulevya. Mimi nimpongeze sana Mhe. Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam. Mimi najiuliza kweli wenzetu Tanzania Bara leo wametangaza wauza unga wote, wavutaji, nawapongeza. Sasa hivi ukitizama Dar es Salaam yule muuza unga anatafuta njia pa kwenda au mvutaji, lakini sisi tumekaa kimya kwa nini. Hivyo hapa hakuna wauza unga, hakuna wavutaji unga, unga hauingizwi hapa. Mimi namuomba Mkuu wa Mkoa afanye haraka kuwatangaza wafanyabiashara ya unga, awatangaze hadharani. Kwa sababu hii biashara sio ya kubahatisha au atangaze ikiwezekana hata kesho na waitwe. Kwa sababu muuza unga anajulikana hawezi kutangazwa mtu asiyejulikana mambo yote yako wazi Unguja hii. Hili jambo ni hatari kwa vizazi vyetu na vijana wetu, hivyo naomba atangaze tutakuwa tunajenga *sober house* iwe sisi tunazalisha kijana avute unga halafu tumpeleke *sober house*, kazi yetu itakuwa kutibu tu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hizi *sober house* Pemba zipo na hapa zipo zivunjwe zote ziwe hazipo hasara tu. Mimi naomba hawa wafanyabiashara wakamatwe haraka kama wenzetu Bara tuwaunge mkono hii operesheni twende nao sambamba tutaimaliza kwa muda wa wiki mbili tu hapa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo mimi niseme muda umekwisha lakini hata ukiangalia hapa *airport* udhibiti wa madawa hasa haupo. Kwa sababu zile mashine zao hata unga hazioni, sisi *experience* wa kutizama huyu mtu kaja na unga au hana unga yeye anaangalia mashine na mashine haioneshi unga hata ukitia kwenye begi. Mimi nimeshapita pale tumekwenda na Kamati tushawaambia hebu tia mzigo huu unaonesha nini, kitu cha unga wanaseama kuna rangi nyekundu lakini hujui nini, wanaona chuma, funguo na simu tu. Basi akae mtu pale mamlaka mwenye *experience* na ambaye atamuona anamuweka pembeni amuhoji pia hilo halipo, mtu akija na unga ukimuona uso wake na macho yake unamjua kwamba huyu amekuja na unga. Sasa wawekwe watu angalau *intelligence,* wanafahamu au wapate mafundisho kuwajua watu wa unga wanakuja kwa njia zipi au kwa mambo yepi. Kwa hivyo, wakae pale ili tudhibiti haya mambo ya unga.

Mimi namuomba sana Mhe. Rais wetu wa Zanzibar pia awe mstari wa mbele kabisa katika kutokomeza madawa ya kulevya katika hawa watu wafanyabiashara wasionewe huruma wanatumaliza. Sasa hivi ukiisoma takwimu ya wateja Zanzibar iko juu sana, imekuwa kama hapa ni sehemu ya kuja kuvuta unga tu kustarehe. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Muda wako Mheshimiwa umekwisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono ripoti kwa asilimia mia moja, ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo baada ya hapo ni Mhe. Shehe Hamad Mattar kama muda utatosha.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia machache.

Kwanza kabisa nichukue fursa hii ya kumpongeza Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pia niipongeze Kamati hii kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kupekua mambo mbali mbali na leo hii wametuletea ripoti yao kuweza kuichangia.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitakwenda moja kwa moja katika udhibiti wa dawa za kulevya. Katika kifungu Namba 5 Kamati ilifanya ziara yake uwanja wa ndege na bandari na kubaini kutokuwepo kwa mashine ya *X-ray* Unguja na Pemba. Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa mashine hii basi ni changamoto moja kubwa ambayo inawakabili wafanyakazi wetu wa sehemu hizi. Kwa sababu wakati mimi sijakuwa Mwakilishi tayari taarifa ambazo zilikuwa zikitoka kwamba wafanyakazi wa *airport* au bandarini wanahusika na kupitisha madawa ya kulevya, kumbe ni kinyume na utaratibu ulivyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ukosefu wa mashine hii mfanyakazi tunampa mzigo mzito sana, mashine zilizopo pale kama hazitoshelezi kuangalia jinsi gani mtu kameza dawa za kulevya katika tumbo lake tutaendelea kusema kwamba tunavaa nguo lakini mgongo wetu uko wazi. Nimuombe Mhe. Waziri kwamba suala hili la ukosefu wa mashine hii lifanyiwe utaratibu wa haraka ili tuweze kuondokana na tatizo hili na kuwapa uzuri wa kazi wale wafanyakazi waliopo pale bandarini na *airport*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Kamati katika kutembea kwake iliona ukosefu wa chumba cha upekuzi kwa wanaoshukiwa kuwa na dawa za kulevya. Hili ni jambo ambalo nalo linarudisha nyuma wafanyakazi wetu na wale wananchi ambao wanapita katika sehemu zile. Mimi ni mtu mzima, nina akili timamu lakini napita pale chumba cha kupekulia hakiko vizuri napekuliwa kinyume cha utaratibu. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri suala hili alifanyie utaratibu ili wananchi wakipita pale waweze kupekuliwa kwa ufasaha kabisa na kiwe chumba cha siri sio pale hadharani.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ilipita na kuona kutokuangaliwa kwa mizigo inayosafirishwa nje ya nchi *cargo*, katika kiwanja cha *Abeid Amani Karume International Airport*. Mhe. Naibu Spika, iko siku tutatiliwa mabomu ndani ya *cargo* hizi na kisiwa kiweze kughariki. Kama ni kweli tatizo hili lipo na halijashughulikiwa na viongozi wetu wote wapo na hili wanalijua, kwa kweli ni tatizo kubwa sana. Mhe. Waziri nakuomba tena suala hili ulishughulikie kwa kina ili nchi yetu tusije tukapata tatizo.

Mhe. Naibu Spika, kamati imekuta kukosekana kwa mawasiliano ya uhakika katika ofisi za wanaohusika na upekuzi na ukaguzi wa madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, kukosekana kwa mawasiliano haya ni hatarishi kwa wale wafanyakazi ambao tumewaweka pale. Likija kutokea la kutokea hatuna la kusema kwa sababu mawasiliano ya uhakika hayapo na serikali inalijua hilo, wapi tutakwenda Mhe. Waziri naendelea kukuomba ulifanyie kazi kwa kina ili liweze kuondoka kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika changamoto zilizoikabili Tume ya Uchaguzi Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, mimi nitachangia hapa kidogo katika Tume ya Uchaguzi iliopo Mkoani Pemba. Mhe. Naibu Spika, naomba ile Ofisi ya Tume ya Uchaguzi iliopo pale Mkoani, ikiwezekana basi itafutiwe Ofisi nyengine iliyokuwa ni nzuri na kule nyuma iliko iondoke, kwa sababu ofisi ile inabebwa na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mkoani, na ndani ya Ofisi ile kwa kweli muna ofisi nyingi hazikidhi haja. Kwa hivyo, naomba sana kushughulikiwa suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kidogo niko katika changamoto zinazoikabili Idara ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Naibu Spika, kamati ilitembelea na kuliona hilo katika kisiwa chetu cha Pemba. Mhe. Waziri nikuombe kwamba watu wamesema kwamba kinga ni bora kuliko tiba, mpaka hii leo bado hatujawa na ghala la uhakika ambalo litadhibiti vifaa vile vya maafa katika kisiwa chetu cha Pemba. Hili jambo sio la mchezo, ni bora kwanza tutafute jinsi ya kulitatua tatizo hili na mvua hizi ziko karibu, hatujui zitanyesha vipi ili tuweze kujipanga mapema basi ni lazima tuweze kutafuta namna ya kuipata ghala hili kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na pia niwashukuru Kamati yote walioshiriki katika ripoti hii. Kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Chambani, naipongeza kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bahati Khamis Kombo kwa mchango wako mzuri. Sasa nitampa nafasi Mhe. Shehe Hamad Mattar.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii nichangie katika hotuba hii.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia afya njema. Nianze kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naipongeza kamati hii kwa kazi kubwa iliyofanya na pia kazi iliyofanywa ni kubwa sana. Kamati zote zilizoundwa naziona kama ni maabara iliyofanywa ili ichunguze maradhi ya Zanzibar. Kwa hivyo, hizi kamati zimepata nafasi ya kuona kila kitu ambacho kuwa kinatuathiri na kipi kitakachoweza kutufaa katika nchi yetu ya Zanzibar. Kwa hivyo, kamati hii, hii itakuwa ni ripoti ya daktari, Mawaziri, Mhe. Rais ni vyema wakazifanyia kazi ili kuona kwamba nchi yetu imefika pahala pazuri, pamoja na michango mengine inayotolewa na Wajumbe hapa Barazani. Kwa hivyo, ni kazi kubwa sana kamati zinazofanya na nina ipongeza sana kwa asilimia mia juu ya mia kabla sijaendelea kuchangia.(*Makofi*).

Pia niipongeze Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi ya uratibu wake katika shughuli za serikali, kwa sababu Ofisi hii kama haikuratibu vizuri na mimi kuna kero ambayo imenikabili jimboni kwangu isingeweza kufanikiwa. Lakini wameweza kuratibu shughuli za serikali mpaka leo ile kero yangu iliyokuwa inanikabili katika upatikanaji wa maji katika Shehia zangu za Finya, Kinyasini na Taifu imeanza kutatuka, haijakamilika. Lakini ilikuwa ni kero ya kisima kilichokuwa FFU Finya pale nacho kimeanza kupata *pump* na tayari maji yanaanza kutoka lakini hayajatosheleza, kwa sababu kwa taarifa niliyonayo maji hayajafikia kule, ingawa *pump* ni ndogo. Lakini hata hivyo ni hatua ya mwanzo, ni imani yangu kwamba itaendelea kuifanyia ili iweze kutosheleza.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wa ripoti hii pale inapozungumzia madawa ya kulevya. Suala la madawa ya kulevya ni janga kubwa sana lakini nasikitishwa sana katika ripoti hii wenzetu wamegundua suala la kubadilishwa kwa ushahidi au kupotea kwa ushahidi kwa washtakiwa kutokana na vyombo husika, iwe Polisi au Mahakama inakuwaje, na hatua gani zinazochukuliwa kulingana na wale watu ambao wanasababisha. Kwa sababu ushahidi ni sehemu moja wapo ya kuendesha kesi na ndio maana unasikia kwamba kesi haiendi kwa sababu hakuna ushahidi. Sasa leo kama ushahidi kama huu, kuna watu wanafanya njama wanaunyemelea na kuuchukua halafu kesi inafutwa. Nani muhusika wa kumkamata na suala hili, ama ni Polisi au Mahakama. Kwa hivyo, ni lazima kuwe na vyombo maalum tena madhubuti vya kuweza

kudhibiti huu ushahidi ili usiweze kuwakosa hawa wahalifu. Kwa hivyo, suala hili ni vyema kutiliwa maanani katika kuona kwamba ushahidi huo haupotei.

Mhe. Naibu Spika, naungana sana na kamati iliyotoa maoni ya kwamba kutoa elimu kuhusu madawa ya kulevya. Madawa ya kulevya ni vyema elimu hii isiishie kwenye maskuli za maandalizi, skuli na madrasa. Mim napendekeza kwamba elimu hii kuhusu athari ya madawa ya kulevya itolewe mpaka kwenye skuli za sekondari na vyuo na mpaka katika Shehia kwa sababu humu wote kila mmoja aweze kujua athari yake, na ikiwezekana ule mpango wa zile sinema ambazo zilikuwa zikioneshwa zamani basi urudi. Vijana wadogo wale na wakubwa zipite sinema za kule vijijini kwenye TV zioneshwe zetu, kama ni michezo ya kuigizwa, kama ni michezo mengineyo ambayo itaweza kuleta ujumbe ule ambao utaonesha athari ya madawa ya kulevya inavyotuathiri Zanzibar na dunia kwa ujumla. Kwa hivyo, ni vyema juhudi hii ikachukuliwa katika kuonesha elimu hii inafikia.

Kwa sababu hivi sasa Mhe. Naibu Spika, baadhi ya skuli zetu za vijijini na mpaka mijini, wamekuwa wanafunzi ni wavutaji wakubwa wa bangi, mpaka wanapelekea sasa wanafukuzana na walimu na wanawapiga walimu na wanafanya vitendo vichafu vile vile ambavyo vinakatazwa kabisa vinafanywa, kwa sababu ulevi ni mama wa maasi. Sasa leo mwanafunzi ameshaanza kulewa yuko skuli anaendelea wapi huyu. Kwa kweli kama hatukumuwahi huyu na tukaweka masomo maalum na tukatoa katika mikutano yetu ya pale *master parade* ya kule maskulini, walimu na hatua nyengine kubwa, basi jamii hii tutaikosea kama hatukufanya hivyo na wao baadae tutawakosa, kwa sababu udongo upatize ungali maji.

Mhe. Naibu Spika, niongeze katika kuona kwamba kamati ilitembelea sana katika Ofisi hizi na kujua athari ya madawa haya. Lakini niiulize kamati je, suala zima la uvutaji wa tumbaku hili tunaliweka wapi. Kwa sababu mchana tulipitisha hapa Sheria ya Chakula, Madawa na Vipodozi na vipi vipodozi vinavyoathiri na vipi vyakula vinavyoathiri. Je, hili suala la tumbaku tunaliweka wapi katika madawa ya kulevya, kamati walivyopita wameliona hili? Kwa sababu tumbaku nayo ni mojawapo kati ya vitu vinavyowaathiri vijana wetu au wananchi wetu. Tumbaku hii mvutaji wa sigara, wataalamu wanaochunguza masuala ya tumbaku wanasema kwamba yule mtu wa pili ndiye anayeathirika zaidi kuliko yule anayevuta, kwa sababu unaweza kuzalisha maradhi ya kensa, *pressure* na mambo mengineyo. Kwa hivyo, hili suala la tumbaku je, katika kamati zao waliliona hili. Kama waliliona watakapokuja naomba walitolee ufafanuzi ili wananchi waweze kulijua na wao baadae tujue ni hatua gani wanaweza kuchukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kuchangia katika ripoti hii kwenye ofisi ya Baraza la Mapinduzi. Kamati imeeleza kwamba walikwenda kuangalia Pemba kule Ofisi ya Baraza la Mapinduzi kwamba haina matatizo yoyote isipokuwa ni bajeti wanatekeleza shughuli zao. Lakini niulize je, kamati hii ilikwenda kutembelea, pale Ofisi walipo sasa hivi ambapo ilikuwa ni Ikulu ndogo ile ndipo walipo hivi sasa. Lakini kwa ninavyojua mimi kama ile Ofisi pale wamekaa kwa muda, lakini ofisi yao hasa ya Baraza la Mapinduzi ni Ofisi ambayo ilikuwa iko karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ambayo sasa hivi wanatumia Ofisi ya Baraza la Mji kwa muda, ile Ofisi ndio Ofisi yao hasa. Sasa sijui kama wameshaliwacha jengo lile. Kama ni hivyo, kule waliko kuna haja ya kubadilisha majengo na kujenga majengo ambayo yataweza kutumia nafasi ndogo, majengo ya ghorofa.

Mhe. Naibu Spika, vile vile kama jengo ni lile ambalo waliondoka pale, na wao waliondoka kwa kutaka kufanya matengenezo, lakini kwa sababu ofisi ya Baraza la Mji inafanya matengenezo, basi hawakupata pakukaa wakaenda kujiweka wao kwa kusogeza siku. Sasa kama Ofisi yao ndio ile basi naomba sana kule lile jengo halifai tena kuitwa ni Ofisi ya Baraza la Mapinduzi. Kile kiwanja ni kizuri na ni kikubwa. Kwa hivyo ni vyema kulijenga jengo la ghorofa ambalo litaweza kubeba Ofisi nyingi ambazo zitaweza kuzisaidia Ofisi za serikali kuondokana na kukodi. Kwa hivyo, nataka ufafanuzi kuhusu Ofisi ya Baraza la Mapinduzi, walioitembelea hasa ni ofisi ile wanayokaa hivi sasa au ni ile yao ya asili.

Mhe. Naibu Spika, mimi ni hayo tu ambayo nilitaka kuchangia katika ripoti hii, wenzangu mengi wameshayasema. Naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia juu ya mia, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Shehe Hamad Mattar nakushukuru sana. Mhe. Jaku Hashim Ayoub uliniomba dakika tano, naomba utumie dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru na bila kupoteza muda nichukue fursa hii kuchangia baadhi tu kidogo ya kero za mambo ya Muungano na hapa ndio pahala pale.

Mhe. Naibu Spika, hii Tanzania inaitwa Tanzania kwa kutokana na kuungana na Zanzibar. Lakini kuna mambo kadhaa wa kadhaa, wenzangu wameyazungumza. Nije kwenye chombo cha *TFF* cha mpira wa miguu. Suala hili nililizungumzwa mara kadhaa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano. Kuna migao inayopatikana karibu mitatu kutoka *FIFA*, kutoka *CAF* na mashindano yalikuwa yanaitwa *CHAN*. Ninachokijua mimi baada ya kujenga

Uwanja wa Gombani hakuna msaada tulioupata kutoka *TFF*, ndio ninachokijua mimi kwamba Uwanja wa Gombani katika mgao wetu Zanzibar tumepata Uwanja wa Gombani. Kisingizio kilichokuja ni kwamba wenzetu wanapeleka utaratibu wao wanaandaliwa wanapewa vitu lakini sisi nashangaa kwa nini hatushirikishwi. Nisipoteze muda. *(Makofi)*

Baada ya hapo, juzi Mhe. Naibu Spika, kumetokea kadhia sio ndogo katika Bandari ya Dar es Salaam na bado kidogo, chakula chetu kikubwa hapa ni chipsi na chipsi zinatokana na mbata mbatat, vimezuiwa mbatata zinataka kupimwa kwa gunia kupakiwa huku. Sasa hiki kitu gani kimekuwa mbatata zinataka kupimwa, lakini miaka yote huko nyuma hazijataka kupimwa. Kwa gunia ili upakie upime ulipie ushuru, mbatata vinatoka kwa ndugu zetu hawa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara wadogo wadogo wanachukua TV zao ndogo moja au mbili wakifika bandarini wananyang'anywa utawaonea huruma, wamejiajiri wale. Wakifika pale zinakamatwa mpaka zinaoza. Kuna Tume yetu ya Fedha ya pamoja iko wapi ile jamani, miaka mingapi imekutana Tume ya Fedha ya pamoja iko wapi, sijui imeishia wapi, sijui miaka mingapi imekutana, sikumbuki. Wazee tunakuwasaidieni msione kama tunapiga kelele hivi tunasaidia kuongoza 'hoi hoi nacho kilindo'. Tume hii imefikia wapi, kuna maamuzi gani.*(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, viongozi wetu alipokuwa madarakani Mhe. Rais Jakaya Kikwete alipokuwa akienda safari alikuwa anaondoka na kiongozi ijapo mmoja kutoka Zanzibar kuunga safari, uwiano huu ulikuwepo. Leo viongozi wameshakwenda safari sijui ngapi, sijui kama kuna kiongozi hata mmoja kachukuliwa, hii nimeshaizungumza Bungeni na nilielezwa kuna kiongozi mmoja atapata safari ya kwenda Canada, Waziri mmoja humu ndani sitaki kumtaja jina, baada ya kuzungumza Bungeni hiyo. Tanzania inatokana na Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuhusu uwakilishi wa Ubalozi nje, pamoja na Zanzibar kuwa ni ndogo lakini udogo wake ni nchi. Tumepiga kelele nafikiri Balozi wawili wameongezwa, ndio nikasema ile 'hoi hoi nacho kilindo'. Hizo ndio kelele tunazopiga sisi tukafanye kazi Bungeni. *(Makofi)*

Mwisho hizi kodi za mara mbili, alizungumza Mhe. Abdalla Maulidi Diwani. Mali ukiitoa Dar es Salaam unaikatisha *VAT* na ikifika hapa unakamatwa, hawa wafanyabiashara wataendelea au watarudi nyuma ni mtihani mkubwa. Leo mali inatoka Uganda, inayotoka Kenya, inayotoka Rwanda, inayotoka Zambia

ikaingia Dar es Salaam haina mateso, lakini mali ukaitoa Zanzibar ukaipeleka Bara utafikiri umepeleka unga. Sasa Muungano huu jamani una faida kwa upande mmoja tu. Sina nia ya kutaka kuuchafua Muungano hapana, Muungano ni muhimu na tuna uhitaji. Lakini sote tuneemeke, isiwe kwa upande mmoja tu, nipe nikupe. Wenzetu wana raslimali nyingi na kutokana na ukubwa wao. *(Makofi)*

Lakini leo mbatata nazo mwisho juzi zinataka kulipiwa kwa gunia. Mhe. Naibu Spika, hiki ni kitu cha aibu. Mali ikitoka Zanzibar ikiingia Dar es Salaam ni mvutano lakini ikitoka Uganda, Kenya, Rwanda haina mashaka. Sasa huu ni ubinadamu gani. *(Makofi)*

Mwisho nafikiri nimalizie kidogo na ndio pahala pake hapa Mfuko wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo sijui kuna utaratibu gani huu mwaka wa pili unakaribia jamani, tusaidieni hali ni ngumu majimboni. Tunajua maisha ukali wake, kama hazipo tupeni maneno mazuri, maneno mazuri nayo ni sadaka, tunaweza kustahamili, tumeshastahamili. Kama tayari ndio neema hiyo Alhamdulillah. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim, malizia.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Naibu Spika, naona umeshaniwashia taa. Nakushukuru sana.

Mhe. Naibu Spika: Sasa ni zamu ya Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora).

Mhe. Hassan Khamis Hafidh (Diaspora): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii jioni ya leo nahisi pia ni mchangiaji wa mwisho kwa leo kwa muda uliobaki.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nachukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Welezi kwa kuniamini, kadhalika na Wazanzibari wote kwa kumchagua Rais Dk. Ali Mohamed Shein kuongoza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, nitaanza kuchangia kwa kuanza katika ukurasa wa 3, kuhusu Tume ya Kitaifa ya Uratibu wa Udhibiti wa Dawa za Kulevya. Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ni Zanzibar, na sasa imekutwa na janga, janga lenyewe lote linasababishwa na madawa ya kulevya. Nitataja baadhi ya athari zilizokuwepo Zanzibar ambazo zinasababishwa na madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar kuna wizi mwingi. Wezi wengi ni watu wenye kutumia madawa ya kulevya. Zanzibar kuna mauaji mengi ya kukatwa mapanga na mambo yote yanasababishwa na watumiaji wa madawa ya kulevya. Mhe. Naibu Spika, udhalilishwaji wa watoto na wanawake wingi wao unasababishwa na watumiaji wa madawa ya kulevya. Pia Ukimwi Zanzibar unasababishwa na watumiaji wa madawa ya kulevya. Mambo mengi mabaya ya nchi yetu yanayofanyika kwa sasa hivi yanasababishwa na watumiaji wa madawa ya kulevya. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, la kushangaza na la kusikitisha tulipotembelea jela ya Zanzibar, tuliwakuta waliofungwa kwa kutumia unga, sio kwa kuleta wala kwa kusambaza unga, kwa kutumia unga wamefungwa watatu. Ndani ya jela ya Zanzibar Mhe. Naibu Spika, hakuna mletaji wala msambazaji unga. Naomba nirudie, Mhe. Naibu Spika, licha ya unga kuwa umejaa Zanzibar, lakini ndani ya jela ya Zanzibar hakuna mletaji wala msambazaji unga. Mhe. Naibu Spika, leo kilichonisikitisha dhidi ya ripoti hii ni mambo manne naomba niyataje, walioandika wameweka changamoto ziko nne. Ufinyu wa jengo la kutumia Tume ya Kitaifa, ufinyu wa bajeti ya Tume, ukosefu wa vyombo vya usafiri na kutomalizika kwa kesi, yaani hivi vyote Kamati inaiombea Tume. Mhe. Naibu Spika, bila ya kuuma maneno, naomba niseme maneno ya Kimapinduzi kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ili upewe tunzo iwe umefanya kazi nzuri ndio upewe tunzo. Mhe. Naibu Spika, kutokana na wingi wa unga Zanzibar, kutokana na wingi wa waleta unga Zanzibar wanaotusababisha athari, basi naiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujiamini kabisa hii Tume haijafanyakazi bado. Tume hii haijafanyakazi naomba ifutwe kwa sababu haina kazi inayoifanya wala kazi iliyoifanya, unga umejaa, unga mwingi Zanzibar na unatuletea athari nyingi katika maendeleo ya nchi hii. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, Tume hii haifanyikazi na inaendelea kulipwa pesa nyingi za wavuja jasho na wanaomba vitu vingi bila ya kufanyakazi. Naiomba Tume ifutwe badala yake Mhe. Naibu Spika, nguvu hizi na uwezo huu upelekwe kwa Wakuu wa Wilaya. Wakuu wa Wilaya waongezewe jukumu la kudhibiti kuleta na kutumia unga Zanzibar. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naamini nguvu hizi wakipewa wakuu wa Wilaya yetu jembe, wakipewa *task* hii wataifanya kwa umahiri na umakini na *outcome* yake itaonekana. Mhe. Naibu Spika, narudia tena Tume ya kudhibiti unga Zanzibar haijafanyakazi na badala yake unga unazidi kuletwa na wanaoleta wanajulikana, lakini wanafichwa kwa sababu ya kutoa labda kitu kidogo sijui Mwenyezi Mungu ndiye anayejua.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ukienda kwenye ukurasa wa 5 Tume ya Uchaguzi. Mimi Tume ya Uchaguzi naipongeza na nampongeza sana Mwenyekiti Mzee Jecha kwa kufanya uchaguzi mzuri na kuweza kumtangaza Hassan Khamis Hafidh kuwa Mwakilishi pamoja na Rais kwa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kadhalika ukienda ukurasa wa 6 kuhusu Wakala wa Serikali wa Uchapishaji. Mhe. Naibu Spika, Wakala wa Serikali wa Uchapishaji kwa kusikia wana mitambo mizuri na mipya lakini inasikitisha sana kwamba bado gazeti na vitu vyengine vya serikali vinachapishwa katika taasisi binafsi au vinachapishwa Bara. Mhe. Naibu Spika, naiomba serikali kwamba vitu hivi vichapishwe katika taasisi ya uchapishaji ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa sababu vyengine ni siri kubwa, vinavuja tunamtafuta aliyevujisha, kumbe *system* ya uchapishaji.

Mhe. Naibu Spika, ukienda ukurasa wa 8 utakuta Idara ya Kukabiliana na Maafa. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kuona Idara ya Kukabiliana na Maafa imekua inasubiri maafa yatokee ndipo wafanye kazi, wao kazi yao kusubiri maafa tu, imekuwa kama wachimba makaburi au *final director,* lakini sioni kwamba wana kazi nyengine, wanasema Waswahili "Kinga ni bora kuliko tiba", mambo yote matatu hapa ufinyu wa bajeti, ukosefu wa ghala la kuhifadhia vitu vya kusubiri maafa, sijui kitu gani, wanasubiri maafa tu wao. Mhe. Naibu Spika, lazima tuibadilishie *system* iwe ina jukumu jengine la kukinga, sio la kuombezea na kusubiri maafa, iwe inakinga maafa yasitokezee. Lazima iwe inafanya *protection and management of disaster* inapotokezea, isiwe inasubiri maafa tu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukurasa wa 9 kuhusu Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Muungano. Mhe. Naibu Spika, naiomba sana Idara hii iendelee kufanyakazi zake vizuri, bado unakuta uratibu huu, unaweza kukuta kwenye *delegation* nzima tena ya chombo cha Muungano, lakini hakuna Mzanzibari hata mmoja, sitaki kutoa ushahidi. Lakini bado kwenye taasisi za Muungano uratibu nauomba ufanyike vizuri, kwa sababu Tanzania ni yetu sote sio ya upande mmoja.

Mhe. Naibu Spika, nikienda katika ukurasa 10 kuhusu Ofisi ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam. Mhe. Naibu Spika, inasikitisha kweli kuona kuna Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Dar es Salaam, lakini Ofisi ile kazi yake ni kusubiri mtu kama mume wake au mke wake kahamishiwa Bara, tena apelekwe kwenye Ofisi ile, licha ya kuwa Idara ile au Ofisi ile kazi yake ni kufanya *co-ordination* ya sehemu zenye *issues*. Idara ile au taasisi ile iko pale

kupelekwa watu aidha mkewe au mumewe kahamishiwa Bara, tena ndio apelekwe kwenye Idara ile, imejaa watu wasiokuwa na kazi pale, kwa sababu ya waume zao au wake zao wako Bara ndio wako pale wanasubiri. Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kufanya kazi kama hivyo kuwalipa watu pesa wakakae kuwasubiri waume zao wako Bara, au wakakae kuwasubiri wake zao wako Bara, haiwezekani. Tunaiomba ile Idara iwe taasisi inayoiletea tija sio kusubiri wake zao au waume zao waliopelekwa Bara.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 12 unazungumzia walemavu. Mhe. Naibu Spika, hawa...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wetu umekwisha, nimepewa taarifa kwamba saa ambayo ninaitizama mimi, saa ile iko nyuma. Kwa hivyo, ina maana kwamba muda tayari umeshapita.

Waheshimiwa Wajumbe, kwanza niseme tu kwamba bado nina wachangiaji wanafika 22 ambao wameomba kuchangia. Tutaendelea kesho tukijaaliwa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, lakini sasa hapa tumefikia mwisho kwa leo na ninaahirisha kikao hadi kesho asubuhi saa 3:00.

(Saa 1:48 usiku kikao kiliahirishwa mpaka tarehe 22/02/2017 saa 3:00 za asubuhi)